**6 FEBRUARI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

**Kikao cha Sita – Tarehe 6 Februari, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**MHE. MARTHA F. MARIKI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2023

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, TAMISEMI, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso.

Na. 87

**Ujenzi wa Vituo vya Afya Kata ya Ipwaga na Ilangu – Katavi**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia ujenzi wa Vituo vya Afya vya Kata ya Ipwaga na Ilangu vilivyoanza kujengwa na wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya Kata ya Ipwaga kilianza kutoa huduma kwa ngazi ya zahanati baada ya kusajiliwa. Mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ilianza taratibu za kuipandisha hadhi kuwa Kituo cha Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ilipokea shilingi milioni 90 fedha kutoka mpango maalum wa kuboresha makazi ya wakimbizi, *Comprehensive Refugee Response Framework (CRRF)* na kuanza ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje. Mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali ilitoa shilingi milioni 50 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali kupitia mapato ya ndani ya

Halmashauri imetenga shilingi milioni 40 na imekwishatoa shilingi milioni 20 kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la wagonjwa wa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa awamu kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na ukamilishaji wa vituo vya afya vya Ipagwa na Ilangu katika Halmashauri ya Tanganyika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Kwa kuwa, ujenzi wa Kituo cha Afya cha Ipwaga unachukua muda mrefu na kuwafanya wananchi wasipate huduma ile iliyokusudiwa. Je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka fedha kwa mwaka wa fedha ujao ili kituo kile kiweze kukamilika? *(Makofi)*

Swali la pili, Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika ina upungufu mkubwa sana wa Watumishi hasa kwenye kada ya afya. Kila kituo cha Afya kinachokuwa kimekamilika wanahamisha baadhi ya watumishi ama kutoka kwenye kituo kingine kwenda kituo kingine, matokeo yake huduma zinakuwa duni kwa sababu ya ukosefu wa rasilimali watu.

Je, ni lini mtapeleka watumishi kwenye kada ya afya waweze kufanya shughuli kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali imepeleka fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya, zahanati lakini pia Hospitali ya Halmashauri katika Wilaya ya Tanganyika, Serikali

inatambua kwamba bado kuna uhitaji wa Ujenzi wa Kituo cha Afya cha Ipwaga na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari kimeishaingizwa kwenye kata za kimkakati kwa ajili ya Ujenzi wa Kituo cha Afya hicho ili kusogeza huduma za afya karibu na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimhakikishie tu kwamba mwaka ujao wa fedha tulitoa fursa hapa Waheshimiwa Wabunge, kutoa Kata moja ya kipaumbele kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya. Kwa hivyo, namuomba Mheshimiwa Mbunge kama hii ni kata ya kipaumbele basi tuchukue tuingize kwenye bajeti ya mwaka ujao katika vile vituo vya afya vya Majimbo ili kiweze kupelekewa fedha kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili kuhusiana na upungufu wa Watumishi. Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanya kazi kubwa sana na imeweka kipaumbele cha kipekee katika ajira za watumishi wa sekta ya afya. Kwa muda wa miaka hii miwili na nusu tayari jumla ya watumishi 18,848 wa sekta ya afya wameajiriwa na kupelekwa kwenye vituo kote nchini vikiwemo vituo hivi vya Tanganyika na nimhakikishie tutaendelea kufanya hivyo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Francis.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Ilunda na Kituo cha Afya cha Gumanga vimebakisha kiasi kidogo sana cha fedha na vifaatiba tayari vimekwenda; Serikali ina mpango gani kutoa hizo fedha ili kuweza kumalizia na hivyo vifaatiba viweze kuingizwa kwenye vituo hivi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninawapongeza Wananchi wa Jimbo la Mkalama kwa kupata vituo vya afya viwili. Kituo cha Afya cha Idunda pamoja na hiki cha Muhanga ambavyo vimekamilika lakini bado mambo madogo madogo. Niwahakikishie kwamba tayari Mheshimiwa Rais, ameishapeleka fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba kwenye vituo vya afya vyote vilivyokamilika lakini pia kwenye zahanati zote zilizokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimuombe Mheshimiwa Mbunge na nimuelekeze kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mkurugenzi wa Halmashauri hii ya Mkalama kuhakikisha wanatenga fedha kutoka mapato ya ndani kumalizia kazi ndogo ambazo zimebaki ili vifaa vikija wananchi waanze kupata kupata huduma haraka iwezekanavyo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyanya, ajiandae Mheshimiwa *Advocate* Olelekaita.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa, kuna siku nilishajibiwa kwamba Kituo cha Afya cha Kihagara kingeweza kupewa wodi kwa kuwa hakina kabisa lakini mpaka sasa bado haijatekelezwa. Je, ni lini Serikali itatekeleza suala hili la kujenga wodi moja angalau katika Kituo cha Afya Kihagara? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli tulitoa *commitment* hiyo ya kujenga wodi angalau moja lakini pia na wodi zingine katika Kituo cha Afya cha Kihagara katika Jimbo la Nyasa na safari ni hatua. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tunatafuta fedha na fedha zikipatikana mapema iwezekanavyo tutapeleka kwa ajili ya ujenzi wodi hiyo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *advocate*.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri mlituandikia barua hapa kwa ajili ya kutoa kituo cha afya kila Jimbo lini zinakuja? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha inasogeza huduma za afya karibu na wananchi wa Majimbo yote likiwemo Jimbo la Kiteto kwa Mheshimiwa Olelekaita. Ni kweli kwamba tulipitisha fomu hapa kwa Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya kujaza kituo cha afya kimoja kwa kila Jimbo cha kimkakati. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Olelekaita kwamba mipango hiyo inaendelea na tunatarajia kwenye mwaka wa fedha ujao fedha hizo zitapatikana kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya kikiwemo hiki cha Kihagara, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Anatropia.

Na. 88

**Idadi ya wanawake wanaoshindwa kumudu *delivery kit***

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza: -

Je, wanawake wangapi wameshindwa kumudu *delivery kit* na kupewa vifaa hivyo na Hospitali au Kituo cha Afya husika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutoa huduma za afya kwa wajawazito wanaojifungua kwa kuzingatia Sera ya Afya ya mwaka 2007. Sera hii imeainisha makundi maalum ya matibabu kwa msamaha ikiwemo huduma ya wajawazito na kujifungua. Katika kipindi cha miaka miwili (2022 na 2023) jumla ya wajawazito 2,707,098 walijifungua kwenye vituo vya kutolea huduma ngazi ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya huduma inayotolewa katika vituo ni kitita cha kujifungulia *(delivery kit)* kwa wajawazito wasiyomudu. Katika kipindi cha mwaka 2022 na 2023 jumla ya wajawazito 10,829 walipewa vifaa vya kujifungulia katika vituo vya huduma za afya ya msingi na kuwawezesha kupata huduma hiyo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Tukubaliane kwamba suala la kujifungua haipaswi kuwa kati ya kifo na kupona lakini Tanzania inaonekana kuwa ni moja kati ya nchi tano chini ya Jangwa la Sahara inayoongoza kwa vifo vya wajawazito na vifo vingi vinasababishwa na magonjwa kuambukiza *infectious disease,* ambayo inapatikana wakati wa kujifungua kwa maana ya kukosa maji na vitu vyenye usafi.

Je, ni kwa nini hizi *delivery kit* zisitolewe bure kwa wajawazito wote ili kupunguza *rate* ya *infectious diseases* wakati wanawake wanajifungua? *(Makofi)*

Swali la pili, ni kwa nini kusitengwe fungu maalum, kuwepo na *ring fenced fund* ambayo itakuwepo *specific* kwa ajili ya kununua na kuwapatia wakinamama *delivery kit* ili kuweza kuokoa maisha ya akina mama Nyankantutu, akinamama wa Nkwenda, akinamama wa Itera na maeneo mengine kote ambapo wakinamama wanakufa wanapojifungua kwa ajili ya kukosa hivi vifaa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anatropia Theonest, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi yetu suala la kujifungua na kifo siyo mambo kwa sasa ambayo yako karibu kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge. Ikumbukwe mwaka 2016 kurudi nyuma vifo vya wajawazito vilikuwa 556 kati ya vizazi hai laki moja, leo tunaongea baada ya jitihada za Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kuweka kipaumbele cha ujenzi wa vituo vya afya, zahati, vifaatiba na madawa, vifo vimepungua kutoka 556 mpaka 104 katika vizazi laki moja. Kwa hiyo, unaweza ukaona namna ambavyo kasi ya kupungua kwa vifo vya wajawazito ilivyo kubwa kutoka 556 katika vizazi laki moja mpaka 104 na kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa *investment* hii kubwa ya Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), katika vituo vya afya ambavyo tunasema hapa kila siku vinakwenda vifaatiba na watumishi tuna uhakika Tanzania itakuwa ni miongoni mwa nchi ambazo zina vifo vichache sana na kwa sasa kwa afya tuko katika hatua nzuri sana kupunguza vifo vya wajawazito.

Swali lake la pili kuhusiana na ku-*ring fence,* kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba *delivery kit* zinazotolewa, zinatolewa bure kwa wajawazito wote, kwa sababu wanazikuta kwenye zahanati, wanazikuta kwenye vituo vya afya na hospitali zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu suala la kujifungua nina uhakika Mheshimiwa Mbunge alishapata baraka ya kupata mtoto linatokea wakati wowote anaweza akawa yupo nyumbani, anaweza akawa yupo katika shughuli zake akahitaji kujifungua wakati wowote kabla hajafika kwenye vituo, ndio maana tumetoa maelekezo ya kuwa na angalau akiba ya *delivery kit* kule nyumbani ili likitokea lolote tusiweze kumpoteza mama mjamzito.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo siyo kwamba *delivery kit* zinauzwa wote wanapata bure lakini tumewepa *emergency*, *preparedness* angalau uwe na kitu cha kuwasaidia *in case* wanahitaji kupata huduma hiyo na fedha hizi zote ziko *ring fenced*. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mipango.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongeza kidogo kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sababu Mheshimiwa Mbunge ameeleza kwamba nchi yetu ni miongoni mwa nchi ambazo tupo chini sana, tuna vifo vingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba kwa takwimu ambazo tunazo kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri, lengo la mpango wa miaka mitano ifikapo mwaka 2025 ilikuwa tuwe tumepunguza kufikia vifo 265 lakini tunazungumzia miaka miwili kabla tumeishapunguza vifo 104. Kwa hivyo tumekamilisha lengo kabla ya muda na imeifanya Tanzania katika Ukanda wa Afrika Mashariki kuwa ni nchi yenye vifo vichache vya wajawazito katika nchi yetu katika ukanda huu, kwa hivyo hii habari nilitaka niiweke vizuri hii rekodi ikae vizuri kulikoni kusema kwamba nchi yetu iko katika hali hiyo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia umesikia? Acha ku-*google* hovyo hovyo bila kujua taarifa sahihi. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Deus Clement Sangu, kwa niaba? Kwa niaba. *(Kicheko)*

Na. 89

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Ilemba - Kwela**

**MHE. AIDA J. KHENANI K.n.y. MHE. DEUS C. SANGU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Ilemba – Kwela?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Jimbo la Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Zahanati ya Ilemba iliyopo Kata ya Ilemba ilisajiliwa mwaka 2005 na inatoa huduma ya ngazi ya zahanati. Zahanati hiyo imejengwa katika eneo lenye ukubwa wa ekari mbili na nusu. Eneo hilo halikidhi ukubwa unaohitajika kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya katika maeneo ya vijijini ambao ni angalau ekari tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga imeanza utaratibu wa kutafuta eneo katika Kata ya Ilemba ili ujenzi wa kituo cha afya ufanyike katika kata hiyo. Serikali imeendelea kutenga fedha na kupeleka fedha katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga kwa ajili ya kuboresha huduma za afya ikiwemo ujenzi wa Kituo cha Afya Laela ambacho katika mwaka wa fedha 2023/2024 kimetengewa fedha za Mfuko wa Benki ya Dunia, shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali na kweli ni matumaini makubwa ya watu wa Jimbo la Kwela.

Kwa kuwa, bajeti inayoendelea kutekelezwa sasa, Serikali ilihaidi kujenga Kituo cha Afya Laela katika Jimbo la Kwela. Ningependa kujua ni lini ujenzi huo utaanza katika Kata ya Laela?

Swali la pili, Kata ya Korongwe ni miongoni mwa kata korofi ni lini mtaanza kujenga Kituo cha Afya Korongwe? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aida Khenani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika mwaka huu wa fedha 2023/2024 Serikali imeainisha kata za kimkakati kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya kwa fedha za Benki ya Dunia. Kata hii ya Laela ni miongoni na ndiyo maana kwenye majibu yangu ya msingi nimesema imeishatengewa milioni 500 tayari timu za Ofisi ya Rais, TAMISEMI zimeishafika katika maeneo hayo zinafanya tathmini na baada ya hapo itafanyika *Environmental Impact Assessment* na kuanza ujenzi mara moja. Kwa hiyo, tunatarajia mapema ndani ya miezi miwili, mitatu tutaanza hatua za awali za ujenzi katika vituo hivi vyote vya Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kweli Kata ya Korongwe ambayo ipo katika mazingira magumu kijiografia lakini ina idadi kubwa ya wananchi, Mheshimiwa Mbunge ameishaiwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI, nikuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tumeishaweka kwenye mpango tunatafuta fedha zikipatikana tutakwenda kuanza ujenzi wa kituo hiki cha afya, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Minza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itakamilisha Ujenzi wa Kituo cha Afya Kiloleli katika Wilaya ya Busega? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Minza, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafahamu kwamba Kituo cha Afya Kiloleli kinatoa huduma kwa ngazi ya kituo cha afya lakini ina upungufu wa baadhi ya miundombinu muhimu. Tayari

tumeshamwelekeza kwanza Mkurungenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega lakini nimshukuru Mheshimiwa Mbunge wa Busega pia kwa sababu amekuwa akifuatilia kwa karibu kushirikiana na Mheshimiwa Minza, sasa niombe niwahakikishie tu kwamba tayari tumeiweka kwenye mpango na fedha ikipatikana tutakwenda kujenga miundombinu inayopungua ili tutoe huduma bora zaidi kwa wananchi, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kata za Lahoda na Kata za Jangalo ni kata za mpakani na zina idadi kubwa sana za watu; je, ni lini sasa Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina kata zaidi ya 3,500, pia tumejenga tayari vituo vya afya zaidi ya 466 ndani ya miaka hii miwili ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na moja na kigezo ni idadi wa watu, umbali wa kituo kutoka kituo cha jirani pia na aina ya jiografia katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu umuhimu wa vituo vya afya katika Jimbo la Chemba, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tumepokea taarifa hii tutakwenda kuifanyia kazi kuona uwezekano wa kupata fedha na kufanya tathmini kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya katika kata hizi ulizozitaja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Serikali ilituahidi kutujengea Kituo cha Afya Masama Kati na ikatuambia tuanze kwa nguvu za mapato ya ndani na nguvu za wananchi. Wananchi wamejitolea na mapato ya ndani tumeweka; je, ni lini Serikali itatuletea fedha kwa ajili ya kumalizia Kituo cha Afya Masama Kati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mafuwe kwamba kwanza fedha za Serikali ni pamoja na fedha za mapato ya ndani. Kwa hiyo, kwamba ahadi ya Serikali ya kujenga Kituo cha Afya cha Masama Kati tayari imeanza kutekelezwa na Serikali kwa kutumia fedha za mapato ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kituo kinakamilika kwa kuunganisha nguvu za fedha ya Serikali Kuu na fedha za mapato ya ndani. Nitumie fursa hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kumuelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Hai kuhakikisha wanatoa kipaumbele kwenye 60% ya miradi ya maendeleo mwaka ujao wa fedha, kutenga fedha ya kutosha kwa ajili ya kujenga kituo cha afya hiki na Serikali itaona namna na kutafuta fedha kwa ajili ya kuongeza nguvu, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, je, ni lini Serikali itajenga majengo ya *mortuary,* maabara na upasuaji kwenye Kituo cha *OPD* Himo ambacho kilipandishwa hadhi kuanzia mwaka 2020? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kimei, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tulishaainisha Kituo cha Afya cha *OPD* Himo miongoni mwa vituo vya kipaumbele ambavyo vina miundombinu michache ikiwemo maabara na jengo la upasuaji na hivi sasa tupo kwenye hatua ya kutafuta fedha, ili tuende kujenga miundombinu hiyo.

Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo hilo kwamba fedha itakapopatikana na tupo kwenye hatua nzuri, tutakwenda kuboresha miundombinu kwenye vituo vyote vyenye miundombinu pungufu kote nchini, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Kilave, Mbunge wa Temeke.

Na. 90

**Kukarabati masoko chakavu ya *Sterio* na Tandika - Temeke**

**MHE. DOROTHY G. KILAVE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati masoko chakavu ya *Sterio* na Tandika – Temeke?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dorothy George Kilave, Mbunge wa Jimbo la Temeke, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uchakavu wa Masoko ya Tandika na *Sterio* katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke. Aidha, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke katika mwaka wa fedha 2023/2024 imetenga shilingi milioni 800 kwa ajili ya ukarabati wa masoko hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi cha shilingi milioni 25.2 tayari kimetolewa kwa ajili ya kufanya tathmini na ukarabati wa vyoo katika Soko la *Sterio*. Ukarabati wa masoko hayo unatarajiwa kuanza mwezi huu wa Februari, 2024 na kukamilika mwezi Juni, 2024.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali pamoja na yote hayo, lakini kiasi cha shilingi milioni 25.2 zimetengwa kwa ajili ya Soko la *Sterio* kwa ajili ya tathmini; je, ni lini sasa tutatenga fedha hizo hizo kwa ajili ya tathmini ya Soko la Tandika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, je, hamuoni iko haja sasa ya wafanyabiashara wa maeneo hayo ya masoko haya mawili, kuwekwa na wao wakae pamoja na Manispaa yetu, waweze kutoa na wao jinsi gani ya kuweza kutengeneza masoko haya, kwa sababu wamewekwa nje sana na masoko yanakuja kutengenezwa. Kwa kuwa wao ndiyo wanatumia yale masoko wanajua ni jinsi gani ya kuweza kufanya vizuri zaidi. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kilave, hili la kwanza la shilingi milioni 25.2 nayo kutengwa kwa ajili ya Soko la Tandika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke imetenga shilingi milioni 800 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa masoko haya mawili. Hivyo basi nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kumuelekeza Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke kuhakikisha katika bajeti aliyotenga ya masoko haya mawili, basi shilingi milioni 25.2 vilevile inakwenda kwa ajili ya kufanya tathmini na ukarabati wa vyoo katika Soko la Tandika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la kuhusishwa kwa wafanyabiashara katika mipango hii ya ukarabati na ujenzi wa masoko haya; vilevile, nitumie nafasi hii mbele ya Bunge lako Tukufu kumuelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kuweza kukaa na wafanyabiashara hawa na kupitia michoro ambayo imekusudiwa kwa ajili ya ujenzi wa

masoko haya na waweze kukubaliana ni namna gani maboresho haya yaweze kufanyika, ili yaendane na shughuli ambazo wanafanya hao wafanyabiashara katika maeneo hayo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kisangi, ajiandae Mheshimiwa Tarimba, ajiandae Mheshimiwa Sophia.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali kla nyongeza.

Je, Serikali ina mpango gani sasa kukarabati Soko la Mabibo katika Halmashauri ya Ubungo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kisangi juu ya ukarabati wa Soko la Mabibo, nichukue nafasi hii tena kumtaka Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kuweza kufanya tathmini juu ya ukarabati unaohitajika kama alivyosema Mheshimiwa Kisangi, lakini vilevile waweze kutenga katika bajeti zao za mapato yao ya ndani kwa ajili ya ukarabati wa soko hili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani, naomba Mheshimiwa Naibu Waziri atupelekee salamu za wananchi wa Kinondoni kwa Mheshimiwa Rais kwa kutuletea shilingi bilioni nane na kutujengea soko kubwa pale Tandale chini ya usimamizi wa Meya wa Kinondoni Bwana Songoro na Mkurugenzi wake Bi. Hanifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu; yapo masoko chakavu sana katika Jimbo la Kinondoni kama vile pale Makumbusho, Kinondoni, Kata ya Ndugumbi, Kata ya Hananasif na Kata ya Kijitonyama; je, Serikali iko tayari kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kuhakikisha kwamba masoko haya sasa yanakwenda kukarabatiwa kabla hata ya Uchaguzi Mkuu unaokuja? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tarimba juu ya uchakavu wa masoko yaliyoko ndani ya Jimbo lake la Kinondoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tayari kupitia Mpango wa *TACTIC* imeanza kupeleka fedha katika majiji na manispaa mbalimbali kwa ajili ya kuweza kufanya *feasibility study.* Tayari wale waliokuwa kwenye *tier 1* wameshapelekewa fedha, kwa ajili ya kuanza kutangaza kazi zile za ujenzi inafuata *tier 2* ambayo inaenda kwenye manispaa sasa, ikiwemo Manispaa ya Kinondoni kwa ajili ya kuweza kupata fedha za ujenzi na ukarabati wa masoko mbalimbali ambayo wanaamua wao, tukirudi kwenye dhana nzima ya *D by D* maamuzi yanafanyika na halmashauri yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimtake Mheshimiwa Tarimba kukaa na Kamati yake ya *Finance* kuweza kuamua na Baraza lake la Madiwani ni maeneo gani ambayo wanayapa kipaumbele katika ukarabati na ujenzi wa masoko haya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri, Soko la Kiwira ni soko kubwa sana linalozalisha na linasaidia sana wanawake wanaofanya baishara pale; ni lini, Serikali itaongeza nguvu kwa Halmashauri ya Rungwe kuweza kujenga soko lile kwa faida ya Wanawake wa Rungwe? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwakagenda, juu ya ujenzi wa Soko la Kiwira, nimtake Mkurugenzi wa Halmashauri

ya Wilaya ya Rungwe kuweza kufanya tathmini na kuona kile ambacho iinahitajika katika kuboresha soko hili la Kiwira katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe na kisha kuweza kuitenga katika bajeti ya mapato yao ya ndani waanze ukarabati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile wanaweza wakaomba *support* kutoka Serikali Kuu na kuona ni wapi ambapo Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaweza ikaweka katika mipango yake na kuweza kuwasaidia kuboresha soko hili la Kiwira.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa tena hii nafasi.

Mheshimiwa Rais aliposimama Tengeru mara ya mwisho kusalimia wananchi, aliahidi kutukarabatia Soko la Tengeru ambalo ni muhimu sana kwa uhai wa Halmashauri ya Meru; je, Serikali imejipangaje kutekeleza hiyo ahadi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Pallangyo, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba ahadi zote za viongozi wetu wakuu ikiwemo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinatimizwa. Hivyo basi, tutakaa na Mheshimiwa Mbunge kuweza kuona katika mipango yetu ndani ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tumejipanga vipi kwa ajili ya kuweza kupeleka fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimtoe mashaka, ahadi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni maelekezo kwetu sisi wasaidizi wake.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo.

Na. 91

**Ujenzi wa madaraja kuunganisha Mbagala na Mkuranga**

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO** aliuliza: -

Je, lini Mbagala na Mkuranga zitaunganishwa kwa kujenga madaraja ya Videte, Mbagakwalu, Churwi, Tabowa na Majimatitu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Jimbo la Mbagala kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Serikali ni kuziunganisha Wilaya za Temeke na Mkuranga mpaka sasa maeneo matatu ya Kilwa, Tambani na Rufu Nampombo yameunganishwa kwa madaraja/makalavati na yanapitika kwa mwaka mzima. Katika jitihada za kuendelea kuwaunganisha wananchi wa Wilaya hizi mbili Serikali imepanga kuboresha kwa kujenga madaraja/makalavati ya Churwi, Tabowa na Majimatitu kupitia Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es salaam *(DMDP)*. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa barabara ya Kilwa hasa eneo la Kokoto mpaka Kongowe lina msongamano mkubwa sana wa magari; je, Serikali ina mapango gani wa dharura wa kuyakarabati madaraja hayo ili ipatikane barabara za michepuko kuondoa msongamano katika barabara hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kukarabati vivuko na madaraja yote yaliyo katika Jimbo la Mbagala kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chaurembo, hili la kwanza la kuweza kutengeneza njia za mchepuko kutoka kwenye Barabara ya Kilwa ili kuweza kuondoa msongamano ule uliokuwepo; nilijulishe Bunge lako Tukufu hili na Mheshimiwa Chaurembo kwamba Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tayari alikwishatoa maelekezo kwamba ile barabara inayotengenezwa ya *BRT* iweze kupanuliwa na kupelekwa umbali mpaka Vikindu. Hivyo basi, katika maeneo haya ambayo ameyataja Mheshimiwa Chaurembo ya Kokoto na maeneo mengineyo nayo barabara hii itakuwa imepanuliwa ili kuondoa msongamano wa magari ambayo yanapita katika barabara ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la tathmini kuweza kufanyika kwa ajili ya mpango wa dharura; nimhakikishie Mheshimiwa Chaurembo ya kwamba tathmini imefanyika hadi kufikia mwisho wa mwezi wa Januari na hivi sasa kuna fedha ambayo imeombwa kwa wenzetu wa Wizara ya Fedha kwa ajili ya kuweza kuanza ukarabati wa maeneo yale ambayo yameathirika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa Jiji la Dar es Salaam, madaraja makubwa ambayo yalikuwa yameathirika zaidi ni saba na nimjulishe Mheshimiwa Mbunge ya kwamba katika madaraja saba ambayo yapo chini ya *TARURA*, madaraja matano tayari yalikuwa yamekwishatengenezwa kwa ajili ya kuweza kuwa yanapitika kwa wakati wote, mawili yametengenezewa vivuko vya muda mfupi na pale ambapo tutazidi kupokea fedha kutoka kwa wenzetu wa Wizara ya Fedha tutaendelea kukarabati maeneo mengine ambayo ni korofi ikiwemo katika Jimbo la Mheshimiwa Chaurembo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata ya Uru Kusini kuna kituo cha afya kinajengwa cha zaidi ya shilingi bilioni moja, lakini hakuna barabara ya kuelekea maeneo hayo; je, ni lini Serikali itajenga barabara kutokea Mawela Kanisani kupitia Kituo cha Walemavu kufika katika kituo hicho? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Njau, nimtake Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Kilimanjaro kuweza kuhakikisha anafanya tathmini ya barabara hii ya Mawela Kanisani, kule Uru na kuona ni namna gani tunaiweka katika mipango yetu ya bajeti ambayo inakuja ya mwaka 2024/2025. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwenye Kata ya Kisangasa kuna daraja ambalo linaunganisha Kijiji cha Kisangasa ambapo ng'ambo ya pili ndipo ambapo huduma za kijamii kwa maana ya mahakama, shule ya msingi na sekondari, lakini hivi ninavyozungumza muda huu daraja lile limekatika na huduma hamna kule; je, Mheshimiwa Naibu Waziri, uko tayari kutoa maelekezo ili kivuko kile kiweze kurejeshwa? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kigua juu ya Daraja hili la Kisangasa ambalo limekatika na kuweza kuondoa huduma kwa wananchi kwenda kwenye maeneo muhimu kama Mahakama na kadhalika, nitumie nafasi hii mbele ya Bunge lako

Tukufu kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kumuelekeza Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Tanga kuweza kufika katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi mara moja na kuweza kufanya tathmini katika eneo hili la Kisangasa na kuweza kuhakikisha kwamba wananchi wanaopata huduma hata kwa kuweka kivuko cha muda ili wananchi waweze kuendelea na shughuli zao za kiuchumi za kila siku. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Malleko; kwa niaba Mheshimiwa Raymond.

Na. 92

**Sera ya Uwekezaji nchini**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND K.n.y. MHE. ESTHER E. MALLEKO** aliuliza: -

Je, upi mpango wa Serikali kubadili Sera ya Uwekezaji iliyopitwa na wakati ili kuwavutia wawekezaji nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ipo katika mchakato wa kuhuisha Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya mwaka 1996 ili iendane na mazingira ya sasa. Tayari Rasimu ya Sera Mpya na mkakati wa utekelezaji imeshaandaliwa na sasa inaingizwa katika mchakato wa maamuzi ndani ya Serikali, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Sera hiyo itawasaidiaje wananchi wa Tanzania walio nje kuja kuwekeza nyumbani kwao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa maeneo ya uwekezaji yalikuwa yameshatengwa ikiwemo Hai, Mkoani Kilimanjaro na Mashetuzi; je, jambo hilo likoje? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Raymond, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa *diaspora* kwa maana ya Watanzania waliopo nje ya nchi, tayari Serikali imesharidhia kuwa na ile hadhi maalum ambayo itawapa nafasi ya kuja hapa Tanzania kuwekeza kama Mtanzania mwingine, wanapata haki nyingi ambazo tumeshapitisha kwa hiyo hiyo changamoto imeshaondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo swali la pili kuhusu maeneo ya Hai na mengine kwa maana ya uwekezaji tutayafuatilia, muhimu ni kwamba Halmashauri husika ni muhimu ziweze kutenga ardhi kwa ajili ya uwekezaji ili wawekezaji waweze kufanya hiyo kazi, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Kasalali Mageni.

Na. 93

**Ujenzi wa Kituo cha Ufundishaji wa Michezo Malya**

**MHE. NG'WASI D. KAMANI K.n.y. MHE. KASALALI E. MAGENI** aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa Kituo cha Ufundishaji wa Michezo katika Chuo cha Michezo Malya utaanza kwa kuwa mkataba ulishasainiwa?

**NAIBU SPIKA:** Sasa ungesema kwa niaba, haya Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, Mbunge wa Sumve lililoulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukufahamisha kuwa Mkataba wa Ujenzi wa Mradi wa Kituo cha Ufundishaji wa Michezo Malya ulisainiwa tarehe 6 Julai, 2023 na kukabidhiwa kwa mkandarasi anayejulikana kwa jina la *China Railway Jianchang Engineering (East Africa Ltd.)* tarehe 2 Desemba, 2023. Mshauri Mwelekezi wa Mradi huu ni *ARU Built Environment Consulting Company Ltd*. kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi, Dar es Salaam. Utekelezaji wa mradi umeanza tarehe 16 Desemba, 2023 baada ya siku 14 za maandalizi *(mobilization)* baada ya kukabidhiwa na unatarajiwa kukamilika tarehe 15 Disemba, 2024.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ng'wasi.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza ningependa kushukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, ni kweli mpaka sasa tunavyozungumza Mkandarasi yupo *site*, ameshatipoti Halmashauri utaratibu wa mwanzo umeshaanza na tayari amekwishaomba fedha za awali kwa ajili ya kuanza mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina swali la nyongeza isipokuwa napenda kuishukuru Serikali na kumshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu ametekeleza ahadi yake tena kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi letu pekee na ombi la wananchi wa Sumve na Wana-Mwanza kwa ujumla ni kuomba kwamba basi Serikali iangalie itoe fedha hii kwa wakati ili mradi huu uweze pia kukamilika kwa wakati na Wanasumve waweze kunufaika nao, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nchi yetu imebarikiwa kuwa na vipaji vya michezo mbalimbali ambavyo vimekuwa haviendelezwi na hivyo kupelekea kuzima ndoto za vijana hawa pia kuikosesha nchi yetu fursa za kiuchumi na kuweza kufanya vizuri kwenye ngazi za Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu; ni lini Serikali itaanzisha shule maalum za michezo kwa ngazi ya msingi na sekondari, ili kuweza kukuza vipaji hivi na kuliletea Taifa letu uchumi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko ni kwamba, kwa sasa Serikali mpango ilionao ni kujenga shule mbili za michezo kwenye kila mkoa, shule 56 kwa mikoa yote ya Tanzania Bara; na mpango huo umeshaanza na kwa sasa tumeanza na shule tisa ambazo ziko mikoa tofauti tofauti kwa ajili ya shughuli hiyo. Hii ya Malya tunafundisha wakufunzi wafundishaji wa shughuli za michezo ambao wanakwenda kwenye shule hizi 56 na hii ni kwa kuanzia tu. Tuna mpango wa kuhakikisha kwamba, tunakuwa na shule ya michezo kwenye kila Wilaya ya nchi hii, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya, Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo, Mheshimiwa Asya Sharif Omar.

Na. 94

**Kudhibiti ujenzi holela katika miji**

**MHE. ASYA SHARIF OMAR** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti ujenzi holela katika miji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Asya Sharif Omar, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa kuna ujenzi holela licha ya uwepo wa sheria zinazoweka masharti ya ujenzi katika miji yetu hapa nchini. Chanzo cha ujenzi holela ni pamoja na ukuaji wa kasi wa miji yetu kutoka kwenye ngazi za vijiji hadi kuwa miji midogo kutokana na shughuli za kibinadamu hasa shughuli za uzalishaji kama kilimo, madini, uvuvi na hata maeneo yaliyopitiwa na miundombinu bora kama barabara za lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na sababu nilizozieleza hapo juu zinazosababisha ukuaji wa haraka wa miji yetu hapa nchini unaochangia kwa kiasi kikubwa ujenzi holela. Serikali kupitia Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na mamlaka nyingine tumekuja na mikakati ya kupima nchi nzima maeneo yote hadi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, Wizara inaendesha Kampeni ya kupima maeneo ya vijiji katika mpango wake wa matumizi bora ya ardhi na kwa maeneo ya miji, halmashauri zetu kwa pamoja na wizara yetu tunapima maeneo yote ya miji. Huko tunayo miradi kama urasimishaji wa makazi na upimaji shirikishi. Hii yote ni mikakati ya kupambana na ujenzi holela.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali itaendelea kukabiliana na changamoto za ujenzi holela usiozingatia taratibu, kanuni na sheria kwenye miji yetu. Niendelee kutoa wito kwa watumishi wa Wizara yetu kufanya kazi kwa weledi na uadilifu mkubwa kuzuia ujenzi holela kwa kushirikiana na wadau wengine kama Halmashauri za Miji, Wilaya, Manispaa na Majiji kwa kusimamia kikamilifu mipango kabambe iliyopitishwa na mamlaka zao bila kuathiri sheria na kanuni zilizopo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asya.

**MHE. ASYA SHARIF OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina swali moja la nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni sheria zipi zinazosimamia jukumu hili la kudhibiti ujenzi holela?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko sheria mbalimbali ambazo zinatawala usimamiaji wa maboresho ya ujenzi katika maeneo yetu. Iko Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura Na. 228, Toleo la Mwaka 2010, kifungu cha 55(2), kinaeleza jukumu la kupanga na kusimamia uendelezaji wa miji katika mamlaka ya upangaji. Vilevile kifungu cha 55(8) na (16) cha sheria hiyo kimeweka katazo la ujenzi bila kupata kibali. Aidha, Fungu la 29 la Sheria ya Mipango Miji, Sura ya 355 linakataza uendelezaji wa ardhi yoyote ndani ya mipaka ya mamlaka ya upangaji bila kuwa na kibali cha uendelezaji wa ardhi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba niulize swali moja la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri; kwa kuwa, tayari Wizara ilishatoa utaratibu

katika mpango kabambe wa uendelezaji na uboreshaji wa miji, likiwemo Jiji la Mwanza ambalo tayari lina *Master Plan* yake. Ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha mipango hii haitavunjwa au haitatekelezwa kinyume kwa kuondoa maeneo yaliyokwishakusudiwa kwenye *Master Plan* na kuyafanyia matumizi mengine ambayo hayakukusudiwa? Nini kauli ya Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kujibu swali la Mheshimiwa Mabula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa baadhi ya maeneo katika nchi yetu, hasa kwenye majiji makubwa ambayo tayari yana mpango mahususi, mpango kabambe wa kuendeleza miji hii, ikiwemo Jiji la Mwanza kumekuwa na utofauti katika kusimamia kile walichojipangia wao wenyewe kwenye utekelezaji wa mipango kabambe ya miji yao. Nitoe rai kwa mamlaka hizi za miji, majiji, kuzingatia yale ambayo yalishapitishwa na mamlaka zao kama mipango kabambe kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, miji ile inatoka na sura nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hili la Mwanza nitoe msisitizo tu kwamba, wazingatie kile ambacho walikubaliana wao wenyewe katika mpango kabambe na fedha nyingi za Serikali zilitumika pale katika kuusimamia ule mradi kwenda kwenye mipango yake.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Tunakwenda Wizara ya Maji, Mheshimiwa Mpakate.

Na. 95

**Mradi wa Maji Tunduru Kusini**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Je, lini mradi wa maji wa Vijiji vya Mbesa, Lijombo na *airport* utakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maji Mbesa-Ndaje utakaonufaisha vijiji vitatu vya Mbesa, Lijombo na *airport* vyenye jumla ya wakazi 12,500. Utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa asilimia 40 ambapo ulazaji wa bomba kuu kutoka kwenye chanzo hadi kwenye tenki umbali wa Kilometa 13.45 umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zinazoendelea sasa ni pamoja na uchimbaji wa mitaro na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa Kilometa 32.13, ukarabati wa matenki mawili yenye jumla ya ujazo wa lita 150,000, ujenzi wa tenki jipya lenye ujazo wa lita 50,000 na ujenzi wa vituo 25 vya kutolea huduma kwa wananchi. Kazi zote hizo zinatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2024.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpakate.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na nimpongeze Mhandisi wa Wilaya kwa kusimamia vizuri mradi huu kwa sababu ni kiporo cha muda mrefu sana kwenye huu mradi, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Mtina ambao ulikamilika zaidi ya miaka miwili iliyopita una changamoto nyingi, wananchi hawapati maji na hayatoki. Je, kuna mkakati gani wa Serikali kuhakikisha kwamba mradi huu unatatua changamoto zote, ili Wananchi wa Mtina waweze kupata maji safi na salama?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; tuna mradi mwingine wa Masuguru, Mcheteni mpaka Mchoteka wa vijiji saba umeanza tangu mwaka 2022 hadi sasa ni vijiji viwili tu ambavyo

mradi huu umeanza; je, ni lini Serikali itakamilisha mradi huu kwenye upande wa Kata ya Mchoteka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kutambua jitihada za Meneja wetu wa Wilaya pale Tunduru, lakini kuhusiana na suala la Mradi wa Mtina Mheshimiwa Mbunge utakumbuka mimi na wewe tulifika kwenye mradi huu na tuliweza kuona kwa pamoja changamoto zake. Sisi kwa upande wetu tumeshakamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ambalo unaliona linaendelea pamoja na mradi kukamilika kumejitokeza *low voltage* katika mtambo wetu wa chanzo cha maji pale Mtina. Kwa hiyo, tayari meneja huyu uliyempongeza anafanya mawasiliano na *REA* na wameshakubaliana baada ya wiki mbili tatizo la *low voltage* litakuwa limeweza kushughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, lini mradi huu wa Mchoteka utakamilika; tunatarajia kufika mwezi Oktoba mwaka huu, Mheshimiwa Mbunge mradi huu utakuwa umekamilika kwa sababu, utekelezaji wake unaendelea vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Liwale shida ya maji ni kubwa sana. Serikali baada ya kulitambua hilo wakatuchimbia visima vitatu kule Kijiji cha Turuki, lakini ni miaka miwili sasa inakwenda maji yale hayajaletwa Liwale Mjini. Nini Kauli ya Serikali juu ya utekelezaji wa mradi ule?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie Bunge lako Tukufu kumuagiza *RM Lindi* kuhakikisha anafika Liwale na anaweza kufanya uzambazaji wa kutoka visima vile vilivyochimbwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hassan.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Tunduru Mjini pampu zake za kusukuma maji zinashindwa kufanya kazi kutokana na kukatikakatika mara kwa mara kwa umeme na unapowaka umeme unakuwa ni *low voltage* na inasababisha Wananchi wa Tunduru Mjini kukosa maji kwa muda mrefu sana. Je, ni lini Serikali itatupatia umeme mbadala kwa maana ya *solar panel* ili kuweza kuondoa adha ya maji pale Tunduru Mjini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kutoka Tunduru Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa *solar* kwenye chanzo cha maji pale mjini, naomba niseme nimelipokea tuweze kuliingiza katika michakato yetu na kuhakikisha tunapata umeme wa uhakika Tunduru Mjini kwenye chanzo cha maji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Serikali imechimba visima vingi sana karibu nane katika Jimbo la Mbulu Mji, lakini hadi sasa ni miaka miwili hatujapata hela ya usambazaji na ujenzi wa miundombinu ya maji kwa ajili ya matenki na mabomba. Je, ni

kwa nini Serikali imeshindwa kutoa fedha kwa ajili ya visima nane vilivyochimbwa katika Jimbo la Mbulu Mji hadi sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kutoka Mbulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijibu kwa ujumla. Visima vyote ambavyo Wizara tumechimba maeneo mbalimbali pamoja na Mbulu Mjini sasa tupo kwenye mchakato wa kuhakikisha vyote tunakwenda kufanya usambazaji na kuona tunasogeza huduma hii kwa kuweka vichotea maji katika makazi ya wananchi. Hivyo, nikutoe hofu Mheshimiwa Mbunge, Mbulu Mjini moja ya wanufaika ambao mkakati tulionao kama Wizara unakwenda kutekelezeka hivi punde.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kabati, ajiandae Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Ng’ang’ange iliyopo katika Wilaya ya Kilolo haina mradi wowote wa maji wala haina hata kisima; je, ni lini Mheshimiwa Waziri utakuja katika kata hiyo ujionee wananchi wanavyopata shida, lakini pia, utembelee na miradi mingine iliyopo katika Mkoa wa Iringa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ritta Kabati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ritta Kabati kwa kweli, amekuwa akilifuatilia suala hili. Nikupongeze sana Mheshimiwa Kabati, lakini kata hii uliyoitaja, kama tulivyozungumza juzi kwamba, tuko kwenye mkakati wa kuona kwamba na kata hii nayo inakuwa mnufaika wa huduma ya maji

safi na salama, tutakwenda kuwachimbia kisima na kuona mradi ambao utawanufaisha wananchi wa kata hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niko tayari kufanya ziara mara baada ya Bunge hili, kujionea na kuhakikisha kuleta msukumo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sengerema tuna ujenzi wa tenki la lita milioni tano ambao mkataba wake ulisainiwa mwaka jana mwezi wa nne, pamoja na usambazaji wa maji Sengerema Mjini kilometa 72. Mpaka leo hii mkataba huo toka umesainiwa kazi hazijaanza kufanyika, nini tatizo lake? Wananchi wa Sengerema wanataka kusikia kutoka kwako Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tabasam, Mbunge wa Sengerema, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba uliosainiwa tayari tupo kwenye hatua za mwisho na tumeshamwelekeza mkandarasi huyu kuhakikisha anafika *site* na kuanza kazi mara moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Nusrat.

Na. 96

**Miradi iliyotekelezwa na fedha za UVIKO-19**

**MHE. NUSRAT S. HANJE** aliuliza:-

Je, miradi gani imetekelezwa kwa fedha za UVIKO-19?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mbunge, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi iliyotekelezwa kwa fedha za UVIKO-19 za mkopo nafuu kutoka *IMF* kiasi cha shilingi trilioni 1.29 ni Sekta ya Maji ikiwemo ununuzi wa mitambo 25 ya kuchimba visima, seti tano za mitambo ya uchimbaji na ujenzi wa mabwawa na seti nne za vifaa vya uchunguzi wa maji chini ya ardhi na miradi ya maji 172 vijijini na miradi 46 mijini. Sekta ya elimu ikiwemo ujenzi wa madarasa 12,000 shule za sekondari na 3,000 shule za msingi shikizi. Ukamilishaji wa vyuo vinne vya *VETA* ngazi ya mikoa na vyuo 25 ngazi ya wilaya na ununuzi wa vifaa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kwenye vyuo 11 vya elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine ni Sekta ya Utalii ikiwemo ununuzi wa mitambo mitano kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya hifadhi 13 za Taifa na kuimarisha mifumo ya utangazaji wa fursa za utalii ikiwemo *Royal Tour*. Sekta ya Afya ni ujenzi na ukarabati wa vyumba vya wagonjwa mahututi *(ICU)* katika hospitali 70 na miundombinu ya kutolea Huduma za Dharura *(EMD)* katika hospitali 101. Uunuzi wa *X-ray* 169, *CT-Scan 29, MRI 4* na mashine za huduma za uchunguzi wa moyo saba na ujenzi wa nyumba 150 za wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika sekta ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, Serikali imeboresha miundombinu na mazingira ya kufanyia biashara kwa wafanyabiashara wadogo (wamachinga) pale *Bahi Road* Dodoma, Halmashauri za Majiji ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Tanga, Mbeya pamoja na Halmashauri za Manispaa ya Kinondoni, Temeke, Ubungo na Morogoro. Vilevile shilingi bilioni 5.542 zimetumika kusaidia kaya maskini 51,290 zilizotambuliwa katika halmashauri 35 kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania *(TASAF),* ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Ufanisi ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali mwaka 2021 na 2022 inaonesha kwamba, utekelezaji wa miradi inayodhaminiwa na UVIKO, *especially* kwenye sekta ya afya na elimu imekuwa imetekelezwa chini sana ya kiwango na kimsingi tija ni ndogo sana na thamani ya fedha ni tofauti kabisa na kilichoko *site* na Taarifa ya Ufanisi ya Mdibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali inasema hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilitaka kujua Serikali imejifunza nini kutokana na fedha za *design* ya UVIKO-19 zinapokuja kwa sababu, tunajua zilivyokuja. Mmejifunza nini *going forward* kwa sababu, tunahitaji *at least* tuone thamani ya fedha na kilichopo *site* kinafanana hivyo. Ni kweli mmepeleka huko, mlifikiri kwa kufanya hivyo na ni vizuri, lakini mmejifunza nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili; kuna sekta nyingine ya utalii, maji na uwezeshaji wananchi kiuchumi; je, Serikali imefautilia kujua ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya upande huo mpaka sasa hivi? Wamefuatilia kufahamu? Nilitaka nifahamu hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, swali la kwanza usilijibu sababu bado hiyo *opinion* ni ya *CAG*, jibu swali la pili.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Nusrat Hanje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafuatilia kila siku katika miradi yote ambayo inafanyika nchini na ndio maana kila sekta katika Serikali hii ipo idara au kitengo cha ufuatiliaji na tathmini kwa ajili ya suala la ufuatiliaji, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Jenejelly.

Na. 97

**Uhaba wa watumishi *TRAB na TRAT***

**MHE. JANEJELLY J. NTATE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza changamoto ya uhaba wa Watumishi katika vyombo vya *TRAB* na *TRAT*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jenejelly James Ntate, Mbunge, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *TRAB* ina jumla ya watumishi 27 ambao kwa sehemu kubwa wanamudu kutekeleza majukumu ya taasisi ikilinganishwa na ikama ya watumishi 35. Aidha, *TRAT* inapaswa kuwa na jumla ya watumishi 36, ambapo kwa sasa kuna jumla ya watumishi 15. Kwa upande wa *TRAT*, Wizara imefanya *hard hunting* ya kupata watumishi wanne wenye uzoefu na kuwasilisha maombi ya uhamisho Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora mwezi Januari, 2024.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, mimi nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, tunaoneshwa kwamba *TRAB* ina upungufu wa watumishi nane, lakini *TRAT* ina upungufu wa watumishi zaidi ya nusu, na hivi ni vyombo vya kutoa haki.

Je, Serikali haijaona kwamba haki haitendeki sawa sawa kwa wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali namba mbili, umesema mmefanya *head hunting*. Tumekuta kwenye taasisi nyingi *head*

*hunting* inaleta sintofahamu mnapo-*hunt* wale watumishi wenye mishahara mikubwa kuliko walio kwenye taasisi.

Je, Serikali mmejipangaje mnapofanya hii *head hunting* kwa watumishi hawa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge Ntate, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba upungufu huo upo kama alivyosema lakini kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, ni kwamba bado kazi zinaendelea na tumeuona; na Serikali itachukua ushauri wako na kuufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali la pili, ni kweli changamoto kama hii iliwahi kujitokeza na ukatokea mgongano kwenye suala zima la tofauti au mpishano wa maslahi lakini nakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hili limefanyiwa kazi na Serikali na halitojitokeza, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa kazi ilifanywa na Serikali katika haya mabaraza, *Tax Revenue Appeals Tribunal* na *Tax Revenue Appeals Body.*

Je, mpaka sasa hivi tuna malimbikizo ya kodi kiasi gani ambayo yameshikiliwa katika mabaraza hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, swali la takwimu. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Protas.

Na. 98

**Msamaha wa matibabu kwa wagonjwa wa sukari na tezi dume**

**MHE. VENANT D. PROTAS** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kutoa msamaha wa matibabu kwa wagonjwa wa sukari na tezi dume nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mbunge wa Jimbo la Igalula, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inasisitiza utekelezaji wa Sera ya Afya ya mwaka 2007 ya kutoa huduma ya msamaha kwa wananchi wasio na uwezo wa kulipia huduma za afya. Hata hivyo, wenye uwezo wa kulipia wataendelea kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama ya kutibu wagonjwa wa sukari kwa mwaka ni shilingi bilioni 300 na gharama za kutibu wagonjwa wote wa tezi dume ni shilingi bilioni 46.42. Hivyo, kupelekea jumla ya gharama za matibabu kwa magonjwa haya mawili tu kufikia shilingi bilioni 346.42 ilhali bajeti ya dawa na vifaa tiba inayotengwa hapa Bungeni kwa mwaka ni shilingi bilioni 200. Hivyo, ikitokea huduma ya matibabu kwa magonjwa haya mawili ikatolewa bure itapelekea huduma nyingine katika nchi kusimama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2022/2023, gharama ya msamaha wa matibabu kwa wagonjwa wa sukari na saratani ya tezi dume ilikuwa ni kiasi cha shilingi bilioni 70.4

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Protas.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na Serikali kwa ujumla, kumekuwa na changamoto sana kama alivyojibu jibu la msingi hapo, ya watu wanaokwenda kupata msamaha, hasa wa kaya maskini. Wanapokwenda pale hawapewi msamaha bali wanaulizwa mswali na baadaye wanaambiwa wakatafute fedha. Wagonjwa wengi wamekuwa waking'ang'aniwa hospitali.

Je, hamwoni kama kuna haja kwa Wizara kutoa mwongozo mahususi kwa watu masikini kweli, wapewe misamaha kama Serikali ya Mama Samia inavyotaka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa sababu haya magonjwa ya sukari na tezi dume yamekuwa sasa ni magonjwa makubwa sana kwa wananchi wetu, hasa kaya maskini.

Je, hamuoni sasa kama tumeweza kuweka ruzuku kwenye mbolea, tumeweka ruzuku kwenye umeme, hamuwezi kuona sasa kama haya ya kuokoa maisha tukaweka ruzuku ili wananchi wetu waweze kuokoa maisha yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili mazuri ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, amesema ni sisi tusimamie vizuri kwenye eneo la msamaha. Mheshimiwa Mbunge, nakuhakikishia tutaenda kuongeza nguvu sana kwenye kusimamia kuhakikisha wote wasio na uwezo wanatibiwa bure kulingana na mwongozo unavyotaka. Nikuombe Mheshimiwa Mbunge, kupitia Baraza lako la Madiwani na Waheshimiwa Wabunge wote, tuendelee kwa pamoja kusimamia na kufuatalia haya mambo kama yanatekelezwa vizuri kule chini, kama ambavyo miongozo inaelekeza.

Swali lako la pili ni hili la ruzuku; kwanza hapa Bungeni tumepitisha tumekwenda kwenye Bima ya Afya kwa Wote.

Tutaenda kutatua hili tatizo. Ndiyo maana wakati tunapambana kupitisha Bima ya Afya kwa Wote, Waheshimiwa Wabunge walisema hatutapitisha mpaka tuoneshwe fedha za kusaidia wale wasioweza kulipia zinapatikana kwenye vyanzo gani. Ndiyo maana Serikali ilionesha vyanzo vya kupatikana fedha kwa ajili ya kulipia bima kwa wasiojiweza ndipo mkaruhusu na ukapitishwa Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunakwenda kwenye bajeti mwaka huu. Tunaanza kufanya maoteo ya bajeti mwaka huu. Basi tutaendelea kujadiliana na kushirikiana kwa pamoja ili tuone ni kwa namna gani tunaweza kupata fedha kidogo kwenye bajeti ili kuweza kuhudumia maeneo hayo. Tuendelee kushirikiana kwa sababu haya ni masuala ya Kibajeti. Tuna matatizo mengi lakini wagonjwa ni wengi. Ukizungumzia kansa ya tezi dume, kuna kansa inayoongoza ambayo ni Kansa ya Kizazi kwa kinamama *(cervical cancer)*, kuna ya matiti na kuna mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ukifungua hii *pandora box* unafungua jambo kubwa sana. Unatakiwa kutafakari kabla ya kusema lolote. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kumekuwa na tabia ya kunyanyapaa wagonjwa kwenye Hospitali ya Wilaya ya Nyang'hwale hususan wazazi na kusababisha kifo cha mama mzazi ambaye amekwenda kujifungua na alipokelewa tangu siku ya Jumamosi, hakupata huduma mpaka siku ya tatu anakwenda kupoteza maisha.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari baada ya Bunge hili tuambatane mimi na yeye ili akawasikilize hawa wananchi kadhia wanayofanyiwa pale kwenye ile hospitali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namwambia niko tayari. Hata ikiwezekana wikendi hii mimi na wewe twende. Nitumie hii fursa kusema kwamba, tukienda

kwenye wilaya yoyote kuna Kamati ya Ulinzi na Usalama na kuna Serikali kamili. Inapotokea Watanzania wananyanyaswa kwenye wilaya mpaka tunakuja huku taifani kushughulikia, tunatakiwa kwanza kabla ya kufikiria kuja huku taifani tuwaze Kamati ya Ulinzi na Usalama na uongozi kamili ulioko kwenye wilaya hiyo, uongozi kamili ulioko kwenye mkoa huo umefanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi hapa kwangu kuna watu juzi walitaka kuiba ushirika. Nilishughulika nao, hakuna mtu aliyeona kwenye *TV* na tukawanyang'anya shilingi milioni 316 na sasa Idara ile ya Ushirika iko vizuri. Ninamwomba kila Mbunge, usisite ukiona mtu ananyanyasa wananchi wako anza kutandika, tukukute huku ukiendelea na zoezi tukusaidie kuwanyoosha wahuni. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Fakharia.

Na. 99

**Msaada kwa wazee**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa msaada kwa Wazee ili waweze kumalizia maisha yao kwa amani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimwa Naibu Spika, Serikali inatambua mchango wa wazee katika ujenzi wa Taifa. Hivyo, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI imefanya utambuzi endelevu wa wazee na kutoa huduma za ulinzi na usalama kwa wazee wasiojiweza

kupitia makazi ya wazee ya Serikali na ninafsi. Huduma hizo ni pamoja na chakula, malazi na makazi. Aidha, Serikali inatoa huduma za afya bila malipo kwa wazee wasiojiweza, ikiwa ni pamoja na kuanzisha madirisha 558 ya huduma za afya kwa wazee na kutoa kipaumbele cha tiba katika zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, mikoa, kanda na Taifa.

Mheshimwa Naibu Spika, hivi sasa Serikali ipo katika mapitio ya Sera ya Wazee ya Mwaka 2003 na kuiboresha ili iweze kuendana na mahitaji ya sasa, ikilenga kuimarisha upatikanaji wa huduma na kuhamasisha uwepo wa pensheni ya jamii kwa wazee, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fakharia.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Maswali yangu ameyajibu vizuri na yanaeleweka na hata baadhi ya wazee watapata faraja kwa jinsi walivyopokea jawabu hilo; lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ipo katika mapitio ya Sera ya Wazee ambayo ilifanywa katika mwaka 2003; je, kwa wale wazee ambao siyo waajiriwa wa Serikali na ambao bado wanahitaji matibabu, Wizara itaweza vipi kuwasaidia ili na wao waweze kupata bima ya afya ya bure? Kwa sababu, waajiriwa wa Serikali wakistaafu wanapata bima ya afya ya bure lakini wale waliokuwa siyo waajiriwa na wao ni wazee, wanastahiki vipi kupata bima ya afya ya bure?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa baadhi ya wazee hukosa wategemezi na wasaidizi wa kuwasaidia, je, Wizara yako inachukua jukumu gani kuwasaidia wale wazee walioko nyumbani ambao hawana wategemezi walau kuweza kupata mlo wao wa siku moja? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Fakharia, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, Serikali inatambua kwamba kuna wazee ambao hawana bima ya afya. Pia, kupitia sera ya mwaka 2003 imetoa mwongozo na kufanya utambuzi endelevu kuhakikisha kwamba, wale ambao hawana bima ya afya waweze kupata bima ya afya bure. Vilevile, Serikali inaendelea kutoa mwongozo wa wazee hao kupatiwa bima ya afya. Pia, Wizara ya Afya inaendelea na mchakato wa kuendeleza bima ya afya kwa wote ikiwemo makundi maalumu na wazee wasiojiweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua uwepo wa wazee ambao hawana familia. Ndiyo maana imeweka vituo 13 vya makazi ya wazee. Hata hivyo, kuna vituo binafsi ya makazi ya wazee 13. Mheshimiwa Rais katika bajeti yake ya mwaka 2023/2024 ametenga fedha shilingi 1,570,255,000/= kwa ajili ya huduma ya wazee hao, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa tunakwenda Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa George Mwenisongole.

Na. 100

**Kumaliza uchunguzi wa Vyama vya *AMCOS* – Mbozi**

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itamaliza uchunguzi kwa Vyama vya *AMCOS* – Mbozi ambavyo havikupatiwa uchunguzi wa awali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa George Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania imefanya uchunguzi wa vyama 20 vya Msingi vya Kahawa Wilayani Mbozi. Uchunguzi huo ulibaini ubadhirifu katika *AMCOS* nane kati ya *AMCOS* 20. Hatua zilizochukuliwa kwa waliobainika kuhusika ni pamoja na kurejesha fedha za wakulima na kuwafikisha katika vyombo vya dola.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya madai ya wakulima wa kahawa yalikuwa shilingi 294,839,037. Serikali imefanikiwa kurejesha jumla ya shilingi 170,210,211 na jitihada zinaendelea ili kurejesha kiasi kilichobaki cha shilingi milioni 124.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika *(COASCO)* linaendelea kukagua *AMCOS* 98 zilizobaki Wilayani Mbozi. Hadi kufika mwezi Machi 2024 ukaguzi tunaamini ukaguzi huu utakuwa umekamilika. Hatua hii ni sehemu ya jitihada za Serikali kuhakikisha uwazi na uwajibikaji katika ushirika na kuwachukulia hatua viongozi watakaobainika kuhusika na ubadhirifu wa mali na fedha za Vyama vya Ushirika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa George.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kipekee, kwanza napenda kumshukuru Kamanda wa TAKUKURU Mkoa wa Songwe, Ndugu yangu Mwakambonje kwa kazi kubwa aliyoifanya. Kwa kweli huyu anastahili kuwa mfanyakazi bora wa mwaka wa TAKUKURU.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni hili; hawa watuhumiwa wengi wanaokamatwa wanafikishwa Mahakamani kwa Sheria ya Madai wakati hii ni uhujumu uchumi.

Je, kwa nini Serikali isiwakamate na kuhakikisha kwamba, viongozi wote wa hivi Vyama vya Msingi ambao wamewaibia wakulima, wafikishwe Mahakamani kwa kosa la uhujumu Uchumi na siyo kosa la madai?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza nampongeza Mheshimiwa George kwa kufuatilia masuala yanayohusu ushirika na ubadhirifu na wizi unaotokea katika maeneo yao. Kwa nini wanashtakiwa kwenye suala la madai; ni kwamba mamlaka na uwezo wa Wizara ya Kilimo ni kufanya uchunguzi. Tukimaliza tunakabidhi vyombo vya Dola ambavyo vyenyewe vinaangalia *merit* ya kesi na kuipeleka Mahakamani kwa mujibu wa sheria. Mara nyingi hatua hii ambapo watu wanapofanya ubadhirifu kwenye vyama vya ushirika, ni kweli mara nyingi kesi zao zinaishia kuwa za madai na wanaenda kulipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchakato wa mabadiliko ya Sheria ya Ushirika ambayo tutaileta katika Bunge lako, kutakuwa na *clause* ambayo itakuwa inaelezea wazi namna gani ubadhirifu unaofanyika katika vyama vya ushirika uweze kupata adhabu kali na kuweza kuwafanya watuhumiwa kuadhibiwa kwa adhabu kali; kusiwape nafasi ambazo wanazitumia sasa hivi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa taarifa ya *COASCO* ya ukaguzi wa *AMCOS* zilizo nyingi hapa nchini ubadhirifu unazidi kuongezeka, je, ni nini sababu na chimbuko la ubadhirifu huu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mpina. Sababu kubwa, kwanza vyama vingi vya ushirika vimeanza ku-*improve* kupata hati safi na ubadhirifu kuanza kupungua; lakini ni ukweli

kwamba ubadhirifu bado upo. Sababu kubwa ni mbili; moja, ni tabia ya ukosefu wa uadilifu wa watu ambao wanapata nafasi katika uongozi. Sababu nyingine ni mfumo wa kuwapata viongozi wa Vyama vya Ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya sheria hii ambayo tunaleta, yataweka mfumo ambao utawafanya viongozi ambao wana *record* na matatizo kuweza kuchujwa. Tabia hii ya ubadhirifu ambayo iko kwenye Vyama vya Ushirika, saa nyingine tunaiona hata ndani ya Serikali na maeneo mengine, hata katika jamii zetu. Kwa hiyo, ni hulka na tabia za watu ambazo nadhani elimu inavyoendelea kutolewa na maombi kwa Mwenyezi Mungu, tunaweza kuibadilisha jamii yetu na kupata viongozi wenye hofu ya Mungu ambao wanapewa mamlaka. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Daniel Awack.

Na. 101

**Uboreshaji wa miundombinu ya Skimu ya Umwagiliaji Bonde la Eyasi**

**MHE. DANIEL A. TLEMAI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaboresha miundombinu ya Skimu ya umwagiliaji katika Bonde la Eyasi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Bonde la Eyasi lililopo Tarafa ya Eyasi Wilaya ya Karatu Mkoani Arusha, lina jumla ya skimu za umwagiliaji nane zenye ukubwa wa hekta 5,298.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali kupitia Tume ya Taifa ya umwagiliaji ilitenga fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na ujenzi wa skimu hizo. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika skimu hizo umekamilika na kazi ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu hizo imeanza kupitia mkandarasi *CRJE (EA) Limited*, kwa mkataba wenye thamani ya shilingi bilioni 38.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba huu unahusisha kazi za ujenzi na usakafiaji wa mifereji ya upili yenye urefu wa jumla ya mita 10,675, mifereji ya kati yenye urefu wa mita 3,020, kuongeza urefu wa mfereji wa Mbuga nyekundu mita 500, ujenzi wa vigawia maji na vivuko, pamoja na ujenzi wa tuta la kuzuia mafuriko lenye urefu wa mita 22,000. Ujenzi huu ukikamilika utanufaisha zaidi ya wakulima 5,350.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutatua changamoto ya uhaba wa maji na kudhibiti mafuriko ya mto Barai, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa ujenzi wa bwawa la umwagiliaji katika Bonde la Eyasi, mchakato wa ununuzi ya kumpata mkandarasi kwa ajili ya Bwawa la Eyasi umekamilika kwa mkataba wenye thamani ya shilingi bilioni 21.8 kupitia Mkandarasi Tunnel Sadd Ariana. Ujenzi wa bwawa hili unaanza Februari, mwaka 2024.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Daniel.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa, kujengwa kwa *scheme* makubaliano kwenye mkataba ni kujenga kwa zege, kwa sasa Mkandarasi anajenga kwa mawe na inaelekea mafuriko yakitokea katika Bonde la Eyasi, *scheme* zile zitakuwa fedha za Serikali zitakuwa zimetoka bure. Je, nini kauli ya Serikali yule mkandarasi kujenga kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba kujenga kwa kiwango cha zege?

Swali la pili, kwa kuwa kazi ipo asilimia 19, je, lini waziri ataweza kutembelea bonde lile ili kunusuru shughuli

zinazoendelea kwenye lile bonde ili isije ikawa Serikali imetoa shilingi bilioni 38 wananchi wale wasipate manufaa ya ule msaada wa shilingi bilioni 38 katika Bonde la Eyasi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Daniel, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu lini nitatembelea tukubaliane tu mimi na yeye kwamba baada ya Bunge tutapanga ratiba ya kwenda kutembelea katika mradi huo mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mabadiliko ya ujenzi ni suala la kitaalam, naomba nichukue *concern* yake nitawaita wataalam kujua kwa nini kuna *change* ya *construction* kutoka kwenye kumwaga zege kwenda kwenye mawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukamilishaji wa mradi, mradi huu unajengwa kwa miezi 24. Kwa hiyo, nataka nimuombe Mheshimiwa Mbunge, asiwe na hofu kuna *schedule of activities* ambazo mkandarasi amepewa na analipwa kutokana na kazi aliyoifanya na tutaendelea kuufuatilia kwa karibu kwa sababu ni mradi mkubwa ambao Serikali inawekeza fedha nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafuriko nataka nimtoe hofu. Sababu ya Serikali kuamua kufanya *design* kwa ajili ya kujenga bwawa ni kulinda *scheme* ile ili isiweze kukumbwa na mafuriko ambayo kila wakati yamekuwa yakiathiri eneo lile. Ndiyo maana Serikali inatumia zaidi ya shilingi bilioni 20 kujenga bwawa kubwa katika eneo lile ili kulinda *scheme* hiyo na uwekezaji unaofanyika katika eneo hilo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi ajiandae Mheshimiwa Mwambe, na Mheshimiwa Katani ajiandae.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bonde la Umba kuna *scheme* za Kitivo, Runguza pamoja na Mnazi

ambazo zimeshafanyiwa usanifu lakini ni muda sasa hakuna shughuli zozote zinazoendelea.

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi katika *scheme* hizi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shangazi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, *scheme* tatu zilizopo katika jimbo lake, *scheme* ya Kitivo, Rungu na Mnazi ni *scheme* ambazo tumemaliza suala la usanifu na upembuzi yakinifu katika mwaka huu wa fedha. Nataka nimuahidi kwamba kabla ya mwaka wa fedha kuisha zitatangazwa *scheme* hizo tatu ili ziweze kupata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetenga pesa kwa ajili ya maboresho ya *scheme* za Ndanda, Maparagwe pamoja na Mkungu zilizopo Jimboni Ndanda lakini *scheme* hizi zilifeli kwa sababu wamiliki wa asili wa maeneo haya ukiwemo ukoo wa Mchekenje wa pale Ndanda, hawakulipwa fidia na Serikali wakati Serikali inachukuwa maeneo haya ili kuyafanya yawe ya *scheme*, sasa tunakwenda kujenga tena upya. Je, waziri anasema nini kuhusiana na suala la fidia kwa wamiliki wa asili wa maeneo haya ambako *scheme* hizo zilikuwepo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimuombe Mheshimiwa Mwambe na niwaombe wananchi wa Jimbo la Ndanda, fedha za umma zinazoenda kujengwa, Serikali haiendi kulima katika *scheme* ile, anayejengewa ni yule mwananchi mwenye eneo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nataka nimuombe Mheshimiwa Mbunge kwamba na niwaombe wananchi wa Ndanda nalifahamu hili tatizo na lilikwamisha mradi mara ya kwanza na kupoteza fedha za umma. Tumewaomba wananchi tunaowajengea *scheme* katika maeneo yao, kwa kuwa uwekezaji unawekezwa kwa faida yao na mashamaba ni mali yao hayachukuliwi na Serikali, siyo sahihi tulipe fidia halafu bado kesho na kesho kutwa tena uende ukagaiwe lile eneo wewe huyo huyo uliyelipwa fidia kwenda kulima pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa kuwa Serikali haina mpango wa kulichukuwa lile shamba kuwa mali yake ni mali yao wao, siyo haki kumlipa fidia kwenye eneo ambalo tunamjengea yeye *scheme*. Kwa hiyo, mimi niweke *clear position* ya Serikali, mahali popote tunapoenda kujenga *scheme* ya umwagiliaji kama hakuna nyumba, hakuna mazao ya kudumu, hakuna makaburi, ardhi ni mali yako Serikali itakujengea *scheme* hatutakulipa fidia kwa sababu lile ni eneo lako na utalima wewe mwenyewe. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwambe ukiuza korosho zinakuwa zako mwenyewe. Mheshimiwa Katani. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kupatikana *scheme* nyingi katika Jimbo la Tandahimba na mazao haya yanauzwa kwa njia ya ulazaji ikiwemo na korosho, kumekuwa na malalamiko, bahati nzuri leo Wananchi wa Tandahimba wapo Bungeni hapa.

Je, nini kauli ya Serikali juu ya malalamiko hayo juu ya ulazaji wa boksi lile kwenye uuzaji wa korosho? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Katani, kuhusu kulaza boksi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme tu kupitia Bunge lako Tukufu, tunaenda kuanza msimu wa ufuta, tunaenda kuanza

msimu wa mbaazi. Minada yote itakuwa ya wazi na itafanyika kwa *TMX*, hakutakuwepo na kulaza boksi tena. Mwaka juzi tulitaka kuweka mfumo wa wazi, mnada wa kwanza vyama vya ushirika vikasema hatuuzi, mnada wa pili wa mfumo wa wazi wakasema hatuuzi, mnada wa tatu wakasema hatuuzi. Tukaruhusu kulaza, tulivyofanya tathmini bei walizozikataa kwenye mnada wa wazi na bei za kulaza hakuna tofauti yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niseme leo wazi msimamo wa Wizara ya Kilimo, mfumo wa stakabadhi ya ghala kwa ajili ya ufuta na mbaazi tutakaoanza msimu unaokuja kuanzia Pwani, Lindi, Mtwara, Ruvuma tutaufanya kwa wazi na kwa kutumia mfumo wa *TMX* na wanunuzi watashindana *online* na siku ya mwisho wakulima wataamua hakutakuwa na kulaza mfumo tena. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Katimba.

Na. 102

**Upanuzi wa Uwanja wa Ndege Mkoa wa Kigoma**

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA** aliuliza: -

Je, lini upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Mkoa wa Kigoma utakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa upanuzi na ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Kigoma, unatekelezwa na Mkandarasi *China Railway Engineering Construction Group* kwa gharama ya shilingi bilioni 46.68 kwa muda wa miezi 18, ambapo mkandarasi

alianza kazi tarehe 05 Septemba mwaka 2023, anatarajia kukamilisha utekelezaji wa mradi huu tarehe 05 mwezi wa tatu, mwaka 2025 kwa mujibu wa mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ujenzi kupitia *TANROADS* inaendelea kusimamia utekelezaji wa mradi huu ili mkandarasi aweze kukamilisha kwa wakati. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zainab.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, aidha nina maswali mawili ya nyongeza.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara zinazounganisha Kiwanja cha Ndege cha Kigoma pamoja na Manispaa ya Kigoma Ujiji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kufahamu ni lini Serikali inaanza kujenga au kurefusha barabara ya kukimbilia ndege Kigoma, yaani *runway extension* nataka kufahamu ni lini kazi hiyo inaanza? (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza Mheshimiwa Zainab, ameuliza barabara ambazo zinaingia *Airport* kwa maana ya *access roads*. Barabara ambazo amezitaja Mheshimiwa Zainab, zipo chini ya *TARURA* lakini nikubaliane naye kwamba Serikali ya Awamu ya Sita katika kujenga *airport* ya kisasa ya Mkoa wa Kigoma, haiwezekani tukawa na *airport* ya kisasa halafu tuna barabara za vumbi. Kwa hiyo, kupitia kwa Kaka yangu Mheshimiwa Waziri Mchengerwa, nimuombe tuangalie namna ambavyo *TARURA* itawezeshwa ili barabara hizi ziweze kujengwa wakati tunakamilisha *airport* basi barabara hizi pia ziwe zimejengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili Mheshimiwa Zainab Katimba anauliza *runway* ya *airport* ya Kigoma ni fupi na kwamba itakuwa *extended* lini. *TANROADS* jukumu lake ni kufanya ujenzi lakini najua wizara pacha Wizara ya Uchukuzi wapo katika mazungumzo na *EIB* ili baada ya kukamilisha ujenzi wa jengo la abiria pamoja na *control tower* basi suala hili la *extension* ya *runway* liweze kufuata. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Njombe kutokana na mchango mkubwa wa zao la parachichi, Serikali imeahidi kujenga uwanja wa kisasa wa ndege. Ni lini uwanja huo utaanza kujengwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Mwanyika kwa ufuatiliaji lakini suala hili kama nilivyosema vipo viwanja ambavyo *TANROADS* tunaendelea na ujenzi kwenye miradi mipya ya ujenzi wa *airport* na kama mnavyofahamu ilikuwa ni Wizara moja ya Ujenzi na Uchukuzi, sasa hivi Wizara ni mbili lakini tunafanya kazi kwa kushirikiana. Kwa hiyo, swali la Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, nimelichukuwa nitalifikisha kwa Wizara pacha kwa Mheshimiwa Profesa Mbarawa ili na hili liingie kwenye vipaumbele. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Londo.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna uwekezaji mkubwa na upanuzi mkubwa wa uwanja wa ndege pale Mikumi. Hivi ninavyozungumza kila siku kuna ndege zaidi ya nane mpaka 10 zinatua. Upanuzi huu unaenda kuongeza idadi ya ndege lakini pia ukubwa wa ndege. Barabara ya kutoka Mikumi mpaka Kilosa sasa hivi hali yake ni mbaya mbaya mbaya sana na Waziri anajua hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nini kauli ya Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Londo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema jana wakati nachangia hoja ya Kamati ya Miundombinu, mkakati wa Serikali kwa mvua za *El Nino* zinazoendelea pale mawasiliano ya barabara na madaraja yanapokatika jitihada za Serikali ni kurudisha mawasiliano mara moja huku tukiendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuhakikisha barabara hizi zinatengenezwa na kukarabatiwa kwa namna ambayo ni ya kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimuagize meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Morogoro kufuatilia barabara hii ya Mikumi - Kilosa ili tuangalie jambo ambalo linaweza likafanyika ili mawasiliano ya barabara hii yaweze kuendelea. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu safi. Mheshimiwa Neema Lugangira, jiandae Mheshimiwa Midimu.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Ninataka kufahamu mwezi Novemba, 2022 Serikali ilitoa kauli kwamba inaweka mikakati ya kujenga *airport* ya Omukajunguti Mkoani Kagera.

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa *airport* ya Omukajunguti ili kufungua Mkoa wa Kagera kiuchumi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwanza nimpongeze Mheshimiwa Lugangira kwa ufuatiliaji lakini jambo hili limekuwa

likifuatiliwa sana na Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Kagera, wakiongozwa na Mheshimiwa Mwijage, Mwenyekiti wetu na mimi ni-*declare interest* kama mwana Kagera jambo hili ni muhimu sana kwa Mkoa wa Kagera. Kwa hiyo, kama nilivyosema Wizara ya Uchukuzi ninaamini jambo hili wameliweka kwenye kipaumbele ili uwanja huu wa Omukajunguti uweze kujengwa na Mkoa wa Kagera uweze kufunguliwa kiuchumi na kutoka kwenye baadhi ya miongoni mwa Mikoa ambayo kwenye rekodi ipo kwenye Mikoa ambayo ipo chini kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimpongeze Mheshimiwa Mbunge na waheshimiwa wabunge wa mkoa wa Kagera na mimi mwenyewe nikiwemo, Wizara ya Uchukuzi tutaendelea kuwakumbusha jambo hili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Midimu, jiandae Mheshimiwa Kilumbe, jiandae Mheshimiwa Kassim.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, ujenzi wa uwanja wa ndege Mkoa wa Simiyu upo kwenye Ilani na eneo tayari limeshatengwa na nizuri lipo karibia na Serengeti, watalii watakuwa wanashuka pale. Je, ni lini ujenzi huo utaanza? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther, kama…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, huna haja ya kusema namuomba wewe sema jibu moja kwa moja.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia hoja ya Mheshimiwa Mbunge na Wizara ya Uchukuzi naamini Mheshimiwa Profesa Mbarawa, kama nilivyosema viwanja vipya vipo chini ya Wizara ya Uchukuzi, Serikali imelisikia na litawekwa kwenye vipaumbele. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Serikali itajega, Mheshimiwa Kilumbe. Jiandae Mheshimiwa Kassim.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nilitaka kurudi pale Uwanja wa Ndege wa Kigoma, upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Kigoma Serikali imechukua maeneo ya wananchi wa Kigoma kwa ajili ya upanuzi huo wa awamu ya pili. Tangu imechukuwa na kufanya uthamini mpaka sasa wananchi wale hawajalipwa na hawawezi kuendeleza makazi yao, vyoo vinavunjika kutokana na mvua. Nini kauli ya Serikali, ni lini watalipwa fedha ili waweze kwenda kwenye makazi yao ya kudumu kuachana na eneo hilo ambalo limechukuliwa na Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hilo lipo kwako, lipo uchukuzi?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni sehemu ya ujenzi wa jengo la abiria pamoja na *control tower*, tathimini ya fidia imeshafanyika na tumepeleka maombi Hazina. Niwaombe wananchi waendelee kuwa na subira wakati jambo hili linafanyiwa kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kassim.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Jimbo la Msalala wanatamani kutumia Kiwanja cha Ndege cha Kahama. Kutokana na barabara inayotoka Kakola kwenda Kahama ni mbovu sana na kwa kuwa Serikali imeshatenga fedha, kibali kimeshatoka hatua zote zimekamilika. Nataka kufahamu Mheshimiwa Waziri, naomba unisaidie sana kwenye hili jambo, ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi wa barabara hiyo wakati kila kitu kimekamilika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Iddi Kassim, amekuwa akifuatilia barabara hii ya Kahama - Kakola kwa umakini mkubwa. Kwa hiyo nimpongeze na nimhakikishie yeye pamoja na wananchi wake kwamba tupo hatua za mwisho, sasa hivi Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali yupo kwenye

hatua ya ku-*vet* mkataba na baada ya hatua hizi kukamilika tutasaini ili ujenzi uweze kuanza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwanza ninakushukuru sana kwa majibu sahihi kwa kuweza kuhimili maswali yote haya. Ahsante sana. (Makofi)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mwakibete.

Na. 103

**Ujenzi wa barabara kwa kutumia teknolojia ya kisasa**

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kutumia teknolojia mpya ya kisasa na ya gharama nafuu katika ujenzi wa barabara nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa matumizi ya teknolojia mbadala katika ujenzi wa barabara ambapo kupitia *TANROADS* imefanya majaribio ya awali kwa baadhi ya teknolojia mpya na inaendelea kutathmini ufanisi wake kwenye mazingira yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtaalam wa ujenzi kwa kutumia teknolojia hizo amepatikana na majaribio yatafanyika katika barabara ya Chamwino Ikulu – Babalo – Itiso yenye urefu wa kilometa 1.1 Mkoani Dodoma kwa kutumia teknolojia ya *Geopolymer Stabilizer* na barabara ya Mtwara – Mnivata kilometa

12 Mkoani Mtwara, kwa kutumia teknolojia ya *Amarseal Surface Rejuvenator,* ninashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakibete.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninampongeza Mheshimiwa Waziri, lakini pia ninampongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa kutoa fedha nyingi katika kuboresha miundombinu ya barabara hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza; duniani tuna teknolojia zaidi ya 100 katika kuboresha na kujenga barabara kwa gharama nafuu zaidi ukilinganisha na teknolojia tunazotumia sasa hivi hapa nchini. Hapa nchini tuna teknolojia nne tu; tuna *double surface dressing (DSD)* ambayo kwa kilometa moja inagharimu kati ya shilingi 1,200,000,000 mpaka shilingi 1,300,000,000; pia tuna *Asphalt Concrete* ambayo inagharimu kati ya shilingi 1,500,000,000 mpaka shilingi 1,700,000,000; na tuna teknolojia ya *Asphalt Concrete Modified* ambayo inagharimu kati bilioni 1.7 mpaka bilioni 2.5 na ya nne ni *intercept…*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa twende kwenye swali.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali, kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kuondokana na gharama zote hizi ili kuleta teknolojia nzuri na bora ukizingatia kwamba kipindi hiki cha mafuriko nchini barabara nyingi zimeharibika? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa majaribio yameshafanyika zaidi ya teknolojia nane na zote zimekuwa kwenye majaribio kwa muda mrefu na majawabu yake huwa hayatoki; je, Mheshimiwa Waziri analithibitishiaje Bunge hili kwamba teknolojia hii ambayo sasa hivi mmeanza kujaribu italeta matunda na tija kwa wananchi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Atupele Mwakibete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, ametaja teknolojia zipo nyingi, ametaja takribani 100, lakini hapa nchini tumetumia baadhi ya teknolojia, nimhakikishie Mheshimiwa Mwakibete, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi tunaangalia teknolojia hizi na namna ambavyo zina-*apply* katika mazingira yetu na baadhi ya hizi teknolojia tumeanza kuzitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, *so far,* miradi mingi ambayo inaendelea kutumia teknolojia hizi ni barabara za *TARURA,* wataalam wametuambia kwamba teknolojia hizi zimeonesha kuwa na manufaa kwenye barabara ambazo yanapita magari ambayo hayana uzito mkubwa. Kwa hiyo, tutaendelea kuangalia namna barabara ambazo zimetengenezwa kwa teknolojia hizi zinavyo-*behave,* halafu baada ya hapo tuweze kujenga kwa kilometa nyingi kwa kadri tathmini zitakavyokuwa zinatuonesha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kufanya ziara Jimboni kwangu na mkutano mkubwa pale Mlangali.

Sasa swali langu, ile Barabara ya Mkiu – Liganga – Madaba, eneo lile la Mkiu kuna kona moja magari leo yapo pale siku ya tatu; ili kuokoa fedha inayotumika kwa matengenezo ya dharura, je, Serikali haioni haja ya kujenga eneo lile kwa kiwango cha lami? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali na Mheshimiwa Kamonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mvua za *El-Nino* zinaendelea kunyesha, ninachoweza kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wananchi wa Jimbo la Ludewa ni kwamba ninamuagiza Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Njombe afike eneo hili mara moja ili tuone namna ya kurudisha mawasiliano wakati tunaendelea kujipanga kuangalia suluhisho la kudumu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Waziri amejibu maswali mengi. Mheshimiwa Waziri, ahsante sana na hongera sana.

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Samweli. *(Makofi)*

Na. 104

**Changamoto za mawasiliano Kata za Hanang**

**MHE. ENG. SAMWELI X. HHAYUMA** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani kumaliza changamoto za mawasiliano ya simu Kata za Gesambalang, Gehandu, Simbay, Sirop na Gidahababiyeg - Hanang?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Samweli Hhayuma, Mbunge wa Jimbo la Hanang, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha inafikisha huduma ya mawasiliano ya simu katika vijiji vyote nchini kama Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020-2025 inavyoelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* imeanza utekelezaji wa ujenzi wa mnara katika Kijiji cha Matangarimo kilichopo katika kata ya Sirop kupitia mradi wa Tanzania ya Kidigitali ambapo kijiji husika kitafikishiwa huduma za mawasiliano na kampuni ya simu ya Honora (Tigo).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kata za Gesambalang, Gehandu, Simbay pamoja na Gidahababiyeg zitafanyiwa tathmini kuangalia mahitaji halisi ya kufikisha huduma za mawasiliano kisha vijiji vya kata husika vitaingizwa katika orodha ya miradi itakayotekelezwa na *UCSAF* kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Samweli.

**MHE. ENG. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali madogo mawili.

Swali la kwanza, kwa kuwa ukiacha maeneo ambayo yametajwa kwenye majibu ya Serikali, baadhi ya maeneo ya Kata ya Gitting, Kata ya Bassodesh na Kata Hirbadaw na maeneo mengi yana changamoto ya mtandao; je, Serikali ipo tayari kufanya tathmini ya uimara wa mtandao *(signal strength)* katika Wilaya ya Hanang ili hatimaye kutibu tatizo hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, tulishiriki kwenye utiaji saini wa miradi ambayo itaenda kutekelezwa na Mradi wa *UCSAF;* je, ni lini miradi hiyo itatekelezwa ili kutatua tatizo la changamoto ya mtandao kwenye maeneo yetu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Samweli Hhayuma, Mbunge wa Hanang, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimejibu katika swali la msingi ni kwamba maeneo ambayo yana changamoto tutayafanyia tathmini na baadaye tutayaingiza katika bajeti ijayo ili yakafanyiwe tathmini na kuhakikisha kwamba minara inajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali pili, ni kweli kabisa Mheshimiwa Mbunge ameendelea kuwa msemaji na mfuatiliaji wa miradi yote inayotakiwa kufanyika ndani ya Jimbo lake ikiwemo hii ya ujenzi wa minara 758, na Mheshimiwa Mbunge tulifanikiwa kuingiza kata nyingine ya Dirma ambayo ina wakazi takribani 8,500 na kuna vijiji takribani vitatu ambavyo Bassaldesh, Galosendo pamoja na Dirma yenyewe wanaenda kupata huduma ya mawasiliano kupitia mtandao wa Tigo na ujenzi tayari wameshafanya *survey* na mkandarasi kati ya mwezi huu anaingia katika eneo la kutekeleza mradi huo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere, ajiandae Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, ninataka kuuliza swali; nini kauli ya Serikali katika makampuni ya simu yaliyojenga minara katika maeneo ya vijijini na hayalipi kodi za vijiji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza na Mheshimiwa Getere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kodi za aina mbili; kuna kodi ya pango ambapo hii kodi inalipwa kulingana na mmiliki wa ardhi, kama ardhi inamilikiwa na mtu binafsi basi kampuni ya simu italipa kwa mtu binafsi na kama eneo hilo linamilikiwa na Serikali ya Kijiji basi mtoa huduma atalipa kwenye Serikali ya Kijiji, lakini jambo lingine ni kwamba kuna *service levy* ambayo huwa ni asilimia tatu ya faida ya makampuni katika Halmashauri husika na hizi fedha huwa zinapelekwa katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Ofisi ya Rais, TAMISEMI inazishusha kwa Wakurugenzi wa Halmashauri

husika na wao wanaziingiza kwenye mapato kulingana na Baraza la Madiwani watakavyoamua namna gani mgawanyo utafanyika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa ameshakuelewa. Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto ya mawasilaini kwa baadhi ya maeneo ya Jimbo la Lushoto kukosa mawasiliano, lakini Kata ya Ubiri imejengewa mnara mpaka sasa hivi mnara ule una zaidi ya mwaka mmoja haufanyi kazi; je, ni tatizo gani lililosababisha mnara ule usifanye kazi mpaka leo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni eneo ambalo ni *specific* kuhusu mnara *specific*, kama Serikali tunalipokea na tutatuma wataalam wetu wakatazame changamoto ya mnara huo na baadaye tutachukua hatua sitahiki. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa alifika Jimbo la Mbulu Vijijini na aliona kata ambazo hazikuwa hazina mawasiliano na ukatoa ahadi kwamba minara itajengwa; je, lini minara hiyo inajengwa ili mawasiliano yapatikane Mbulu Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Flatei, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa nimefika katika Jimbo hili na nikajionea changamoto ya mawasiliano na kata husika ambazo zipo kwenye changamoto hiyo tuliziingiza katika utekelezaji wa minara katika maeneo hayo na katika maeneo hayo tayari watoa huduma wameshapatikana na tupo kwenye mkataba wa miezi 24. Kwa hiyo, tunaamini kwamba ndani ya kipindi hicho utekelezaji wa miradi hiyo utakuwa umekamilika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante, ninakushukuru. Wizara ya Maliasili, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu.

Na. 105

**Tembo kuharibu mazao na kuwadhuru wananchi**

**MHE. SUBIRA K. MGALU** aliuliza:-

Je, upi mpango wa kuzuia tembo kuharibu mazao na kuwadhuru wananchi wa Kiwangwa, Bwilingu na Mkangena wanaozunguka Hifadhi ya Wami Mbiki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuimarisha ulinzi wa mali na maisha ya watu dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo ya Kiwangwa, Bwilingu Mkange na maeneo yanayozunguka Hifadhi ya Pori la Akiba la Wami Mbiki. Hatua hizo ni pamoja na kuweka vituo vya muda vinne vya askari kwenye maeneo ya Kiwangwa, Mkange, Bwilingu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile vituo hivyo zimepatiwa vitendea kazi kama gari na pikipiki kwa ajili ya doria za kuthibiti wanyamapori wakali na waharibifu. Vilevile kuimarisha doria za

udhibiti wa wanyamapori kwenye maeneo yenye changamoto, lakini vilevile kutoa elimu kwa jamii kuhusu namna bora ya kuepuka madhara yanayoweza kusababishwa na wanyamapori wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatoa rai kwa wananchi kuzingatia maelekezo yanayotolewa na wataalam na kutoa taarifa mapema pindi Wanyamapori wanapovamia maeneo yao. Jitihada hizi kwa pamoja zitaendelea kupunguza changamoto ya Wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo haya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mgalu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri yenye matumaini ya vituo hivi vinne vya muda vilivyofunguliwa Kata ya Mkange, Bwilingu, Ubena na Kiwangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili madogo ya nyongeza; pamoja na kufunguliwa kwa vituo hivi na kuwepo kwa askari doria hao, lakini bado changamoto ya wanyama hao waharibifiu hasa tembo pamoja na kwamba wanakuwa wanaondolewa na kurejea tena ipo katika maeneo hayo na maeneo mengine.

Je, Serikali imefikia hatua gani ya tathmini kwa wananchi 47 waliopata madhara hayo yakiwemo kuharibiwa kwa mazao yao na kusabibisha njaa katika maeneo hayo pia kifo katika Kijiji cha Matuli, Kata ya Bwilingu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa jibu la msingi linaonesha Serikali imeendelea kutoa kutoa elimu kwa wananchi mbalimbali juu ya kujikinga na madhara hayo na elimu moja wapo ilikuwa ikitolewa kwa wanawake kuhusu ufugaji nyuki, na kwa kuwa ziara ya UWT Taifa chini ya Mwenyekiti Mama Chatanda na Mama Shomari, tumekutana na makundi mbalimbali ya wanawake yenye kutaka kufuga nyuki; je, Serikali ina mpango gani wa kushirikiana na Umoja wa Wanawake

Tanzania na Wabunge wanawake ili kusaidia vikundi vinavyotaka kufuga nyuki ikiwemo mtandao wa kufuga nyuki katika Halmashauri ya Chalinze? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hili la nyuki kama unaliweza lijibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Subira Mgalu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hili la matukio 47 ambayo yametokea na wananchi wale bado hawajalipwa, tayari kwa sasa wataalam wetu wapo uwandani, wanafanya tathmini ili kuona ni kwa kiasi gani wananchi wale wanaweza kupewa malipo stahiki kulingana na kile kilichotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika matukio haya 47, matukio 46 yalikuwa ni ya wakulima ambao mashamba yao yameharibiwa na tukio moja lilikuwa ni mwananchi kujeruhiwa. Ninamuomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira wataalam wetu wakimaliza kazi ile nina uhakikia wananchi hawa watapata fidia inayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hili suala la pili la vikundi vya ufugaji nyuki, Wizara ipo tayari kushirikiana na Jumuiya ya Akinamama na Wabunge wa Viti Maalum na Majimbo pale ambapo tutakuwa na vikundi tupo tayari kushirikiana nao kutoa elimu ya ugani, lakini vilevile kutoa mizinga kwa ajili ya kuendeleza ufugaji nyuki nchini. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Ngassa.

Na. 106

**Ujenzi wa Jengo la Mahakama ya Wilaya ya Igunga**

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Jengo la Mahakama ya Wilaya ya Igunga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Mahakama ya Tanzania imeendelea kuimarisha majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kujenga majengo mapya na kukarabati yaliyopo. Kutokana na uhaba wa majengo ya Mahakama majengo haya yanajengwa na kukarabatiwa kwa awamu kwa kuzingatia mpango wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Mahakama na kadri fedha zinavyopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Igunga ni moja ya Wilaya ambazo hazina jengo la Mahakama ya Wilaya kwa muda mrefu. Kwa sasa Mahakama ya Wilaya inafanya kazi ndani ya jengo moja na Mahakama ya Mwanzo Igunga Mjini jengo ambalo lilijengwa kwa ajili ya Mahakama ya Mwanzo. Hivyo, jengo ni finyu kutosheleza Mahakama ya zote mbili kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo na kwa kuzingatia mpango wa ujenzi wa Mahakama, jengo la Mahakama ya Wilaya ya Igunga linatajariwa kujengwa katika bajeti ya mwaka 2024/2025.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngassa.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana, kwanza ninaanza kuishukuru Serikali kwa kutuingiza katika mpango wa ujenzi wa Mahakama yetu ya Wilaya kwa mwaka 2024/2025, kwa kuwa ni jambo ambalo nimelifuatilia kwa miaka mitatu na hatimaye Serikali yetu sikivu imelipokea nashukuru sana upande wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ipo kwenye programu ya kuboresha miundombinu ya Mahakama ikiwepo Mahakama za Mwanzo na Mahakama za Wilaya; je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuambatana na mimi baada ya Bunge hili tuweze kwenda kufanya ziara pale Jimboni Igunga aweze kuona hali ya miundombinu yetu na kwa kuwa wanaendelea na programu ya kuiboresha? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Mbunge Nicholaus George Ngassa kwa kufuatilia ujenzi wa Mahakama ya hii ya Wilaya na niseme kwamba suala la ziara kutembelea maeneo ni jukumu la kimsingi la Mawaziri. Hivyo, ninaridhia nakukubali kuambatana naye kutembelea eneo hili ambapo Mahakama itajengwa, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa muda wetu umekwisha na maswali yamekwisha.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, ni wageni waliokaa Jukwaa la Spika ambao ni wageni wa Mheshimiwa Spika na Rais wa *IPU* kutoka Bunge la Uganda; Kamati ya Bunge ya Maliasili na Nishati wakiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa Dkt. Otiam Emmanuel Otaala; Mheshimiwa Katalihwa Donald Byabazaire, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Feta Geoffrey, Mjumbe; Mheshimiwa Bukenya Christine Sendaula, Mjumbe; na Ndugu Mpitsi Jacquiline Oidu, Katibu Kamati, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 32 wa Mheshimiwa Omari Kipanga, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia; wapiga kura wake kutoka Mafia, Mkoa wa Pwani, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 40 wa Mheshimiwa Anna Lupembe, Wanamaombi kutoka Jijini Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 41 wa Mheshimiwa Ritta Kabati, Kwaya ya *The Vine* kutoka Kanisa la *New Vine Church* ya Jijini Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, wananchi kutoka Kibaha, Mkoa wa Pwani, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 65 wa Mheshimiwa Katani Katani, viongozi wa UWT Wilaya ya Tandahimba, Mkoa wa Mtwara wakiongozwa na Ndugu Arafa. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Iddi Kassim, wapigakura wake kutoka Wilaya ya Kahama Mkoa wa Shinyanga. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 80 kutoka Idara ya Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 40 wa Kwaya ya Erico kutoka Wilaya ya Chamwino Mkoa wa Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Madaktari Bingwa na watumishi mbalimbali wa kada za afya kutoka *Saifee Hospital Tanzania Limited* Dar es Salaam wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji Dkt. Hussein Hassan Ally ambao wapo katika viwanja vya Bunge kwa huduma ya upimaji wa afya ya moyo, karibuni sana madaktari kwa kazi nzuri mnayoifanya. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023

**NAIBU SPIKA:** Mwenyekiti, haya Waheshimiwa inatosha, nadhani haya makofi mmechukua dakika tano zake. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kutoa Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini. Naomba Taarifa hii ya Kamati yote iingie kwenye kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge yaani *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini niwasilishe Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Majukumu na Shughuli za Kamati kwa mwaka 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa hii inajumuisha Shughuli za Kamati zilizotekelezwa katika kipindi cha mwaka mzima yaani Februari, 2023 hadi Januari, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, muundo wa taarifa hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Aidha, uwasilishaji wake unalenga kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu ambayo ni kueleza majukumu yaliyotekelezwa na Kamati kwa kipindi hicho ili yaweze kujadiliwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani ya Kamati kuwa, hatua hii italiwezesha Bunge lako Tukufu kutekeleza jukumu la kuisimamia Serikali kwa niaba ya wananchi na hivyo kuweza kuishauri vyema juu ya hatua stahiki za kuchukua kwa maslahi ya Taifa na kwa kuzingatia ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kuanzia Februari mwaka 2023 hadi Januari mwaka huu, Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini imetekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa Maazimio yaliyotokana na taarifa ya mwaka ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni mwezi Februari, 2023;

(ii) Ziara za ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2022/2023;

(iii) Uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti kwa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2022/2023, na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(iv) Uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti kwa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai hadi Disemba, 2023);

(v) Uchambuzi wa taarifa za utendaji wa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini na Taasisi zilizopo chini yake;

(vi) Uchambuzi wa Mkataba wa *IRENA* wa mwaka 2009 na;

(vii) Ziara za mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya mapendekezo 23 yalitolewa na Kamati na kuazimiwa na Bunge lako Tukufu katika mkutano wa kumi. Maazimio mawili yalitekelezwa kikamilifu, maazimo 20 yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na azimio moja halikutekelezwa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, azimio ambalo halikutekelezwa kabisa linahusu Serikali kuharakisha mchakato wa upatikanaji wa sheria ya joto ardhi hapa nchini kabla ya kukamilika kwa mwaka 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha (Julai – Disemba, 2023) kwa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini. Lengo la kufanya hivyo ni kutathmini ukusanyaji wa maduhuli na upatikanaji wa fedha katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa ukusanyaji wa maduhuli ulikuwa chini ya wastani wa asilimia 50 iliyopaswa kufikiwa katika kipindi hicho kwa Wizara zote. Aidha, upatikanaji wa fedha ulikuwa mzuri kwa Wizara ya Madini kwa kufikia asilimia 67 kwa upande wa Wizara ya Nishati wastani ulikuwa chini ya lengo yaani asilimia 43 huku hali ikiwa duni kwenye fedha za matumizi mengineyo *(OC)* asilimia 12.6. Maelezo zaidi kuhusu utekelezaji wa bajeti wa kipindi cha Julai hadi Disemba 2023 kwa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini yanapatikana katika ukurasa wa 9 hadi wa 12 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi na utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Wizara ya Nishati. Jumla ya taarifa kumi na tatu (13) zinazohusu utendaji wa Wizara ya Nishati na taasisi zake zilichambuliwa na Kamati kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere *(JNHPP),* taarifa iliyowasilishwa kwenye kamati mwezi Januari, 2024 ilionesha kuwa utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 95.83 na malipo ya shilingi trilioni 5.85 sawa na asilimia 89.24 yalikuwa yamefanyika na inatarajiwa mradi huu utakamilika ifikapo Juni, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijulishwa kwamba hadi Januari mwaka 2024 ujazo wa maji ulifikia urefu wa kina cha mita 167 kutoka usawa wa bahari ambacho kinaruhusu kuanzisha uzalishaji wa umeme. Aidha, mtambo wa kwanza wa uzalishaji wa umeme utawashwa na kuzalisha umeme mwezi huu wa Februari, 2024 na mtambo wa pili utawashwa mwezi ujao yaani mwezi Machi, 2024 na kwa pamoja inatarajiwa itazalisha megawati 470 ambazo zitaingizwa kwenye Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya uzalishaji na upatikanaji wa umeme nchini, taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati mwezi Januari, 2024 ilionesha kuwa, hadi mwezi Disemba, 2023 uwezo wa mitambo ya kufua umeme (*installed capacity*) kutoka vyanzo mbalimbali vilivyounganishwa katika Gridi ya Taifa ulifikia *MW* 1,889.84**.** Kiasi hiki ni ongezeko la uwezo wa *MW* 195.29 katika

kipindi cha mwaka mmoja ikilinganishwa na uwezo wa *MW* 1694.55 mwaka 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ongezeko hilo bado uzalishaji wa umeme nchini (*available capacity*) ulikuwa wastani wa *MW* 1200 kiasi ambacho ni kidogo ikilinganishwa na mahitaji ambayo ni *MW* 1,482.80 hali iliyosababisha upungufu wa umeme wastani wa *MW* 283. Hivyo kusababisha maeneo mengi ya nchi kuingia katika mgao wa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia *(LNG)*. Hadi sasa jumla ya futi za ujazo Trilioni 57.54 za gesi asilia zimegunduliwa katika maeneo mbalimbali nchini na kuwezesha uzalishaji kufikia wastani wa futi za ujazo milioni 250 kwa siku hadi kufikia Oktoba, mwaka jana. Asilimia 80 ya gesi inayozalishwa inatumika kuzalisha umeme, jumla ya *MW* 1,198.82 ambayo ni sawa na asilimia 63.82 ya uwezo wote wa uzalishaji umeme nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi hiki cha uzalishaji wa gesi ni kidogo ikilinganishwa na hazina ya gesi iliyogunduliwa na mahitaji ya nchi kutokana na uwezo mdogo wa kifedha, uchakavu wa baadhi ya visima vya gesi. Kamati ilielezwa kuwa, Serikali inachukua hatua za muda mfupi za kuongeza uzalishaji wa gesi yaani futi za ujazo milioni 50.05 ndani ya mwaka 2024. Ni rai ya Kamati kuongeza uzalishaji wa gesi na hivyo kuchangia ongezeko la uzalishaji wa umeme na matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa mafuta hapa nchini. Nchi yetu kwa sasa inapita katika kipindi kigumu cha mfumko wa bei ya mafuta. Jambo hili linaathiri ukuaji wa uchumi kwa kusababisha kwa bei ya bidhaa na huduma kupanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zilizowasilishwa kwenye Kamati mwezi Januari, mwaka huu, zinaonesha kuwa kati ya mwezi Septemba, 2023 hadi Disemba, 2023 jumla ya tani za mafuta 2,083,795 ziliingizwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba mafuta yaliyoingizwa kwa ajili ya matumizi ya ndani

yaliongezeka kwa tani 103,903 sawa na asilimia 10.23 ikilinganisha na tani 1,014,842 zilizoingizwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi hiki kiliingizwa nchini kupitia zabuni 42 zilizoratibiwa na Wakala wa Uingizaji wa Mafuta kwa pamoja. Kati ya zabuni hizo, shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC)* lilishinda zabuni moja tu ya kuagiza mafuta ya dizeli na zabuni 41 zilienda kwenye kampuni saba za binafsi na kampuni moja haikushinda zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uendelezaji wa leseni za Shirika la Taifa la Madini (*STAMICO);* hadi Agosti, 2023 Shirika lilikuwa linamiliki jumla ya leseni 167. Katika ya hizo, wamefanya utafiti leseni 24 na hivyo leseni 43 zinahitaji utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipata mafunzo kuhusu wajibu wa wamiliki wa leseni za miradi ya madini ikiwemo inayomilikiwa na *STAMICO*. Ili kutatua changamoto zinazohusu *CSR,* Serikali ilitunga kanuni za wajibu wa wamiliki wa leseni za madini kwa jamii za mwaka 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni hizo zimeainisha mambo kadhaa ikiwemo mmliki wa leseni kuwajibika kuishirikisha Halmashauri ya Kijiji au Mtaa unaoguswa na mradi katika kuainisha vipaumbele vya jamii wakati wa zoezi la kuandaa mpango na wajibu wake katika jamii. Aidha, kazi zote zinazohusu usimamizi wa wajibu wa mmliki wa leseni zitakuwa chini ya Kamati ya wataalam itakayoundwa. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Kamati ya wataalam imetoa majukumu ya kuhakikisha jamii inanufaika na uwepo wa miradi inayohusu madini katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo muundo wake unatia mashaka kwani hauna uwakilishi wa wananchi kutoka maeneo yanayoizunguka utekelezaji wa mradi jambo ambalo lanaweza kuibua malalamiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo zaidi kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini na

mambo yanayobainika ni kama inavyoonekana katika ukurasa wa 12 hadi 48 ya Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na mapendekezo, Wizara ya Nishati, utekelezaji na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina;

Kwa kuwa, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka hazina (hasa za nje) hauridhishi kwani hadi kufikia Disemba, 2023 ulikuwa kwa wastani wa asilimia 42 (fedha za nje (*IMF*) kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)* hazikupatikana kabisa);

Kwa kuwa, hali hiyo inachangia Wizara na taasisi zake kushindwa kutekeleza kikamilifu majukumu yaliyopangwa na hivyo kuathiri huduma tarajali kwa wananchi kutoka katika Wizara na taasisi zake.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Serikali ihakikishe fedha zinazoidhinishwa kwa Wizara ya Nishati na Taasisi zake zinapatikana kwa utoshelevu na kwa wakati,

(b) Serikali ijielekeze kutenga fedha kutoka vyanzo vya ndani ili kuepuka adha ya utegemezi wa fedha za nje ambazo mara nyingi hazipatikani kwa uhakika na kwa wakati na kwa uhakika,

(c) Serikali iboreshe mfumo wa ufuatiliaji wa fedha za nje zilizotengwa kwenye bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya usambazaji na upatikanaji wa umeme nchini;

Kwa kuwa, hali ya usambazaji na upatikanaji wa umeme nchini siyo ya kuridhisha kutokana na ukame, uhaba wa gesi, uchakavu wa miundombinu na uchache wa vituo vya kupoza umeme;

Na kwa kuwa, hali hiyo inaathiri uzalishaji wa bidhaa na huduma nchini huchangia ongezeko la mfumko wa bei na hivyo kuadhiri ukuwaji wa uchumi kwa ujumla.

Kwa Hiyo Basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Serikali ihakikishe mradi wa bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere unakamilika haraka kwa kuanza uzalishaji kuanzia,

(b) Februari, 2024 kama ilivyoahidi ili kuongeza umeme nchini,

(c) Serikali ihakikishe mradi wa kufunga mitambo ya kupoza hewa *(chillar)* katika kituo cha Kinyerezi I *Extension* ili kuongeza uzalishaji wa umeme kutoka MW 160 hadi MW 185 unakamilika ifikapo Disemba, 2024,

(d) Serikali ihakikishe mitambo ya kuzalisha umeme inafanyiwa ukarabati wa mara kwa mara ili kuepuka uchakavu ambao unaathiri uwezo wa mitambo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya mafuta kuwa juu.

Kwa kuwa, bei ya mafuta inaendelea kuwa juu kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na uhaba wa fedha za kigeni, gharama za kubadlisha fedha za kigeni *(exchange rate),* ukosefu wa maabara za kupima ubora wa mafuta katika bandari za Mtwara na Tanga, na ufinyu wa maghala ya kuhifadhia mafuta;

Na kwa kuwa, hali hiyo inachangia ongezeko la mfumko wa bei kwenye bidhaa na huduma nchini na hivyo kuchangia ongezeko la gharama za maisha na kuibua hisia za chuki miongoni mwa wananchi dhidi ya Serikali.

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba;

(a) Serikali ikamilishe upanuzi wa miundombinu ya Bandari ya Dar es Salaam na ujenzi wa maabara za kupima ubora mafuta katika Bandari za Tanga na Mtwara ili kuongeza kasi na uwezo wa upatikanaji wa mafuta;

(b) Serikali ichukue hatua madhubuti kuhakikisha nchi inajitosheleza katika akiba ya fedha za kigeni hususani dola za Marekani;

(c) Serikali ichukue hatua ili kuongeza uwezo wa maghala ya kuhifadhia mafuta na hivyo kuiwezesha nchi kuwa na akiba ya kutosha ya mafuta; na

(d) Serikali iiwezeshe *TPDC* kwa kuijengea mazingira wezeshi kibiashara ili iweze kushindana kwenye soko la ndani na nje ya nchi na hivyo kuihakikishia nchi usalama wa mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ongezeko la magari yanayotumia gesi asilia *(CNG)* dhidi ya vituo vya kujaza vilivyopo;

Kwa kuwa, matumizi ya gesi asilia kwenye magari yameongezeka nchini kutoka 1139 mwaka 2020/2021 hadi magari 3000 mwaka 2022/2023) kutokana na unafuu wa gesi wa takribani asilimia 40 ikilinganishwa na *petrol* na diseli.

Na kwa kuwa, ongezeko la magari linasababisha foleni kwenye vituo vitano vya kujaza gesi vilivyopo nchini yaani Dar es salaam, Pwani na Mtwara na hivyo wenye magari kulazimika kutumia muda mrefu katika kusubiri kujaza gesi.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba;

Serikali iongeze idadi ya mtandao wa vituo vya kujaza gesi kwenye magari nchini kwa kuanza na maeneo ambayo taratibu za awali za ujenzi zimeanza yaani Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma na vituo vya *GPSA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama na uhaba wa wakaguzi wa mfumo wa gesi asilia kwenye magari;

Kwa kuwa, magari mengi yanayoingizwa nchini hayana mfumo wa kutumia gesi asilia hivyo yanalazimika kuwekwa mfumo huo nchini na wamiliki watahitaji;

Na kwa kuwa, baadhi ya wamiliki wa magari wanashindwa kuweka mfumo wa kutumia gesi asilia kwenye magari kutokana na gharama yaani shilingi 2,000,000 kwa gari, uchache wa wakaguzi wa mfumo nchini (10) na uchache wa karakana zipo nne.

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba;

(a) Serikali ichukue hatua zitakazowezesha kupunguza gharama za kufunga mfumo wa kutumia gesi kwenye magari;

(b) Serikali ichukue hatua za kuongeza idadi ya wakaguzi wa mfumo wa magari yanayotumia gesi asilia; na

(c) Serikali ianze kuhamasisha uingizaji wa magari nchini yenye mfumo wa kutumia wa gesi asilia ili kupunguza gharama za kuweka mfumo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Madini; kuhusu kusuasua kwa fidia kwa wananchi wanaopisha miradi ya uchimbaji wa madini.

Kwa kuwa, kumekuwa na uchelewashaji wa fidia kwa wananchi wanaohama kwenye maeneo yao ili kuruhusu utekelezaji wa miradi ya uchimbaji wa madini;

Na kwa kuwa, hali hiyo inachangia kudidimiza wananchi kiuchumi kutokana na kutoruhusiwa kufanya shughuli za kimaendeleo na kijamii katika maeneo hayo na hivyo kujenga chuki dhidi ya wawekezaji na serikali;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba;

(a) Serikali isimamie kikamilifu suala la fidia na kuhakikisha wananchi wanalipwa kwa wakati ili kuondoa malalamiko dhidi ya serikali na kuwakwamua dhidi ya athari za kiuchumi, kisaikolojia na kijamii;

(b) Serikali ihakikishe wawekezaji wanaweka fedha katika mfuko wa fidia ya ardhi kabla ya kuwaondoa wananchi katika

maeneo yao jambo litakalowahakikishia wananchi hao kulipwa fidia na kwa wakati;

(c) Serikali ihamasishe wananchi kulipwa fidia kwa njia ya kupewa hisa huru katika miradi ya uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uboreshaji wa Sheria na Kanuni katika Sekta ya Madini.

Kwa Kuwa, baadhi ya changamoto zinazoikabili sekta ya madini zinachangiwa na udhaifu kwenye baadhi ya sheria na kanuni za sekta ya madini.

Na kwa kuwa, udhaifu huo unaathiri masuala mbalimbali ikiwemo usimamizi wa baruti, usimamizi wa biashara ya makinikia na uchenjuaji wa madini ghafi, uratibu wa masoko na maonesho ya kimataifa ya madini na biashara ya madini ya Tanzanite;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iharakishe ukamilishaji wa mchakato wa;

(a) Kutunga sheria ya usimamizi wa baruti nchini kwani iliyopo ya mwaka 1963 imepitwa na wakati;

(b) Kufanya marekebisho ya sheria ya Madini, Sura ya 123 ili kuwezesha usimamizi wa biashara ya makinikia na uchenjuaji wa madini ghafi nchini;

(c) Kurekebisha Kanuni za Eneo Tengefu la Mirerani ili kuruhusu biashara ya madini ya Tanzanite yaliyosanifiwa (kukatwa na kung'arishwa) kufanyika pia maeneo mengine nje ya Mirerani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wa sera, sheria na kanuni kuhusu wajibu wa mmiliki wa leseni za madini kwa jamii *(corporate social responsibility-CSR)*.

Kwa kuwa, utoaji na upatikanaji wa huduma za kijamii *(CSR)* unasuasua kutokana na baadhi ya wamiliki wa leseni za uchimbaji wa madini kuchukulia jambo hilo kuwa hisani, jambo ambalo ni

kinyume na kanuni za wajibu wa wamiliki wa leseni za madini kwa jamii za mwaka 2023;

Na kwa kuwa, jambo hilo linachangia jamii zinazozunguka miradi ya uchimbaji madini kutonufaika na huduma za kijamii *(CSR)* kutoka kwa mwekezaji pamoja na kusababisha migogoro baina ya wawekezaji na jamii hizo.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe inasimamia kikamilifu utekelezaji wa kanuni za wajibu wa wamiliki wa leseni za madini kwa jamii za mwaka 2023 ili wamiliki wa leseni watimize wajibu wao kikamilifu na jamii husika ziweze kunufaika na uwekezaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Kwa namna ya pekee napenda nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, (Mbunge); kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu katika utekelezaji wa majukumu yake. Pia, nakushukuru wewe Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, (Mbunge); pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa namna wanavyokusaidia katika kuendesha vikao vya Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa kuniamini mimi pamoja na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, (Mbunge) na kuendelea kutupa ushirikiano uliowezesha utekelezaji bora wa majukumu ya Kamati. Kwa namna ya kipekee naomba majina yao yatambuliwe na kuingizwa kwenye kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, napenda kumshukuru Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko, Mbunge, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati na Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, Mbunge, Waziri wa Madini, kwa ushirikiano wao mzuri wanaotupatia katika kutekeleza majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, namshukuru Mheshimiwa Judith Kapinga, Naibu Waziri wa Nishati na Mheshimiwa Stephen Kiruswa, (Mbunge), Naibu Waziri wa Madini kwa namna wanavyowasaidia Waheshimiwa Mawaziri wao na hivyo kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninamshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Mramba na Naibu wake Ndugu Athuman Mbuttuka, Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini Ndugu Khery Mahimbali na Naibu wake Ndugu Msafiri Mbibo kwa namna wanavyowaongoza watendaji wa Wizara na Taasisi zake na kwa ushirikiano mzuri wanaoipa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc,* kwa namna anavyoongoza Watendaji wa Ofisi ya Bunge. Jambo ambalo limechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza kikamilifu majukumu yake ya kikatiba na kukamilisha maandalizi ya taarifa hii kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukurani hizo, naliomba Bunge lako Tukufu lipokee na kuijadili taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KUHUSU SHUGHULI ZA KAMATI KWA MWAKA 2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA BUNGENI

## SURA YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini niwasilishe

Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Majukumu na Shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2023 hadi Januari, 2024.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** muundo wa taarifa hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 na imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

(a) Sehemu ya Kwanza inahusu utangulizi ambao unatoa maelezo ya jumla ya Utangulizi ikijumuisha mbinu zilizotumika katika kutekeleza majukumu ya Kamati;

(b) Sehemu ya Pili ambayo inatoa maelezo kamili kuhusu namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake na masuala yaliyobainika kutokana na utekelezaji wa kazi hizo; na

(c) Sehemu ya Tatu ambayo inaeleza maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati.

### 1.3 Madhumuni ya Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, uwasilishaji wa taarifa hii unalenga kueleza majukumu ambayo Kamati imeyatekeleza kwa kipindi cha Februari, 2023 hadi Januari, 2024. Kwa ujumla taarifa inaonesha hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa masuala mbalimbali chini ya Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini. Aidha, taarifa inabainisha maeneo yenye mafanikio pamoja na yale yenye changamoto.

**Mheshimiwa Spika**, ni imani ya Kamati kuwa, hatua hii italiwezesha Bunge lako Tukufu kutekeleza jukumu la kuisimamia Serikali kwa niaba ya wanachi na hivyo kuweza kuishauri vyema juu ya hatua stahiki za kuchukua kwa maslahi ya Taifa na kwa kuzingatia ustawi wa wananchi. Hatua hii ni utekelezaji wa matakwa ya Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

### 1.4 Njia na Mbinu zilizotumika

**Mheshimiwa Spika,** ili kuboresha utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ya Nishati na Madini ilitumia njia na mbinu mbalimbali kama ifuatavyo: **-**

a) Vikao vya kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Wizara na Taasisi zake kwa lengo la kutathmini utendaji, mafanikio na changamoto zinazowakabili;

b) Ziara za ukaguzi wa miradi mbalimbali iliyotengewa fedha kwa lengo la kutathmini hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wake; na

c) Semina na ziara za mafunzo.

### 1.5 Msingi wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika,** msingi wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge unatokana na Ibara ya 96(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977[1] . Ni kwa kuzingatia muktadha huo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imeundwa kupitia Kanuni ya 137[2] ikisomwa pamoja na Kifungu cha 5(k) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 6(11) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Nishati na Madini imepewa wajibu wa kusimamia shughuli zinazotekelezwa na Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini. Vilevile, kifungu cha 7(1)(a-d) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kimeainisha majukumu yafuatayo kwa Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta ikiwemo Kamati ya Nishati na Madini: -

a) Kushughulikia bajeti ya Wizara na taasisi inazozisimamia;

b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara

---

[1] 96.-(1) Bunge laweza kuunda Kamati za Bunge za namna mbalimbali kadri litakavyoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa madaraka yake.

[2] 137.-(1) Kutakuwa na Kamati za Kudumu za Bunge kama zilivyoainishwa kwenye Nyongeza ya Nane ya Kanuni hizi.

inazozisimamia kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 136 (14)[3] ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023;

c) Kushughulikia taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na

d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu katika Wizara hizo.

**SURA YA PILI**

## 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kuanzia Februari, 2023 hadi Januari, 2024, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imetekeleza shughuli zifuatazo: -

(a) Uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa Maazimio yaliyotokana na taarifa ya mwaka ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni mwezi Februari, 2023;

(b) Ziara za ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2022/2023;

(c) Uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti kwa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, na mwelekeo wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(d) Uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti kwa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini kwa kipindi cha Nusu mwaka (Julai hadi Disemba, 2023);

(e) Uchambuzi wa taarifa za utendaji wa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini na Taasisi zilizopo chini ya Wizara hizo;

(f) Uchambuzi wa Mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu wa Mwaka 2009 (*Statute of the International Renewable Energy Agency -IRENA*); na

[3] Kamati yoyote ambayo Spika atapeleka kwake kwanza Muswada au jambo lingine lolote, itahesabiwa kuwa ndiyo Kamati inayohusika kushughulikia Muswada au jambo hilo.

(g) Ziara za mafunzo.

**2.1.1 Uchambuzi wa utekelezaji wa Maazimio yaliyotokana na Taarifa ya Mwaka ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni Mwezi Februari, 2023**

**Mheshimiwa Spika,** jumla ya mapendekezo ishirini na tatu (23) yalitolewa na Kamati na kuazimiwa na Bunge lako Tukufu katika mkutano wa kumi. Kwa ujumla, maazimio hayo yalilenga kuhakikisha Serikali inatekeleza kikamilifu majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika vikao vya Kamati vilivyofanyika Mwezi Januari, 2024**,** Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili taarifa ya utekelezaji wa maazimio hayo kutoka Wizara zote mbili inazozisimamia. Katika uchambuzi huo, Kamati imebaini yafuatayo: -

a) Maazimio mawili (2) sawa na asilimia tisa (9%) yametekelezwa kimamilifu.

b) Maazimio ishirini (20) sawa na asilimia themanini na saba (87) yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

c) Azimio moja (1) sawa na asilimia nne (4%) halijatekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya maazimio ya Bunge yaliyotekelezwa kikamilifu ni pamoja na: -

(a) Kuwawajibisha watu wote waliozembea na kusababisha kupasuka kwa Bwawa la Williamson Diamond Ltd na

(b) Kusimamiwa kikamilifu kwa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali ikiwemo usimamizi wa ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme la **JNHPP** ambao umekamilika kwa **asilimia 95.83** na majaribio ya kuzungusha mitambo kwa ajili kuzalisha umeme yameanza mwezi Januari, 2024.

Aidha, pamoja na mafanikio katika utekezaji wa maazimio hayo, kamati imebaini kwamba azimio moja halijatekelezwa, ambalo linahusu Serikali kuharakisha mchakato wa upatikanaji wa Sheria ya Jotoardhi nchini kabla ya kukamilika kwa mwaka 2023.

**Mheshimiwa Spika,** hadi sasa Serikali haijawasilisha Bungeni muswada utakaowezesha kutungwa kwa sheria hiyo. Ni rai ya Kamati kwamba Bunge lako tukufu liisisitize Serikali juu ya umuhimu wa kutekeleza azimio hili kikamilifu na kwa wakati ili kuwezesha nchi kuwa na mwongozo wa kisheria katika usimamizi wa jotoardhi.

**2.1.2 Ziara za Ukaguzi wa Miradi iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023 inaweka masharti kwa Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati ya Nishati na Madini ya kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha. Ili kuzingatia masharti haya, Kamati ilifanya ziara katika Mkoa wa Dodoma, Tanga, Pwani na Dar es Salaam. Katika mikoa hiyo, kamati ilikagua jumla ya miradi saba (7) iliyo chini ya Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini. Masuala yaliyobainika katika ukaguzi wa miradi hiyo yaliwasilishwa Bungeni kupitia Taarifa za Kamati kuhusu uchambuzi wa bajeti za Wizara hizo mwezi Aprili na mwezi Juni, 2023.

**2.1.3 Uchambuzi wa Bajeti**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Bajeti za Wizara inazozisimamia ikiwa ni utekelezaji wa masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023. Taarifa hizo zilibainisha masuala mbalimbali kama vile hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, ambazo zilieleza kwa kina kuhusu utekelezaji wa vipaumbele na majukumu ya Wizara, hali ya ukusanyaji wa maduhuli na upatikanaji wa fedha.

Aidha, taarifa hizo zilieleza mwelekeo wa bajeti inayofuata ikijumuisha maeneo ya vipaumbele, makadirio ya makusanyo ya maduhuli na makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Pamoja na mambo mengine, taarifa hizo zilionesha ongezeko la bajeti za Wizara zote mbili ambazo ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi wa Taifa letu. Kwa upande wa Wizara ya Nishati (Fungu 58) bajeti iliongezeka kutoka shilingi 2,905,981,533,00.00 mwaka 2022/2023 hadi kufikia shilingi 3,048,632,519,000.00 mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 4.9. Kwa upande

mwingine bajeti ya Wizara ya Madini (Fungu 100) iliongezeka kwa asilimia 7 kutoka shilingi 83,445,260,000.00 katika mwaka wa fedha 2022/2023 hadi kufikia shilingi 89,357,491,000.00 katika mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza bajeti katika wizara hizi ambazo zina mchango katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

### 2.1.4 Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba, 2023)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili taarifa kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai – Disemba, 2023) kwa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini. Lengo lilikuwa ni kutathmini mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli na upatikanaji wa fedha ili kuweza kuishauri Serikali ipasavyo hasa ikizingatiwa kuwa katika kipindi hicho, ukusanyaji wa maduhuli na upatikanaji wa fedha unatakiwa kufikia angalau asilimia 50.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi huo ni kama ifuatavyo: -

**a) Wizara ya Nishati**

Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ilipangiwa kukusanya maduhuli ya **Shilingi 20,392,000.00**. Hadi kufikia Disemba 2023, kiasi cha **Shilingi 4,915,826.02** kimekusanywa sawa na **asilimia 24.11**. Aidha, kwa upande wa bajeti, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 1,310,852,090,180.49** ambayo ni sawa na **asilimia 43** ya kiasi cha **Shilingi 3,048,632,519,000** kilichoidhinishwa na Bunge kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 1.**

Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, upatikanaji wa fedha za matumizi mengineyo (OC) siyo wa kuridhisha kwani kiasi kilichopokelewa ni **Shilingi 9,029,849,765.76** sawa na **asilimia 12.6** ya kiasi kilichoidhinishwa cha shilingi **71,637,112,000**. Kutokupokelewa kwa fedha hizi kulitokana na Wizara kutokupokea fedha za IMF **shilingi 53,200,000,000** kupitia *ECF* kwa ajili ya kutekeleza miradi ya TANESCO (Gridi imara) na REA (HEP) na OC ya Wizara na taasisi zake za PURA na TPDC. Kukosekana kwa fedha hizi kunachangia kutokukamilika kwa miradi

iliyokusudiwa na watumishi kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

**Kielelezo Na. 1: Upatikanaji wa Fedha kwa Wizara ya Nishati kwa kipindi cha Julai - Disemba, 2023**

| AINA | KILICHOIDHINISHWA | KILICHOPOKELEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **MISHAHARA** | 16,292,586,000 | 8,504,475,706.86 | 52.2 |
| **OC** | 71,637,112,000 | 9,029,849,765.79 | 12.6 |
| **MAENDELEO NDANI** | 2,609,156,128,000 | 1,048,268,417,405.14 | 40.18 |
| **MAENDELEO NJE** | 351,546,693,000 | 245,049,347,302.73 | 69.70 |
| **JUMLA** | 3,048,632,519,000 | 1,310,852,090,180.49 | 43.00 |

**Chanzo:** Taarifa ya Wizara ya Nishati ya Januari, 2023 na usanifu wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba kwa ujumla upatikanaji wa fedha uko chini ya lengo ukilinganisha na kiasi kilichotarajiwa kupokelewa katika kipindi hicho. Ni ushauri wa Kamati kwamba serikali ihakikishe fedha zinazotengwa na kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu zinatolewa kwa wakati na kikamilifu ili kutoathiri utendaji kazi wa Wizara.

**b) Wizara ya Madini**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ilipangiwa kukusanya maduhuli ya **Shilingi 1,006,705,169,300**. Hadi kufikia Disemba 2023, Wizara ilikuwa imekusanya Shilingi **403,226,887,503.43** sawa na **asilimia 40.05** ya lengo. Kwa upande wa bajeti, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 110,530,115,847.01** kati ya **Shilingi 163,008,241,000.00** zilizoidhinishwa na Bunge sawa na **asilimia 67.81**. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, fedha za matumizi mengineyo (OC) ni **shilingi 23,097,988,584.79** na Mishahara ni **shilingi 10,708,179,719.83** mtawalia. Aidha, fedha zilizopokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni **shilingi 75,830,808,750.17** kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 2.**

**Kielelezo Na. 2: Upatikanaji wa Fedha kwa Wizara ya Madini kwa kipindi cha Julai - Disemba, 2023**

| AINA | KILICHOIDHINISHWA | KILICHOPOKELEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| MISHAHARA | 20,307,498,000 | 10,708,179,719.83 | 52.73 |
| OC | 45,877,443,000 | 23,991,127,377.01 | 52.29 |
| MAENDELEO NDANI | 96,823,300,000 | 75,830, 808,750.17 | 78.32 |
| JUMLA | 163,008,241,000.00 | 110,530,115,847.01 | 67.81 |

**Chanzo:** Taarifa ya Wizara ya Madini ya Januari, 2023 na usanifu wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba ukusanyaji wa maduhuli upo chini ya lengo jambo linaloweza kuathiri utendaji kazi wa Wizara. Ni ushauri wa Kamati kwamba serikali ihakikishe inakusanya maduhuli kikamilifu kadri yalivyotengwa na kuidhinishwa na Bunge lako tukufu ili kutoathiri utendaji kazi wa Wizara.

### 2.1.5 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina wajibu wa kufuatilia utendaji wa Wizara inazozisimamia ikiwa ni utekezaji wa Masharti ya Kifungu cha 7(1)(d)[4] cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika vikao vilivyofanyika mwezi Agosti, 2023, Oktoba, 2023 na Januari, 2024, Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili taarifa mbalimbali za utendaji wa Wizara inazozisimamia kama ifuatavyo: -

### (a) Wizara ya Nishati

**Mheshimiwa Spika**, jumla ya taarifa kumi na tatu (13) zinazohusu utendaji wa Wizara ya Nishati na taasisi zake zilichambuliwa na Kamati kama ifuatavyo: -

[4] Majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge za kisekta yatakuwa Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo.

**i) Utekelezaji wa Mradi wa Bwawa la kufua umeme la Julius Nyerere (JNHPP)**

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ya Wizara ilionesha kuwa, hadi kufikia tarehe 31 Julai, 2023 utekelezaji wa mradi huu kwa ujumla ulikuwa umefikia **asilimia 90.19**. Hali kadhalika hadi tarehe 31 Julai, 2023, malipo ya utekelezaji wa mradi huo yalikuwa Shilingi **Trilioni 5.53** sawa na **asilimia 84.3** ya gharama yote ya mradi wa shilingi Trilioni 6.558.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa iliyowasilishwa kwenye kamati mwezi Januari, 2024 ilionesha kuwa Mradi huo umefikia **asilimia 95.83** ambapo tayari malipo ya shilingi **trilioni 5.85** sawa na **asilimia 89.24** yalikuwa yamefanyika. Aidha, inatarajiwa kuwa mradi huu utakamilika ifikapo mwezi Juni, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu kujaza maji kwenye bwawa, hadi kufikia Januari, 2024 ujazaji ulifikia urefu wa kina cha mita 167 kutoka usawa wa bahari. Kiasi hicho kinatosha kuanza uzalishaji wa umeme. Kutokana na hali hiyo, tarehe 8 januari, 2024 Wizara ilisafirisha umeme kutokea chalinze hadi kwenye bwawa kwa lengo la kufanya majaribio ya mitambo ya kufua umeme. Kamati ilielezwa kuwa mtambo wa kwanza utaanza kuzalisha umeme mwezi Februari 2024 na mtambo wa pili mwezi Machi, 2024 ambayo kwa pamoja inatarajiwa kuzalisha umeme wa **MW 470** ambazo zitaunganishwa kwenye gridi ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi wa JNHPP unaenda sambamba na utekelezaji wa mradi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 yenye urefu wa kilomita miamoja sitini (160) kutoka kituo cha kuzalisha umeme JNHPP hadi Chalinze. Mradi huo unagharimu Shilingi **Bilioni 158**. Pia unaenda sambamba na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Chalinze chenye uwezo wa MVA 1,500 unaogharimu Shilingi **Bilioni 124**. Miradi yote ilipangwa kukamilika Desemba, 2023. Hata hivyo, haikuwezekana kutokana na sababu mbalimbali. Kamati ilijulishwa kuwa mradi utarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Februari, 2024.

### ii) Hali ya Uzalishaji na Upatikanaji wa Umeme Nchini

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imekuwa na utaratibu wa kupokea taarifa kuhusu uzalishaji na usambazaji wa umeme nchini. Lengo la kufanya hivyo ni kufahamu mafanikio na changamoto zinazoikabili sekta ya umeme nchini ili kuwa katika nafasi nzuri ya kuishauri na kuisimamia Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa iliyowasilishwa kwenye kamati katika vikao vya mwezi Januari, 2024 ilionesha kuwa hadi kufikia mwezi Desemba, 2023 uwezo wa mitambo ya kufua umeme (*installed capacity*) kutoka vyanzo mbalimbali vilivyounganishwa katika Gridi ya Taifa ulifikia **MW 1,889.84.** Kiasi hiki ni ongezeko la uwezo wa **MW 195.29** katika kipindi cha mwaka mmoja ikilinganishwa na uwezo wa **MW 1694.55**[5] mwaka 2022. Pamoja na ongezeko hilo bado uzalishaji wa umeme nchini (*available capacity*) ulikuwa wastani wa **MW 1200** kiasi ambacho ni kidogo ikilinganishwa na mahitaji ambayo ni **MW 1,482.80** na hivyo kusababisha upungufu wa umeme wastani wa **MW 283.**

**Mheshimiwa Spika**, sababu za uzalishaji wa umeme kuwa mdogo ni pamoja na upungufu wa maji kwenye mabwawa tegemezi yakiwemo mtera, kidatu na kihansi, uchakavu wa mitambo ya kuzalishia umeme na miundombinu ya kusafirishia umeme, na upungufu wa gesi ya kuzalishia umeme. Aidha, athari za upungufu huo wa umeme ni maeneo mengi ya nchi kuingia katika mgao wa umeme.

### iii) Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia (LNG)

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania imekuwa ikifanya shughuli za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa gesi asilia ambapo hadi sasa jumla ya futi za ujazo **Trilioni 57.54** za gesi asilia zimegunduliwa katika maeneo mbalimbali nchini. Ugunduzi huo, umewezesha uzalishaji wa gesi asilia nchini kufikia wastani wa futi za ujazo **milioni 250** (250mmscfd) kwa siku hadi kufikia mwezi Oktoba, 2023. Uzalishaji huu ni ongezeko la **asilimia 13.3** ukilinganisha na uzalishaji wa futi za uzajo **Milioni 220.6** uliofikiwa katika kipindi

---

[5] Taarifa ya Kamati ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Kwa kipindi cha Februari, 2022 hadi Januari, 2023, ukurasa wa 12.

kama hicho mwaka 2022[6]. Aidha, **asilimia 80** ya gesi inayozalishwa inatumika kuzalisha umeme jumla ya **MW 1,198.82** ambazo ni sawa na **asilimia 63.82** ya umeme wote unaozalishwa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, kiasi hiki cha uzalishaji ni kidogo ikilinganishwa na hazina ya gesi iliyogunduliwa na mahitaji ya nchi kutokana na uwezo mdogo wa kifedha na uchakavu wa baadhi ya visima vya gesi. Katika kukabiliana na hali hii, Kamati ilielezwa kuwa Serikali inachukua hatua za muda mfupi za kuongeza uzalishaji wa gesi futi za ujazo **milioni 50.05** ndani ya mwaka 2024 kwa: -

(a) Kuongeza msukumo wa gesi kwenye visima na mabomba ya gesi katika kitalu cha songosongo;

(b) Kukarabati kisima cha songosongo Namba 7;

(c) Kutoboa maeneo mapya ya kuzalisha gesi katika visima vya Mnazi bay Mbili na Mnazi bay tatu (MB 2 na MB 3); na

(d) Kuchoronga visima viwili (2) vya uzalishaji wa gesi asilia katika kitalu cha mnazi bay.

**Mheshimiwa Spika,** ni rai ya kamati kwamba Serikali iongeze kasi ya kutekeleza miradi hii iliyopo katika hatua za muda mfupi ili kuongeza uzalishaji wa gesi asilia na hivyo kuchangia ongezeko la uzalishaji wa umeme na matumizi mengineyo**.**

**iv) Mradi wa kusambaza umeme Vijijini (REA) awamu ya Tatu Mzunguko wa pili**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unahusu usambazaji wa umeme kwenye Mikoa 24 ya Tanzania Bara na unagharimu kiasi cha Shilingi **trilioni 1.593**. Mradi unahusisha kujenga njia za umeme Msongo Mdogo **kilomita 12,447**, njia za umeme Msogo wa kati jumla ya **kilomita 23,669** na kuunganisha umeme kwenye **vijiji 4,071** vyenye wateja wa **awali 89,562**.

[6] Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa Kipindi cha Februari, 2022 hadi Januari, 2023, ukurasa wa 23

Hadi kufikia Disemba, 2023 umeme ulikuwa umewashwa kwenye **vijiji 3,335** sawa na **asilimia 82** na kuunganishia jumla ya wateja wa **awali 41,622** sawa na **asilimia 46.5**. Aidha, jumla ya kilomita 7,086.48 za njia ya msongo mdogo sawa na **asilimia 57** na njia za msongo wa kati kilomita 21,669 zimekamilika sawa na **asilimia 92.**

**Mheshimiwa Spika**, kasi ya utekelezaji wa mradi huu ilionekana kuwa ya kusuasua kutokana na sababu mbalimbali ambapo kamati iliiagiza serikali kuchukua hatua za makusudi katika kukabiliana na hali hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, ingawa takwimu za jumla zinaonesha kwamba kati ya **vijiji 4,071** vilivyo kwenye mradi ni **vijiji 3,335** sawa na **asilimia 82** ndio vimefikiwa na umeme, bado idadi ya wananchi ambao wameunganishiwa na umeme iko chini kwani kati ya **wateja 89,562** waliokusudiwa ni **wateja 41,622** sawa na **asilimia 46.5** ndio wameunganishiwa na huduma ya umeme. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa hali hiyo inachangiwa na ukosefu wa nguzo katika maeneo husika kwa ajili ya ujenzi wa njia za msongo mdogo. **Ni rai ya Kamati kuwa Serikali ichukue hatua za makusudi ili kuongeza mtandao wa njia za msongo mdogo vijijini ili kuondoa malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusiana na kutopata huduma ya umeme licha ya kwamba umefika kwenye vijiji vyao**.

**v) Hali ya upatikanaji wa Mafuta Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** nchi yetu kwa sasa inapita katika kipindi kigumu cha mfumuko wa bei ya mafuta. Jambo hili linaathiri ukuaji wa uchumi kwa kuwa linasababisha kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma. Kutokana na hali hii, Kamati imejiwekea utaratibu wa kuitaka Serikali kuwasilisha hali ya upatikanaji wa mafuta nchini katika vikao vyake mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** takwimu zilizowasilishwa kwenye Kamati mwezi Januari, 2024 zinaonesha kuwa kati ya mwezi Septemba, 2023 hadi Desemba, 2023 jumla ya Tani za mafuta **2,083,795** ziliingizwa nchini ambapo kati ya hizo, **tani 1,118,746** sawa na **asilimia 53.7** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya ndani na tani 965,049 sawa na **asilimia 46.3** zilikuwa kwa ajili ya kwenda nchi Jirani (*on transit)*.

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba mafuta yaliyoingizwa kwa ajili ya matumizi ya ndani yaliongezeka kwa **tani 103,903** sawa na **asilimia 10.23** ikilinganisha na **tani 1,014,842** zilizoingizwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022.

Kiasi hiki kiliingizwa nchini kupitia zabuni arobaini na mbili (42) zilizoratibiwa na Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa pamoja (PBPA). Kati ya zabuni hizo, shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) lilishinda zabuni moja (1) tu ya kuagiza mafuta ya dizeli na zabuni 41 zikienda kwenye kampuni saba (7) za binafsi na kampuni moja haikushinda zabuni.

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo wa biashara ya mafuta nchini unaonesha kwamba bei ya mafuta iliendelea kuwa juu kutokana na sababu zifuatazo: -

(a) Kupanda kwa bidhaa hiyo katika soko la dunia;

(b) Vita baina ya Urusi na Ukraine ambayo imesababisha upungufu wa meli za kusafirisha mafuta na ongezeko la bima;


(c) Uhaba wa fedha za kigeni hususani Dola ya Kimarekani nchini;

(d) Gharama za meli kusubiri kushusha mafuta bandarini kwa muda mrefu kutokana na uwezo mdogo wa miundombinu ya upokeaji wa mafuta katika bandari ya Dar es Salaam; na

(e) Kuongezeka kwa gharama za kubadilisha fedha za kigeni dhidi ya shilingi ya Tanzania *(exchange rate*) kama ilivyo kwenye Kilelezo Na. 3.

Aidha, uchambuzi zaidi wa Kamati ulibaini kuwa uwezo mdogo wa maghala ya kuhifadhia mafuta yaliyopo nchini pia unachangia ongezeko la bei ya mafuta kwani nchi haina uwezo wa kuhifadhi mafuta kwa muda mrefu. Mathalani, uagizaji wa mafuta kwa mwezi umeongezeka kutoka wastani wa **tani 300,000** kwa mwezi mwaka 2012 hadi kufikia **tani 600,000** kwa mwezi mwaka 2022 ambapo miundombinu ya kuhifadhia mafuta haijaongezeka uwezo.

**Kielelezo Na. 3: Wastani wa Gharama za kubadilisha fedha za kigeni kwa kipindi cha Septemba hadi Disemba, 2022 na Septemba hadi Disemba, 2023**




**Chanzo: Wizara ya Nishati na Usanifu wa Kamati**

**vi) Utekelezaji wa Mradi wa njia ya kusafirisha umeme kwa ajili ya uendeshaji wa reli ya Kisasa (SGR)**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inatekeleza mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza na Kigoma. Reli hii itatumia nishati ya umeme katika kuendesha treni, hivyo TANESCO kwa kushirikiana na TRC inatekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu ya umeme kwa ajili ya uendeshaji wa treni.
Mradi wa umeme kwa ajili ya SGR unatekelezwa sasa uko katika awamu mbili na unagharimu jumla ya shilingi **Bilioni 173.73**. Awamu ya kwanza inaanzia Kinyerezi Dar es Salaam hadi Kingolwira Morogoro na unahusu upanuzi wa kituo cha Umeme na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 220 yenye urefu wa **kilomita 160** na mradi huu umekamilika.

**Mheshimiwa Spika,** awamu ya pili inahusu ujenzi wa miundiombinu ya kusafirisha na kupoza umeme kuanzia Msamvu

Morogoro hadi Kintinku Singida. Awamu hii imegawanyika katika sehemu mbili (sehemu ya kwanza Lot 2-1 Msamvu Morogoro hadi Ihumwa Dodoma na sehemu ya pili Lot 2-2 Ihumwa Dodoma hadi Kintinku Singida) na inahusisha ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha umeme msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilomita 416. Hadi kufikia Novemba, 2023, sehemu ya kwanza ilikuwa imefikia **asilimia 98.09** na sehemu ya pili ilikuwa imefikia **asilimia 99**.

**vii) Utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa vituo vya gesi iliyoshindiliwa (*CNG*) katika kuendesha mitambo na magari**

**Mheshimiwa Spika,** gesi inayozalishwa songosongo na Mnazi bay hutumika kuzalisha umeme (80%) na asilimia ishirini (20) hutumika kwa ajili ya viwanda, matumizi ya nyumbani na kuendeshea magari. Hadi kufikia mwezi Januari, 2024 kulikuwa na jumla ya vituo vitano (5) kwa ajili ya kujaza gesi asilia kwenye magari. Kati ya vituo hivyo, vitatu (3) vimejengwa Dar es Salaam, kimoja Pwani na kimoja (1) Mtwara ambacho kinahudumia magari ya kampuni ya saruji ya Dangote. Aidha, hadi Januari, 2024 jumla ya **magari 2,970** yalikuwa yamefungwa mfumo wa gesi na yanautumia.

**Mheshimiwa Spika**, matumizi ya gesi katika kuendeshea magari ni nafuu ikilinganishwa na matumizi ya mafuta. Hata hivyo, takwimu zinaonesha kuwa idadi ya magari yaliyofungwa mfumo wa gesi nchini ni ndogo. Hali hii imesababishwa na mambo yafuatayo: -

(a) Uchache wa vituo vya kujazia gesi (vituo vinne, ambapo Dar es Salaam vipo vitatu ((3)) na Pwani kimoja ((1));

(b) Gharama za kufunga mfumo wa gesi kuwa juu (wastani wa **shilingi 2,000,000** kwa gari); na

(c) Uchache wa watalaam hususani wakaguzi wa mifumo hiyo (wapo wakaguzi kumi (10) waliosajiliwa na TBS).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaona kuna haja kwa Serikali kuongeza jitihada za kujenga vituo vya kutosha na kuongeza mtandao wa gesi nchini hususani maeneo ya kimkakati vikiwemo vituo vya GPSA, ili kuwezesha upatikanaji wa gesi hiyo kwa wingi na kwa urahisi.

### viii) Uchambuzi wa Mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu (IRENA) wa Mwaka 2009

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua mkataba husika (IRENA) kwa kuwianisha jukumu la msingi ambalo ni kuendeleza, kuhamasisha na kuongeza matumizi ya aina zote za nishati jadidifu[7] dhidi ya malengo ya ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020-2025), malengo ya Wizara ya Nishati, sera ya taifa ya nishati ya Mwaka 2015 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka mitano (2021/22-2025/26).
Uchambuzi ulibaini kuwa mambo hayo yote yanashabihiana na Mkataba wa IRENA kwani yanalenga kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya nishati jadidifu (renewable energy). Kwa kuzingatia faida hizi ambazo nchi yetu itazipata, Bunge lako tukufu lilikubali kuridhia mkataba huo.

### i) Ziara ya Mafunzo katika Sekta ya Nishati

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara za mafunzo ndani na nje ya nchi. Ziara za ndani zilifanyika katika Mikoa ya Dodoma, Tabora, Tanga, Morogoro na Dar Es Salaam na ya nje ilifanyika New Delhi nchini India. Lengo la ziara za ndani ya nchi ilikuwa kujifunza na kukagua utekelezaji wa miradi chini ya Wizara ya Nishati, ilhali ziara nje ya nchi ililenga kupata uzoefu ambao nchi ya India imeupata katika sekta ya gesi na mafuta. Maelezo kuhusu ziara hizo ni kama ifuatavyo: -

### a. Bwawa la kufua umeme Mtera-Dodoma

**Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa bwawa hili ulianza mwaka 1970 na kukamilika mwaka 1988 ambapo imefungwa mitambo miwili yenye uwezo wa kuzalisha umeme **MW 80**.
Ziara ya Kamati iliyofanyika mwezi Septemba, 2023 ilishuhudia upungufu wa maji kwenye bwawa hili uliosababisha mitambo kufanya kazi chini ya uwezo wake kwa kufua umeme wa **MW 70** tofauti na uwezo wake wa **MW 80**. Aidha, upungufu wa maji katika bwawa hili ulichangia upungufu wa maji kwenye bwawa la Kidatu kwani bwawa la mtera lilijengwa mahsusi kwa ajili ya

[7] Ibara ya II ya Mkataba wa IRENA

kuhifadhi maji ya kuendeshea mitambo ya kufua umeme katika bwawa la Kidatu mkoani Morogoro.

**b. Bwawa la Kufua umeme Kihansi-Morogoro**

**Mheshimiwa Spika,** bwawa hili lilianza kujengwa mwaka 1994 na kukamilika mwaka 2000 kwa kufungwa mitambo mitatu yenye uwezo wa kuzalisha umeme wa **MW 180.** Kamati ilielezwa kuwa kutokana na uhaba wa maji katika bwawa, mtambo mmoja ulikuwa umezimwa na hivyo kuathiri uzalishaji wa umeme kwani hadi mwezi Septemba, 2023 uzalishaji ulikuwa **MW 120**.

**c. Bwawa la kufua umeme Kidatu-Morogoro**

**Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa bwawa la kidatu uliofanyika kwa awamu tatu ulianza mwaka 1970 na kukamilika mwaka 1988 na ilifungwa mitambo yenye uwezo wa kuzalisha umeme wa **MW 204**. Wakati kamati inafanya ziara mwezi Septemba, 2023, mitambo ya bwawa hili ilikuwa inazalisha umeme wa **MW 175**. Aidha, upungufu huo wa uzalishaji wa umeme ulisababishwa na ukame pamoja na kupungua kwa maji katika bwawa la mtera Dodoma ambalo ni chanzo kikuu cha maji yanayoingia katika bwawa la kidatu.

**Mheshimiwa Spika,** katika vituo vyote vya mtera, Kihansi na kidatu mitambo yote ilizalisha umeme pungufu ya uwezo wake. Upungufu wa maji ambao kwa sehemu kubwa umeathiri uzalishaji wa umeme katika vituo hivyo umesababishwa na uhaba wa mvua kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, uharibufu wa mazingira na shughuli za kibinadamu katika vyanzo vya maji yanayoingia kwenye mabwawa katika vituo hivyo. Kamati ilielezwa kwamba miongoni mwa hatua zinazochukuliwa na Serikali ili kunusuru mazingira kwenye vyanzo vya maji yanayokwenda kwenye mabwawa ni pamoja na TANESCO kutenga shilingi **Bilioni 5** kila mwaka ili kuwezesha jamii kupitia taasisi za serikali na zisizo za serikali (CSR) kuboresha mazingira hayo.

**Mheshimiwa Spika,** mbali na uhaba wa maji kwenye mabwawa ya kuzalisha umeme, Kamati ilielezwa Kwamba uchakavu wa mitambo ya kuzalisha umeme unachangia kushuka kwa uzalishaji

wa umeme katika vituo vyote. Kamati ilielezwa kwamba mitambo hiyo inahitaji ukarabati wa kawaida haraka iwezekanavyo na tayari Serikali imeshaini mikataba ya matengenezo kwa baadhi ya mitambo.

**d. Kiwanda cha kuweka mfumo joto kwenye mabomba ya kusafirishia mafuta kutoka Hoima Uganda hadi Chongoleani Tanga**

**Mheshimiwa Spika,** mafuta yatakayosafisrishwa kupitia bomba la mafuta (EACOP) kutoka Uganda hadi Tanzania yapo katika hali ya kimiminika kigumu kisichoweza kusafirishwa kwa njia ya bomba la kawaida. Ili mafuta yaweze kuwa katika hali ya kimimimika laini na hivyo kusafirishwa kwa urahisi ni lazima yapashwe joto, hivyo kimeanzishwa kiwanda kwa ajili ya kutengeneza na kuweka mfumojoto (*thermal installation system-TIS*) kwenye mabomba yatakayotumika kusafirishia mafuta hayo. Kamati ilielezwa kuwa mradi huu ambao ni wa kwanza barani Afrika hadi mwezi Septemba, 2023 utekelezaji ulikuwa umefikia asilimia tisini na tano (95%) na ulitarajiwa kukamilika Disemba, 2023.

**e. Ziara katika miradi ya gesi na mafuta nchini India**

**Mheshimiwa Spika,** mwezi Novemba, 2023, Kamati ilifanya ziara ya mafunzo ya siku tano kwenye sekta ya gesi na mafuta nchini India. Kamati ilipata mafunzo kutoka kampuni kubwa za gesi na mafuta ambazo kwa sehemu kubwa zinamilikiwa na Serikali ya India. Baadhi ya miradi iliyotembelewa na Kamati ni ifuatavyo: -

i) *Kituo cha Kampuni ya Mafuta India (IOCL-LPG) cha kutengeneza, kujaza na kusambaza gesi kwa ajili ya kupikia na matumizi mengine ya kibiashara pamoja na kituo chake cha utafiti na maendeleo kilichopo Trikikalan na Faridabad;*

ii) *Kituo cha Kampuni ya Bharat (BPCL) kinachohusika na kutafiti, kuzalisha na kuuza gesi na bidhaa za mafuta pamoja na kituo cha utafiti na maendeleo kilichopo Noida, New Delhi;*

iii) *Kituo cha kuzalisha na kusambaza gesi inayotokana na tungamotaka (Compressed Bio Gas-CBG) kilichopo Faridabad-New Delhi; na*

iv) *Kituo cha kuchakata gesi asilia kwa ajili ya kutengeneza umeme, bidhaa za petroli na kusafisha mafuta (Panipat Refinery Plant Complex-PRPC)*

**Mheshimiwa Spika,** kwa sehemu kubwa kampuni na vituo hivyo vinamilikiwa na Serikali na vinazalisha na kusambaza mitungi ya gesi ya kupikia kwa takribani kila familia. Mitungi ya gesi **milioni 5.5** husambazwa kwa siku, wastani wa mitungi **bilioni 2** kwa mwaka.

Mitungi yote ya gesi hutengenezwa nchini india, na asilimia 80 ya gesi huagizwa kutoka nje na asilimia 20 pekee ndiyo huzalishwa nchini. Vipo vituo vya kujaza gesi kwenye magari takribani **milioni 5** kwa siku, na lengo ni kufikia magari **milioni 16** ifikapo mwaka 2030.

**Mheshimiwa Spika,** mafanikio katika sekta ya gesi na mafuta nchini India yamechangiwa na mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na: -

1. Kuwa na vituo vya utafiti na uendelezaji *(research and development)* na kutekeleza kikamilifu matokeo ya tafiti ya vituo hivyo;

2. Kuwa na kampuni zinazojitegemea katika masoko, usambazaji gesi (City Gas Distributor-CGD) na uzalishaji na ujazaji wa gesi kwenye mitungi jambo lililowezesha ufanisi wa kila idara;

3. Kuweka mfumo wa kidigitali na kanzidata ya wateja wote ambapo kila mteja anasajiliwa ili kuweza kumfikia na kujua historia ya matumizi ya gesi;

4. Uwepo wa ruzuku ya Serikali kwa kaya zisizojiweza kumudu gharama za kununua gesi ambapo pesa ya kununulia gesi huingizwa moja kwa moja kwenye akaunti ya mteja baada ya kampuni ya kusambaza gesi (CGD) kumfikishia gesi; na

5. Kuweka bei sawa ya gesi kwa watu wote ambao hawaguswi na ruzuku ya serikali.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ziara hiyo yapo masuala kadhaa ambayo Kamati imejifunza ambayo ni pamoja na: -

(i) Umuhimu wa Serikali kuwa mmiliki mkuu wa biashara ya mafuta na gesi na kutumia watalaam wabobevu katika sekta ya mafuta na gesi, biashara, teknolojia na uwekezaji;

(ii) Ili Serikali iweze kupiga hatua katika sekta ya mafuta na gesi, ni vyema taasisi zake kuwa na vitengo vinavyojitegemea kwenye utafiti na maendeleo vikiwa na vifaa vya kisasa na watalaam wabobevu katika sekta ya gesi, mafuta na uwekezaji;

(iii) Ili kufikia azma ya nchi kwenye matumizi ya nishati ya gesi katika kupikia na kuachana kabisa na matumizi ya nishati nyingine, ni vyema serikali ikaandaa na kutekeleza mkakati kabambe wa kaya, wafanyabiashara na taasisi zinazotoa huduma ya chakula kutumia gesi katika kupikia.

(iv) Ni vyema nchi ikaweka jitihada katika teknolojia na uwekezaji kwenye miradi ya nishati jadidifu hususani miradi isiyotumia gharama kubwa katika kuwekeza.

(v) Ili kuwa na nishati toshelezi nchini inayokidhi mahitaji ya sasa na ya miaka mingi ijayo, ni vyema Serikali ikawekeza katika miradi mingi mbalimbali itakayochangia upatikanaji wa nishati na

(vi) Ipo haja ya nchi kusomesha watalaam katika vyuo vya nchi zilizoendelea katika sekta ya nishati na gesi na kuwatumia katika miradi ya gesi na mafuta.

**a) Wizara ya Madini**

**Mheshimiwa Spika,** kupitia Wizara ya Madini, Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili taarifa za utendaji kama ifuatavyo: -

**i) Hali ya uendeshaji wa Migodi nchini ambayo Serikali ina Hisa na Fidia kwa Wanachi wanaopisha Miradi hiyo**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kutekeleza Sheria ya Madini Sura 123 inayotoa nafasi kwa Serikali kushiriki katika miradi ya uchimbaji madini kwa miradi yenye leseni za uchimbaji wa Kati na uchimbaji Mkubwa. Sheria hii imeweka masharti kwa Serikali kumiliki hisa huru (*non-dilutable free carried interest*) zisizopungua asilimia 16[8]. Aidha, matakwa ya sheria hii ni mojawapo ya utekelezaji wa Sheria zilizolenga nchi kuwa na umiliki kwenye rasilimali asilia pamoja na kuhuisha mikataba yenye masharti hasi katika maeneo yanayohusu rasilimali asilia za nchi[9].

**Mheshimiwa Spika,** kwa sasa Serikali inahisa kwenye kampuni tano (05) ambapo kampuni nne (4) zinahusika na miradi mikubwa ya migodi ya madini na kampuni moja (1) inahusika na mradi wa mgodi saizi ya kati. Aidha, kutokana na hisa hizo, serikali inawajumbe wawili (2) kati ya wajumbe watano (5) wa Bodi kwenye kila kampuni. Hadi kufikia mwezi Agosti, 2023 watanzania **3,110** walikuwa wameajiriwa kwenye miradi hiyo sambamba na serikali kuendelea kukusanya mapato ya kodi na tozo za aina mbalimbali. Taarifa kuhusu kampuni hizo ni kama zilivyoainishwa katika Kielelezo **Namba nne (4)** cha taarifa hii.

**Kielelezo Na. 4:**
**Mchango wa Kampuni ambazo Serikali ina hisa hadi kufikia Agosti, 2023**

| Na. | **Jina la Kampuni** | **Kampuni iliyoingiwa Ubia na Serikali** | **Hisa za Serikali (%)** | **Mapato ya Serikali TZS** | **CSR (TZS)** | **Manunuzi (TZS)** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Twiga Minerals Corporation Limited | Barrick Gold Corporation | 16 | 1,456,432,002.398.08 | 18,371,303,299.42 | 2,117,769,398,400 |

8 Kifungu cha 10 cha Sheria ya Madini, Sura ya 123
9 Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi Katika Mikataba ya Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 450 pamoja na Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusu Umiliki wa Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 449.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2. | Tembo Nickel Corporation Limited (TNCL) | LZ Nickel | 16 | 6,646,028,668.91 | 252,105,980.00 | 19,063,803,816 |
| 3. | Williamson Diamond Limited (WDL) | Kampuni ya Petra Diamonds Limited | 37 | 66,815,164,819.99 | 207,815,550.00 | 739,597,455,648 |
| 4. | Sotta Mining Corporation Limited | Nyanzaga Mining Company Limited | 16 | 552,589,020.00 | 24,466,368 | 7,794,712,800 |
| 5. | Faru Graphite Corporation Limited (FGCL) | Mahenge Resources Limited | 16 | 1,393,536,478.05 | 47,980,800 | 1,393,536,478.05 |
| 6. | Mamba Minerals Corporation Limited (MMCL) | Ngualla Group, UK Limited | 16 | 224,766,300.60 | 2,166,341,300 | 26,868,180,000 |
| | **Jumla Kuu (TZS)** | | | **1,532,064,087,585** | **21,045,546,929** | **2,893,423,283,326** |

**Chanzo: Wizara ya Madini na usanifu wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa kamati umebaini kuwa mchango unaotokana na ununuzi wa bidhaa na huduma hapa nchini kwa kampuni ambazo serikali inahisa bado uko chini. **Ni rai ya Kamati kuwa serikali iongeze usimamizi katika eneo hili katika kuhakikisha makampuni hayo yananunua bidhaa zinazopatikana maeneo yanayozunguka mradi au maeneo mengine hapa nchini.**

Aidha, kamati imebaini kuwa Serikali imekuwa ikilazimika kuunda kampuni mpya pale inapohitajika kuwa mbia kwenye kampuni ya uwekezaji katika sekta ya madini jambo linaloweza kuchelewesha mchakato wa uwekezaji na pia kuzalisha kampuni nyingi zenye majukumu yanayofanana. Ni mtazamo wa **Kamati kwamba kuna haja ya Serikali kuitumia kampuni ya STAMICO katika umiliki wa**

**hisa kwenye baadhi ya migodi kwani kampuni hiyo ina watalaam na inaruhusiwa kuwekeza kwenye sekta ya madini.**

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu fidia, katika miradi mitano ambayo serikali inahisa wananchi walipisha maeneo yao ili kuruhusu uwekezaji. Taarifa zilizowasilishwa kwenye kamati zinaonesha kwamba katika miradi hiyo hakuna mradi ambao wananchi wamelipwa fidia kwa asilimia miamoja (100%). **Ni mtazamo wa kamati kuwa serikali isimamie kikamilifu suala la fidia na kuhakikisha wananchi wanalipwa kwa wakati ili kuondoa malalamiko dhidi ya serikali na kuwakwamua dhidi ya athari za kiuchumi, kisaikolojia na kijamii**.

**ii) Uendelezaji wa leseni za Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)**

**Mheshimiwa Spika,** hadi Agosti, 2023 Shirika lilikuwa linamiliki jumla ya leseni za **madini 167** katika maeneo mbalimbali nchini. Kati ya hizo, **leseni 143** hazijafanyiwa utafiti na **24** ndizo zenye utafiti. Aidha, Shirika linaendeleza miradi mitano (5) ya uchimbaji wa madini kwenye leseni zenye utafiti. Miradi hiyo ni uchimbaji wa makaa ya mawe Kabulo-Kiwira, uchakataji wa kokoto Chigongwe, Dodoma, uchimbaji wa dhahabu Biharamulo, Buhemba-Butiama na Buckreef, Geita.

Hadi kufikia Juni, 2023 jumla ya **shilingi 3,234,173,410.00** zilikusanywa katika miradi hiyo kutokana na kodi na tozo mbalimbali. Pia Shirika kwa kushirikiana na TANESCO linaendelea na majadiliano na wawekezaji ili kuzalisha umeme wa **MW 200** katika Mradi wa Makaa ya Mawe Kiwira-Mbeya.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa kamati umebaini kuwa kutokufanyika kwa utafiti katika maeneo mengi yenye leseni kunazuia maeneo hayo kupata wawekezaji. **Ni rai ya kamati kuwa maeneo ambayo shirika lina leseni, yafanyiwe utafiti wa kijiolojia haraka iwezekanavyo na taarifa zake zifahamike ili kuvutia wawekezaji.**

### iii) Usimamizi wa Madini ya Tanzanite na Mkakati wa kuuza Madini hayo nje ya eneo la Mirerani.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Tume ya Madini imeendelea kutekeleza jukumu la kusimamia shughuli zinazohusiana na madini nchini ikiwemo uuzaji wa madini ya Tanzanite, Mirerani. Tume ilianzisha ofisi ya Madini Mirerani ambayo inasimamia eneo tengefu la Mirerani na Wilaya ya Simanjiro. Katika kuhakikisha kunakuwa na udhibiti wa biashara ya madini ya Tanzanite, mwaka 2021, Serikali iliamua shughuli zote za ununuzi na uongezaji thamani madini ya Tanzanite zifanyikie Mirerani.

Uamuzi huu wa Serikali umeonekana kutoleta matokeo yaliyotarajiwa kutokana na kuathiri soko la madini hayo nchini. Ili kukabili changamoto hiyo, Serikali inampango wa kuruhusu biashara ya madini ya Tanzanite yaliyosanifiwa (kukatwa na kung`arishwa) ifanyike pia kwenye maeneo mengine ya kimkakati ili kuiwezesha nchi kunufaika na rasilimali hiyo. Miongoni mwah atua za serikali katika mpango huo ni kurejesha maonesho ya Kimataifa ya vito na usonara ya Arusha na kuanzisha maonesho na minada ya kimataifa ya madini nchini.

### iv) Utendaji wa kituo cha Jeomolojia (TGC)

**Mheshimiwa Spika,** kituo hiki kilianzishwa mwaka 2009 kwa lengo la kuboresha manufaa yatokanayo na rasilimali madini pamoja na kuhamasisha uongezaji thamani wa madini nchini. Kwa sasa kituo kinatoa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu katika fani za vito na teknolojia ya usonara ngazi ya astashahada na stashahada. Kituo pia kinazalisha bidhaa zitokanazo na rasilimali madini pamoja na kutoa huduma za utambuzi wa madini ya vito na bidhaa zake, tafiti za madini ya vito na huduma za ushauri kwenye madini ya vito na usonara.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya majukumu ya kituo kuonekana kuwa ya msingi, uchambuzi wa kamati ulibaini kuwa bado kituo hakifahamiki vya kutosha kwa watanzania na hivyo kuwakosesha huduma zitolewazo na kituo ikiwa ni pamoja na kuathiri idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa katika mafunzo yatolewayo na kituo. Kamati ilielezwa sababu zinazochangia hali hii kuwa ni pamoja na

kukosekana kwa hati ya uanzishaji wa kituo, ufinyu wa miundombinu ikiwemo mabweni, uchache wa watumishi na ufinyu wa bajeti.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba changamoto hizi zimekuwa zikijirudia kila mwaka hivyo **inaishauri Serikali itatue changamoto hizo ili kukiwezesha kituo kutekeleza majukumu yake kikamilifu.**

**v) Utendaji kazi wa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST)**

**Mheshimiwa Spika,** majukumu ya msingi ya taasisi hii ni pamoja na kufanya tafiti za jiosayansi, kutoa huduma za kimaabara katika jiosayansi, kuratibu na kushauri juu ya majanga ya asili ya jiolojia ikiwemo volkano na maporomoko ya ardhi, kutoa ushauri wa kijiosayansi na kukusanya na kutunza takwimu na taarifa za jiosayansi. GST inatekeleza majukumu hayo kupitia maabara tatu (3) ambapo mbili (2) zipo Dodoma na moja (1) Geita.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023 bajeti ya **shilingi 2,400,000,000.00** iliyotengwa kwa ajili ya taasisi hii iliiwezesha kununua vifaa mbalimbali vya kimaabara ambavyo vimesaidia kupunguza malalamiko ya wateja kutokana na utambuzi wa madini ya vito na kuongezeka idadi ya sampuli kwenye maabara kutoka **17,000** hadi kufikia **22,232**.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya jitihada hizi, bado GST iinakabiiliwa na changamoto mbalimbali zinazoathiri utendaji kazi wake zikiwemo:-

(a) Ufinyu wa bajeti kwa ajili ya kufanya utafiti wa jiokemia na jiofizikia (kwa njia ya kurusha ndege). Hadi oktoba, 2023 utafiti wa kina wa jiofizikia kwa njia ya kurusha ndege ulikuwa umefanyika kwa **asilimia 16**;

(b) Upungufu wa Vitendea kazi vya kimaabara hususani vya jiofizikia unaoathiri utambuzi wa aina za miamba na sifa zake;

(c) Uchakavu wa miundombinu ya kimaabara; na

(d) Upungufu wa watumishi unaokwamisha GST kuanzisha ofisi za kanda.

**vi) Marekebisho ya Sheria na kanuni katika sekta ya Madini**

**Mheshimiwa Spika,** katika majadiliano ya kikazi baina ya kamati na Serikali, ilibainika kuwa baadhi ya changamoto zinazoikabili sekta ya madini utatuzi wake unahusu kutungwa kwa sheria mpya na zilizopo kufanyiwa marekebisho. Miongoni mwa sheria inayopaswa kutungwa ni sheria kuhusu usimamizi wa matumizi ya baruti kwani iliyopo ni ya Mwaka 1963 na haikidhi mahitaji ya sasa. Aidha, marekebisho ya sheria yanayohitajika ni kuweka masharti kuhusu uwezekano wa biashara ya makinikia kufanyika nchini, kuitambua maabara ya Tume ya Madini, kuruhusu uendeshaji wa minada ya madini ya kimataifa na kuruhusu biashara ya madini ya Tanzanite kufanyika nje ya eneo la mererani. **Ni rai ya kamati kwamba serikali iharakishe mchakato wa kuwasilisha Bungeni miswada ya kuwezesha kutungwa na kurekebisha Sheria husika. Aidha, serikali ifanye marekebisho kwenye kanuni zilizopo ili kutatua changamoto zinazokwamisha ustawi wa sekta ya madini nchini.**

**vii) Utendaji kazi wa Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI)**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/2024 TEITI imeendelea kutekeleza vipaumbele vyake sita ilivyojiwekea ikiwemo kutoa ripoti ya 14 kuhusu uwazi katika sekta ya madini, mafuta na gesiasilia nchini, kujenga mfumo wa kielektroniki utakaotumiwa na kampuni za uziduaji pamoja na taasisi za Serikali kuripoti malipo yanayofanywa na kampuni za madini, mafuta na gesi asilia na kufanya tafiti mbalimbali kuhusu uwazi wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia.

**Mheshimiwa Spika,** TEITI imefanikiwa kutekeleza majukumu yake mbalimbali ikiwemo kuelemisha umma kuhusu matumizi ya takwimu zinazotokana na ripoti za TEITI, Kutoa ripoti kumi na tatu (13) kwa kipindi cha Julai, 2008 hadi Juni, 2021 na kuelimisha watumishi wa halmashauri namna ya kuhakiki malipo yanayotokana na shughuli za rasilimali asilia.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo, taaisisi hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo bajeti ndogo, ukosefu wa vitendea kazi, uchache wa watumishi pamoja na watumishi viongozi akiwemo mtendaji mkuu kukaimu kwa muda mrefu nafasi zao, baadhi yao takribani miaka sita (6).

**viii) Utafiti na Uendelezaji wa leseni za madini kwenye maeneo ya Hifadhi**

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Madini imeendelea kutoa leseni kwenye baadhi ya maeneo ya hifadhi za wanyama ikiwemo hifadhi ya Burigi chato, Swagaswaga, Mwalimu nyerere na Saadani ambapo hadi oktoba, 2023 jumla ya **leseni 44** zilikuwa zimetolewa ikiwemo leseni **mbili (2)** kwa ajili ya uchimbaji mkubwa na arobaini (40) za utafutaji wa madini. Kwenye hifadhi za misitu, jumla ya **leseni 293** za uchimbaji mdogo zilitolewa Chunya, Songwe, Geita, Katavi, Tabora na Mbogwe. Katika kutoa leseni hizi, Wizara hulazimika kuzingatia sheria nyingine zinazohusu hifadhi za Wanyamapori, hifadhi za Taifa na hifadhi za misitu.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa utoaji wa leseni katika hifadhi za taifa, mapori tengefu na mapori ya akiba upo chini ikilinganishwa na utoaji wa leseni kwenye hifadhi za misitu. Ili kutekeleza ahadi za viongozi wa kitaifa kuhusu uchimbaji wa madini kwenye maeneo ya hifadhi, **ni mtazamo wa kamati kuwa mamlaka zote zinazohusika na usimamizi wa maeneo hayo zishirikiane katika utendaji ili kuwezesha utekelezaji wa lengo hili.**

**ix) Ziara na Semina za Mafunzo katika Sekta ya Madini**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara za mafunzo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Kagera, Dodoma na Lindi pamoja na semina mbalimbali kwa lengo la kujionea na kujifunza utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Wizara ya Madini kama ifuatavyo: -

**(a) Wajibu wa Wamiliki wa Leseni za Madini kwa Jamii (CSR)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata mafunzo kuhusu wajibu wa wamiliki wa leseni za miradi ya madini ikiwemo inayomilikiwa na

STAMICO. Ili kutatua changamoto zinazohusu CSR, serikali ilitunga Kanuni za Wajibu wa Wamiliki wa Leseni za Madini kwa jamii za Mwaka 2023[10]. Kanuni hizo zimeainisha mambo mbalimbali ikiwemo mmiliki wa leseni kuwajibika kuishirikisha halmashauri ya kijiji au mtaa unaoguswa na mradi katika kuainisha vipaumbele vya jamii wakati wa zoezi la kuandaa mpango wa wajibu wake kwa jamii. Aidha, kazi zote zinazohusu usimamizi wa wajibu wa mmiliki wa leseni ikiwemo kuhakikisha miradi inayotekelezwa na wamiliki wa leseni inazingatia thamani ya fedha[11]. Aidha kazi zote zitakuwa chini ya Kamati ya Watalaam ambayo inaundwa na wajumbe wafuatao kutoka katika halmashauri husika:
(1) Mkurugenzi Mtendaji-Mwenyekiti;
(2) Afisa Mipango-Katibu;
(3) Afisa wa Tume ya Madini wa eneo husika;
(4) Wawakilishi wawili wa mmiliki wa leseni ya madini;
(5) mhandisi;
(6) Wakili wa Serikali;
(7) Afisa Mazingira;
(8) Afisa Maendeleo; na
(9) afisa kutoka eneo mahsusi la utekelezaji wa mradi.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kamati ya watalaam imepewa majukumu mazito katika kuhakikisha jamii inanufaika na uwepo wa miradi inayohusu madini katika maeneo husika. **Hata hivyo, kamati inamashaka endapo muundo wa kamati hiyo unaweza kuleta tija katika utendaji kazi wake sambamba na kulinda kikamilifu maslahi ya jamii husika kutokana na ukweli kwamba haina uwakilishi wa wananchi kutoka maeneo yanayozunguka utekelezaji wa mradi.**

**(b) Ziara katika mradi wa madini ya Nikeli, Kabanga-Ngara**

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilishiriki uzinduzi wa kulipwa fidia ya jumla ya **shilingi Bilioni 33.08** kwa wananchi **1,341** waliopisha mradi wa uchimbaji madini ya Nikeli na madini mengine ambata pamoja na ujenzi wa kiwanda cha kusafisha madini unaotekelezwa na Kampuni ya Tembo Nickel. Mradi umeanza kazi za awali na baadhi ya wananchi wamehama kupisha

---

[10] Tangazo La Serikali Na. 409 la tarehe 23 Juni, 2023
[11] Kanuni ya 7(b) ya Kanuni za CSR za Mwaka 2023.

utekelezaji wa mradi. **Kamati inaisisitiza serikali kuhakikisha inasimamia kikamilifu ulipwaji wa fidia kwa wananchi ili kuondoa uwezekano wa kutokea sintofahamu ambazo huzalisha migogoro baina ya mwekezaji na wananchi lakini pia chuki kutoka kwa wananchi dhidi ya serikali kwa hisia kwamba imeshindwa kuwatetea.**

**(c) Mkutano wa Kimataifa wa Madini na Uwekezaji Tanzania wa Mwaka 2023**

**Mheshimiwa Spika,** mkutano huu uliwakutanisha wadau na wawekezaji wa madini kutoka nchi mbalimbali duniani na Serikali ilipata fursa ya kueleza na kuonesha rasilimali madini zilizopo nchini. Kupitia mkutano huo, Kamati ilibaini kuwa nchi yetu ina fursa nyingi katika sekta ya madini ikiwa ni pamoja na madini ya chini ya sakafu ya bahari kama vile *silicon manganese* ambayo nchi haijawa na uwezo wa kuyachimba. **Ni rai ya kamati kuwa Serikali iendelee kuandaa mikutano ya kimataifa na kutumia kikamilifu kutangaza fursa za biashara ya madini mbalimbali yanayopatikana nchini**.

**(d) Mradi wa Kokoto Chigongwe, Dodoma**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unamilikiwa na shirika la STAMICO ambapo upo katika hatua ya kufunga mtambo wenye thamani ya shilingi **1,137,168,331** wenye uwezo wa kuzalisha **tani 2000** za kokoto kwa siku. Lengo la mradi ni kuhudumia miradi mikubwa ya serikali ikiwemo ujenzi wa majengo, viwanja vya ndege na barabara. Kamati ilifahamishwa kuwa mawe yanayotegemewa kuzalisha kokoto yameshafanyiwa vipimo vya kimaabara na yameonekana yanafaa kuzalisha bidhaa bora. Aidha, mawe yaliyopo kwenye eneo hilo yanafikia tani **milioni 13.3** kiasi ambacho kinawezesha mradi kudumu kwa muda wa **miaka 33**.

**Mheshimiwa Spika,** mradi unatekelezwa na shirika moja kwa moja kwa mfumo wa *force account* na ulipangwa kukamilika mwezi Januari, 2024. Ukaguzi wa kamati umebaini kuwa utekelezaji wa mradi upo nyuma ya muda kwa kuwa utekelezaji wake hadi januari, 2024 ulikuwa umefikia **asilimia 70** tu. **Aidha, kamati ilishauri serikali kufikiria kuzalisha bidhaa nyingi zaidi ikiwemo *tiles, marble* na tofali za *paving* kwa kutumia mawe**

**yanayopatikana katika eneo hilo. Katika kuhakikisha mradi unakuwa na tija zaidi, kamati ilishauri ubora wa bidhaa uzingatiwe ili kukidhi matakwa ya wateja**.

## 2.2 Yaliyobainika wakati wa ufuatiliaji wa Sekta za Nishati na Madini

**Mheshimiwa Spika,** ufuatiliaji uliofanywa na Kamati kwa Wizara inazozisimamia kwa mujibu wa Kanuni[12] umeiwezesha Kamati kubaini changamoto mbalimbali ambazo kwa kiasi kikubwa zinachangia kukwamisha lengo la nchi katika kuhakikisha ustawi wa wananchi[13]. Katika ufuatiliaji huo, Kamati imebaini masuala yafuatayo: -

**2.2.1** Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Nishati uko chini ya wastani ambao ni asilimia 50. Hadi kufikia Disemba, 2023 upatikanaji wa fedha za Wizara ulikuwa umefikia asilimia 43 tu;

**2.2.2** Ukusanyaji hafifu (wastani wa asilimia 32.08) wa maduhuli kwa Wizara zote mbili ikilinganishwa na lengo tarajiwa katika kipindi hicho. Hadi kufikia Disemba, 2023 Wizara ya Nishati ilikusanya asilimia 24.11 na Wizara ya Madini ilikusanya asilimia 40.05;

**2.2.3** Idadi ya watumishi katika baadhi ya taasisi chini ya Wizara zote mbili iko chini ikilinganishwa na mahitaji;

**2.2.4** Hali ya upatikanaji wa Umeme nchini bado hairidhishi ikilinganishwa na mahitaji kwa sababu uwezo wa uzalishaji umepungua na hivyo kusababisha mgao wa maeneo mengi nchini;

**2.2.5** Kusuasua kwa utekelezaji wa mpango wa kuzalisha umeme wa makaa ya mawe kupitia mradi wa Kabulo-Kiwira baina ya TANESCO na STAMICO.

**2.2.6** Kusuasuau kwa utekelezaji wa miradi ya kuimarisha gridi ya umeme (Gridi imara) nchini;

---

[12] Kanuni ya 7 (1) (d) ya Nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023

[13] Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977

**2.2.7** Utekelezaji wa Miradi ya REA kwa lengo la kuhakikisha wananchi wote wa vijijini wanapata umeme siyo wa kuridhisha;

**2.2.8** Bei ya mafuta kuendelea kuwa juu kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo uhaba wa fedha za kigeni hususani Dola za Kimarekani, gharama za kubadlisha fedha za kigeni (exchange rate) na uwezo mdogo wa miundombinu ya kushusha mafuta katika bandari ya Dar es Salaam;

**2.2.9** Ukosefu wa Maabara za kupima ubora wa mafuta katika bandari ya Tanga na Mtwara;

**2.2.10** Idadi ndogo ya vituo vya kujaza gesi iliyoshindiliwa kwenye magari (CNG) na hivyo kutokukidhi mahitaji;

**2.2.11** Gharama kubwa za kufunga mfumo wa kutumia gesi kwenye magari (wastani wa shilingi milioni mbili kwa gari);

**2.2.12** Uzalishaji mdogo wa gesi asilia nchini ikilinganishwa na uhitaji kwa ajili ya matumizi mbalimbali;

**2.2.13** Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) kushindwa katika zabuni za kuagiza mafuta na hivyo nchi kutegemea kampuni binafsi katika uagizaji wa mafuta kwa ajili ya matumizi ya nchi na nchi jirani;

**2.2.14** Utekelezaji wa ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020-2025) kuhusu nchi kuwa na nishati jadidifu ya **MW 1,100**[14] inayotokana na upepo, jotoardhi na nishati jua sio ya kuridhisha;

**2.2.15** Hali ya utafiti nchini katika sekta ya madini kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya "High Resolution Geophysical Survey" ili kuboresha taarifa za kijiolojia sio ya kuridhisha;

**2.2.16** Kusuasua kwa wamiliki wa leseni za madini katika utoaji wa huduma kwa jamii (Corporate Social Responsibility-CSR);

**2.2.17** Ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha maeneo yao ili kufanikisha utekelezaji wa miradi ya madini sio wa kuridhisha;

---
[14] Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020, ukurasa wa 104

**2.2.18** Taasisi za Serikali zilizo chini ya Wizara ya Madini hususani GST, STAMICO, TEITI, Tume ya Madini na TGC zinahitaji kuwezeshwa; na

**2.2.19** Uelewa mdogo wa jamii kuhusu wajibu wa TEITI katika sekta ya madini, mafuta na gesi na namna jamii inavyopaswa kunufaika na miradi kutokana na sekta hizo.

## SURA YA TATU

### 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO
### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kazi nzuri zinazofanywa na Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini ambazo Kamati kama msimamizi imezishuhudia katika kipindi cha mwaka mzima wa shughuli za Kamati, bado kuna changamoto mbalimbali zinazozikabili Wizara hizi ambazo zimekuwa kikwazo katika kufikia malengo mbalimbali ya nchi kama zinavyoonekana kwenye Taarifa hii. Kutokana na changamoto hizo, Kamati inatoa mapendekezo yafuatayo: -

### 3.2 Mapendekezo ya Jumla
### 3.2.1 Kusuasua kwa utekelezaji wa Bajeti (ukusanyaji wa maduhuli)

**KWA KUWA** ukusanyaji wa maduhuli kama ilivyoidhinishwa na Bunge katika Wizara zote mbili uko chini ya lengo kwani hadi Disemba, 2023 ukusanyaji ulikuwa wastani wa asilimia 32.08 ya lengo;

**NA KWA KUWA** hali hiyo inachangia kukwamisha Wizara na taasisi zake kutekeleza kikamilifu na kwa wakati shughuli mbalimbali zilizopangwa kutekelezwa katika kipindi hicho na hivyo kuathiri matarajio ya wanachi ya kupata huduma bora kutoka katika Wizara hizo na taasisi zake;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba; Serikali ihakikishe kunakuwa na mikakati madhubuti itakayowezesha ukusanyaji wa maduhuli kutekelezwa kikamilifu ili kutoathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa na Wizara na taasisi zake.

### 3.2.2 Kusuasua kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**KWA KUWA** utekelezaji wa baadhi ya miradi unasuasua ikiwemo mradi wa Kinyerezi I *Extension* **MW 185**, mradi wa kusambaza umeme vijijini (awamu ya tatu mzunguko wa pili), mradi wa kuzalisha mkaa mbadala wa kupikia (Kiwira na Kisarawe) na ujenzi wa ofisi ya Tume ya Madini Dodoma;

**NA KWA KUWA** kusuasua huko kunasababisha ongezeko la gharama za utekelezaji wa miradi hii, kukosesha wananchi huduma iliyotarajiwa kutokana na miradi hiyo na kuathiri utendaji katika taasisi ambazo zinatekeleza miradi hiyo;

**NA KWA KUWA** kusuasua huko kunaendelea kuchochea uharibifu wa mazingira kwani wananchi wanakata miti kwa ajili ya kuni na kuchoma mkaa ambavyo pia vinawaathiri kiafya;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba; Serikali ihakikishe utekelezaji wa miradi unafanyika kikamilifu na kwa wakati na hivyo kuokoa ongezeko la gharama, kuwezesha wananchi kupata huduma tarajiwa kutokana na miradi hiyo na kupunguza uharibifu wa mazingira.

### 3.3 Wizara ya Nishati

### 3.3.1 Utekelezaji wa Bajeti (upatikanaji wa fedha kutoka hazina)

**KWA KUWA,** mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka hazina (hasa za nje) hauridhishi kwani hadi kufikia Disemba, 2023 upatikanaji ulikuwa kwa wastani wa **asilimia 43** (fedha za nje (IMF) kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) hazikupatikana kabisa);

**NA KWAKUWA**, hali hiyo inachangia Wizara na taasisi zake kushindwa kutekeleza kikamilifu majukumu yaliyopangwa na hivyo kuathiri huduma tarajali kwa wananchi kutoka katika wizara na taasisi zake;

**KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;**

(a) Serikali ihakikishe fedha zilizoidhinishwa kwa Wizara ya Nishati na taasisi zake zinapatikana kwa utoshelevu na kwa wakati;

(b) Serikali ijielekeze kutenga fedha kutoka vyanzo vya ndani ili kuepuka adha ya utegemezi wa fedha za nje ambazo mara nyingi hazipatikani kwa uhakika na kwa wakati; na

(c) Serikali iboreshe mfumo wa ufuatiliaji wa fedha za nje zilizotengwa kwenye bajeti.

### 3.3.2 Hali ya Usambazaji na Upatikanaji wa Umeme nchini

**KWA KUWA,** hali ya usambazaji na upatikanaji wa umeme nchini siyo ya kuridhisha kutokana na ukame, uhaba wa gesi, uchakavu wa miundombinu na uchache wa vituo vya kupoza umeme;

**NA KWA KUWA** hali hiyo inaathiri uzalishaji wa bidhaa na huduma nchini na hivyo kuathiri ukuaji wa uchumi na kuchangia ongezeko la mfumuko wa bei;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba;

a) Serikali ihakikishe mradi wa bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere (JNHPP) unakamilika haraka na kuanza uzalishaji kuanzia Februari, 2024 kama ilivyoahidi;

b) Serikali ihakikishe mradi wa kufunga mitambo ya kupoza hewa (chillar) katika kituo cha Kinyerezi *I Extention* ili kuongeza uzalishaji wa umeme kutoka **MW 160** hadi **MW 185** unakamilika ifikapo Disemba, 2024;

c) Serikali kupitia TPDC iongeze uzalishaji wa gesi asilia katika visima vya Songosongo na Mnazi bay (MB2 na MB3) na ili kuongeza uzalishaji wa umeme; na

d) Serikali ihakikishe mitambo ya kuzalisha umeme inafanyiwa ukarabati wa mara kwa mara ili kuepuka uchakavu ambao unaathiri uwezo wa mitambo hiyo.

### 3.3.3 Bei ya Mafuta kuwa juu

**KWA KUWA,** bei ya mafuta imeendelea kuwa juu kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na uhaba wa fedha za kigeni, gharama za kubadlisha fedha za kigeni (exchange rate), ukosefu

wa maabara za kupima ubora wa mafuta katika bandari za Mtwara na Tanga, na ufinyu wa maghala ya kuhifadhia mafuta**;**

**NA KWA KUWA,** hali hiyo inachangia ongezeko la mfumuko wa bei kwenye bidhaa na huduma nchini na hivyo kuchangia ongezeko la gharama za maisha na kuibua hisia za chuki miongoni mwa wananchi dhidi ya Serikali;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba;

(a) Serikali ikamilishe upanuzi wa miundombinu ya Bandari ya Dar es Salaam na ujenzi wa maabara za kupima ubora mafuta katika bandari za Tanga na Mtwara ili kuongeza kasi na uwezo wa upakuaji wa mafuta;

(b) Serikali ichukue hatua madhubuti kuhakikisha nchi inajitosheleza katika akiba ya fedha za kigeni hususani dola za Marekani;

(c) Serikali ichukue hatua ili kuongeza uwezo wa maghala ya kuhifadhia mafuta na hivyo kuiwezesha nchi kuwa na akiba ya kutosha ya mafuta; na

(d) Serikali iiwezeshe TPDC kwa kuijengea mazingira wezeshi kibiashara ili iweze kushindana kwenye soko la ndani na nje ya nchi na hivyo kuihakikishia nchi usalama wa mafuta.

### 3.3.4 Ongezeko la magari yanayotumia gesi asilia (CNG) dhidi ya vituo vya kujaza vilivyopo

**KWA KUWA**, matumizi ya gesi asilia kwenye magari yanaongezeka nchini (kutoka magari takribani 1139 mwaka 2020/2021 hadi kufikia takribani magari 3000 mwaka 2022/2023) kutokana na unafuu wa gesi wa takribani asilimia 40 ikilinganishwa na mafuta hususani katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Mtwara;

**NA KWA KUWA,** ongezeko hilo limesababisha foleni kwenye vituo vitano vya kujaza gesi vilivyopo nchini na hivyo wenye magari kulazimika kutumia muda mwingi katika kujaza gesi;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba; Serikali iongeze idadi na mtandao wa vituo vya kujaza gesi kwenye magari nchini kwa kuanza na maeneo ambayo taratibu za awali za ujenzi zimeanza ambayo ni Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma na vituo vya GPSA.

### 3.3.5 Gharama na uhaba wa wakaguzi wa mfumo wa gesi asilia kwenye magari

**KWA KUWA,** magari mengi yanayoingizwa nchini hayana mfumo wa kutumia gesi asilia hivyo yatalazimika kuwekewa mfumo huo nchini iwapo wamiliki watahitaji;

**NA KWA KUWA**, baadhi ya wamiliki wa magari wanashindwa kuweka mfumo wa kutumia gesi asilia kwenye magari kutokana na gharama kuwa kubwa (shilingi 2,000,000 kwa gari), uchache wa wakaguzi wa mfumo nchini (10) na uchache wa karakana (4);

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba;

a) Serikali ichukue hatua zitakazowezesha kupunguza gharama za kufunga mfumo wa kutumia gesi kwenye magari;

b) Serikali ichukue hatua zitakasaidia kuongeza idadi ya wakaguzi wa mfumo wa magari yanayotumia gesi asilia; na

c) Serikali ianze kuhamasisha uingizaji wa magari nchini yenye mfumo wa kutumia wa gesi asilia ili kupunguza gharama za kuweka mfumo.

## 3.4 Wizara ya Madini

### 3.4.1 Kusuasua kwa fidia kwa wananchi wanaopisha miradi ya uchimbaji wa madini

**KWA KUWA,** kumekuwa na uchelewashaji wa fidia kwa wananchi wanaohama kwenye maeneo yao ili kuruhusu utekelezaji wa miradi ya uchimbaji wa madini;

**NA KWA KUWA**, hali hiyo inachangia kudidimiza wananchi kiuchumi kutokana na kutoruhusiwa kufanya shughuli za

kimaendeleo na kijamii katika maeneo hayo na hivyo kujenga chuki dhidi ya wawekezaji na serikali;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba:

a) Serikali isimamie kikamilifu suala la fidia na kuhakikisha wananchi wanalipwa kwa wakati ili kuondoa malalamiko dhidi ya serikali na kuwakwamua dhidi ya athari za kiuchumi, kisaikolojia na kijamii;

b) Serikali ihakikishe wawekezaji wanaweka fedha katika mfuko wa fidia ya ardhi kabla ya kuwaondoa wananchi katika maeneo yao jambo litakalowahakikishia wananchi hao kulipwa fidia na kwa wakati; na

c) Serikali ihamasishe wananchi kulipwa fidia kwa njia ya kupewa hisa huru katika miradi ya uchimbaji wa madini.

### 3.4.2 Taarifa za Utafiti wa Madini kuwanufaisha wachimbaji wadogo na kuvutia wawekezaji

**KWA KUWA**, sehemu kubwa ya nchi (asilimia 84) halijafanyiwa utafiti wa teknolojia ya kisasa (High Resolution Geophysical Survey);

**NA KWA KUWA,** hali hiyo inasababisha uendelezaji wa leseni za madini kufanyika kwa gharama kubwa bila kuwa na uhakika wa taarifa za madini katika eneo husika jambo linalochangia upotevu wa mitaji na uharibifu wa mazingira kutokana na uchimbaji wa kuhamahama;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Serikali ihakikishe inatekeleza mikakati yake ya kuongeza eneo lililofanyiwa utafiti wa teknolojia ya kisasa (high resolution geophysical survey) kutoka asilimia kumi na sita ya sasa hadi kufikia asilimia hamsini mwaka wa fedha 2024/2025;

### 3.4.3 Uboreshaji wa Sheria na Kanuni katika Sekta ya Madini

**KWA KUWA**, baadhi ya changamoto zinazoikabili sekta ya madini zinachangiwa na udhaifu kwenye baadhi ya sheria na kanuni za sekta ya madini;

**NA KWA KUWA** udhaifu huo unaathiri masuala mbalimbali ikiwemo usimamizi wa baruti, usimamizi wa biashara ya makinikia na uchenjuaji wa madini ghafi, uratibu wa masoko na maonesho ya kimataifa ya madini na biashara ya madini ya Tanzanite;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba; Serikali iharakishe ukamilishaji wa mchakato wa:

a) Kutunga sheria ya usimamizi wa baruti nchini kwani iliyopo ya mwaka 1963 imepitwa na wakati;

b) Kufanya marekebisho ya sheria ya Madini, Sura ya 123 ili kuwezesha usimamizi wa biashara ya makinikia na uchenjuaji wa madini ghafi nchini;

c) Kurekebisha kanuni za eneo Tengefu la Mirerani ili kuruhusu biashara ya madini ya Tanzanite yaliyosanifiwa (kukatwa na kung`arishwa) kufanyika pia maeneo mengine nje ya Mirerani; na

d) Kutengeneza kanuni zitakazotoa mwongozo wa minada na maonesho ya kimataifa ya madini nchini.

### 3.4.4 Usimamizi wa sera, sheria na kanuni kuhusu wajibu wa mmiliki wa leseni za madini kwa jamii (corporate social responsibility-CSR)

**KWA KUWA,** utoaji na upatikanaji wa huduma za kijamii (CSR) unasuasua kutokana na baadhi ya wamiliki wa leseni za uchimbaji wa madini kuchukulia jambo hilo kuwa hisani jambo ambalo ni kinyume na kanuni za wajibu wa wamiliki wa leseni za madini kwa jamii za mwaka 2023;

**NA KWA KUWA,** jambo hilo linachangia jamii zinazozunguka miradi ya uchimbaji madini kutonufaika na huduma za kijamii (CSR)

kutoka kwa mwekezaji pamoja na kusababisha migogoro baina ya wawekezaji na jamii hizo;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba; Serikali ihakikishe inasimamia kikamilifu utekelezaji wa kanuni za wajibu wa wamiliki wa leseni za madini kwa jamii za mwaka 2023 ili wamiliki wa leseni watimize wajibu wao kikamilifu na jamii husika ziweze kunufaika na uwekezaji huo.

## SURA YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuhitimisha hoja ya Kamati kama ifuatavyo: -

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee naendelea kukushukuru na kukupongeza wewe Spika wa Bunge letu Tukufu Mhe. Dkt Tulia Aksoni (Mb) kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu katika utekelezaji wa majukumu yake. Namshukuru Naibu Spika Mhe. Mussa Azzan Zungu, (Mb) pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa namna wanavyokusaidia katika kuendesha vikao vya Bunge letu.

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa kuniamini mimi pamoja na Makamu Mwenyekiti Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda, (Mb) na kuendelea kutupa ushirikiano uliowezesha utekelezaji bora wa majukumu ya Kamati katika kipindi chote. Kwa namna ya kipekee naomba majina yao yatambuliwe na kuingizwa kwenye kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Dkt. David Mathayo David, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda, Mb - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Aleksia Asia Kamguna, Mb
4. Mhe. Tabasamu Hamisi Mwagao, Mb
5. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb

6. Mhe. Constantine John Kanyasu, Mb
7. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb
8. Mhe. Sophia Hezron Mwakagenda, Mb
9. Mhe. Tumaini Bryceson Magessa, Mb
10. Mhe. Angeline Sylvester Lubala Mabula, Mb
11. Mhe. Iddi Kassim Iddi, Mb
12. Mhe. Jesca David Kishoa, Mb
13. Mhe. John Marko Sallu, Mb
14. Mhe. Juliana Didas Masaburi, Mb
15. Mhe. Maimuna Ahmad Pathan, Mb
16. Mhe. Masache Njelu Kasaka, Mb
17. Mhe. Ndaisaba George Ruhoro, Mb
18. Mhe. Nicodemas Henry Maganga, Mb
19. Mhe. Joseph Kasheku Musukuma, Mb
20. Mhe. Saada Mansour Hussein, Mb
21. Mhe. Eng. Samwel Hhayuma Xaday, Mb
22. Mhe. Martha Festo Mariki, Mb

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia kuwashukuru Mhe. Dotto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Antony Peter Mavunde (Mb), Waziri wa Madini, kwa ushirikiano wao mzuri wanaoipatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake. Aidha, namshukuru Mhe. Judith Salvio Kapinga (Mb) Naibu Waziri wa Nishati na Mhe. Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa (Mb) Naibu Waziri wa Madini kwa namna wanavyowasaidia mawaziri wao na hivyo kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Vilevile ninamshukuru Katibu Wakuu wa Wizara ya Nishati Mhandisi Felschesmi Mramba na Naibu wake Ndugu. Athuman Mbuttuka na Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini Ndg. Khery Mahimbali na Naibu wake Ndg, Msafiri Mbibo kwa namna wanavyowaongoza watendaji wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano mzuri wanaiopa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** namshukuru sana Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Joyce Mwihambi (*ndc*) pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza kikamilifu majukumu yake ya Kikatiba. Kipekee namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein (*ndc*), Mkurugenzi Msaidizi wa Idara za Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto (*ndc)*, Makatibu wa Kamati Ndg. Chacha

Nyakega, Ndg. Jesca Sanga na Ndg. Praisegod Lukio pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Rukia Shaban kwa utendaji wao mzuri wa kazi.

**4.2 Hoja**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya shukrani hizo, naliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili Taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

Dkt. David Mathayo David, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**

06 Februari, 2024

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge, kabla ya kuchangia niwaombe, Mheshimiwa Naibu Waziri ndiyo Waziri wa Nishati. Naomba mumpe fursa kwanza pale asikilize michango yenu na kidogo mpunguze kumtembelea tembelea ili aweze kusikiliza na awe na majibu sahihi. Tunaanza na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, ajiandae Mheshimiwa Musukuma na Mheshimiwa Lulida. *(Makofi)*

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma, kwa kutuwezesha kuendelea kulitumikia Bunge letu tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa

anayoendelea kuifanya katika Serikali yake na hasa katika wizara hizi mbili ambazo Kamati inazitolea taarifa; yaani Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini. Kuna kazi kubwa sana imefanyika na ambayo Watanzania wanaendelea kuona na wataendelea kuona matunda yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo, kwa uwasilishaji mzuri wa taarifa na kwa uongozi wake mzuri wa Kamati hii ambayo ni nyeti sana miongoni mwa Kamati za Bunge. Napenda kutumia nafasi hii niliyopewa kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge wenzangu na wapiga kura wake kwamba, tunaye mwenyekiti mahiri sana yanayetuongoza katika Kamati hii. Tangu amechaguliwa kuwa Mwenyekiti, ha-*miss* vikao; anakuwepo kwenye vikao kuendesha vikao vya Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda nijielekeze kuchangia mambo mawili kwenye taarifa hii. Jambo la kwanza ni suala la bei za mafuta, tatizo la mafuta na matumizi ya gesi. Kwa kweli kuna mapinduzi makubwa sana yanayotakiwa kufanyika na ambayo Kamati imeyaona yanafanyika kwenye Wizara zetu hizi mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwanza ambalo nataka nilizungumze ni kwamba, tumekuwa na tatizo kubwa la mafuta. Tatizo liko katika maeneo makubwa matatu. Kwanza, ni upandaji wa bei za mafuta ambao umesababisha mfumko wa bei za bidhaa na huduma, pili ni uhaba wa dola za kununua mafuta yenyewe; na tatu, ni suala la matatizo ya *storage* ya eneo la uhifadhi wa mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba tulikuwa na tatizo lingine la ubora ambalo sasa hifi mfumo huu wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja *(bulk procurement)* umesaidia sana kudhibiti ubora wa mafuta. Hata taarifa ya *EWURA* inaonyesha vituo vilivyokaguliwa asilimia 96.8 mafuta yake yameonekana ni mazuri kabisa. Kwa hiyo tumeweza kufanya kazi kubwa sana ya kudhibiti ubora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa jambo ambalo nilikuwa nalitazama na ambalo nataka niliwekee mkazo ni kwamba, sisi tumepata gesi nchini kwetu na tunaendelea kuvuna gesi, na gesi ina matumizi mbadala ya mafuta katika maeneo mengi. Leo taarifa inaonyesha kwamba, kutoka magari 1,300 sasa tumekwenda mpaka magari 3,000 ambayo sasa yamewekewa mifumo ya kutumia gesi badala ya mafuta ya nishati. Haya ni mapinduzi makubwa sana na ambayo yanatakiwa yapewe kasi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunanunua mafuta kwa bei kubwa na mfumko wa bei ni mkubwa nchini, sasa kama magari yetu tunaweza kutumia kutumia gesi badala ya mafuta; kwa nini tusiongeze kasi kubwa sana ya kuzalisha gesi na kuweka vituo vya kujaza gesi? Vilevile, kuongeza magari yanayowekewa mifumo ya kutumia gesi ili tuondokane na suala zima la kuongeza idadi ya lita za mafuta tunazonunua Badala yake tuzipunguze ili tuondokane na mzigo huu wa kutafuta dola kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano tu. Ni kwamba, inaonyeshwa gari ndogo iliyowekewa mfumo wa kutumia gesi inaweza ikatumia gesi ya shilingi 16,000 kusafiri umbali wa kilometa 200. Lakini kilometa hizo hizo 200 gari hiyo ndogo ikitaka kusafiri kwa kutumia mafuta basi itatumia pesa siyo chini ya shilingi 60,000, kwa hiyo, ina-*save* karibu shilingi 40,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukaona kwamba huu ni ukombozi mkubwa sana. Tukiweza kutumia gesi kwenye gari zetu nyingi tutaweza kufanya gharama za usafiri na usafirishaji ziwe nafuu sana katika nchi yetu. Sasa changamoto katika hili inakuja kwenye maeneo yafutayo: - *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja; lazima tuongeze uzalishaji wa gesi, yaani kuvuna hiyo gesi kwenye visima. Pili, ni lazima tongeze hizi *filling station*. Kwa sababu watu wakiweka mifumo ya kutumia gesi katika gari zao halafu hakuna vituo vya kutosha vya kujaza gesi itakuwa ni usumbufu mkubwa. Kwa hiyo, hili nalo ni changamoto ambayo Wizara lazima iendelee kulitazama.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine katika hilo ni hizi *accessories* zinazowekwa kubadilisha au kuongeza mfumo wa kutumia gesi katika magari. Gharama yake imekuwa kubwa. Taarifa inaonyesha kwamba gharama inafikia shilingi milioni mbili. Sasa watu wengi hawawezi ku-*afford* kubadilisha hiyo mifumo. Kwa hiyo, lazima Serikali ije na mpango. Kwanza wa kuhakikisha tunapata gharama nafuu ya hizi *accessories* za kubadilisha magari kuja katika mfumo wa gesi, lakini pili, ikiwezekana kuondoa kodi katika vifaa hivi vinavyoweza kuletwa kwa ajili ya kubadilisha magari yetu kuja katika mfumo wa gesi ili kuwezesha magari mengi zaidi kubadili mifumo kutoka kutumia mafuta kuja katika kutumia gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hilo, Serikali ni mdau mkubwa sana katika matumizi ya mafuta. Lazima Serikali sasa ndiyo iwe ya mfano. Tunatarajia mwaka ujao wa fedha, Serikali iangize magari ya kutumia gesi badala ya kutumia mafuta. Ili Serikali yenyewe iwe mdau wa kwanza wa kutumia gesi. Hili liko katika mpango wa Wizara na ninajua watalifanyia kazi kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni mimi niliongoza ujumbe wa Wabunge wenzangu wa Kamati ya Nishati na Madini kufanya ziara nchini India ili kuangalia wenzetu wanavyotumia gesi. Asilimia 65 ya magari yanayotumika nchini India, yanatumia gesi na umeme. Ni asilimia 35 tu ndiyo wanaotumia mafuta. Hawa wameweza kukata gharama kubwa sana ya uendeshaji na hawapati *burden* kubwa ya kutafuta dola kwenda kuyatafuta mafuta huko yaliko. Kwa hiyo, jambo hili nasema ni vizuri lipewe nguvu kubwa sana na Serikali na sisi kwenye Kamati tumeliona kwamba Serikali iko *serious.* Tunataka iongezewe kasi katika kutekeleza hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho katika kuchangia, liwe ni suala la umeme. Gharama ya uzalishaji wa umeme ni kubwa sana, na hasa miundombinu ya uzalishaji wake. Leo tunakwenda kukamilisha Bwawa la Mwalimu Nyerere. Zaidi ya shilingi trilioni sita zimetumika kwa ajili ya mradi huo. Hii ni karibu asilimia 18 ya bajeti nzima ya nchi ambayo ni kama shilingi trilioni 44. Kwa hiyo, miradi hii ya umeme ina gharama kubwa sana

kuianzisha. Ninachokusudia kusema nini? Serikali isijibebeshe mzigo mkubwa wa kuendelea kuanzisha miradi ya kuzalisha umeme, ikaribishe sekta binafsi ili waweke mifumo ya kuhakikisha wanaweka uzalishaji wa umeme kwa njia ya ubia au kwa njia ya mikataba. Yaani wawekezaji hawa wazalishe umeme, *TANESCO* iununue na kuwapa huduma wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka ieleweke, hata hili Bwawa la Mwalimu Nyerere lilikamilika leo na umeme wote *Megawatt* karibu 2,150 wote ufike mahali uingie nchini kwetu bado tutakuwa na upungufu wa umeme kutokana na mahitaji makubwa ya umeme katika migodi ya madini na viwanda ambavyo vinaendelea kukua. Kwa hiyo, ni lazima tuanzishe *projects* mpya za kuzalisha umeme. Umeme wa kutumia makaa ya mawe, umeme wa joto ardhi, umeme wa jua na umeme wa upepo ili tuwe na umeme mwingi. Ukizidi sana tutauza nje, hii ni biashara kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana, nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Musukuma, ajiandae Mheshimiwa Lulida, ajiandae Mheshimiwa *Engineer* Samweli.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nianze kwa kuipongeza Serikali, Waheshimiwa Mawaziri tunaofanya nao kazi, Waziri wa Nishati na Waziri wa Madini, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Tunaona mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuchangia upande wa madini kwa sababu mimi natoka sehemu yenye madini. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa mawazo wake aliyokuja nayo ya kuweza kuonesha nia ya kuipima Tanzania, kwamba mpaka kufikia mwaka 2020/2030 Tanzania yote iwe imekamika kupimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo zuri sana. Tangu tumepata uhuru ni asilimia 16 tu ambayo tulikuwa tumeipima ili kuweza kutambua madini yetu yako wapi. Kwa hiyo, ninachoomba Wizara na Serikali iweke nguvu katika kupima maeneo yote ya Tanzania ili wale wachimbaji wadogo na wakubwa wanapokuja waweze kujua ni sehemu gani wanakwenda kuwekeza ili wasipete hasara na sisi Serikali tuendelee kupata madhuhuri makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili. Ninataka kutoa ushauri kwenye Wizara hii upande wa *STAMICO*. Mara zote nimekuwa nikitoa ushauri, kwamba ni mara chache sana kwa Serikali kufanikiwa upande wa biashara. Tumekuwa na Shirika la *STAMICO* kwa muda mrefu sana limeingia hasara. Sisi wajumbe tuliokuwemo muda mrefu kwenye hii Kamati, tulishafika mpaka kupendekeza *STAMICO i*ondolewe; lakini tunashukuru *MD* Mpya alipokuja alipokuja amefanya kazi nzuri kwa wakati wake. *STAMICO* imefanya kazi nzuri. Tumeenda tumepanda mpaka sasa tumeanza kuwa na mitambo ya ku-*drill* wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tatizo letu Serikalini, unapokuwa umepata sehemu ambayo ni taaluma yako; kwa mfano kwenye ku-*drill*, kufanya *exploration* na mambo mengine, tumeanza tamaa ya kusika kila kona.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina uhakika kabisa kama Bunge hili tutakuwemo kipindi kijacho, tutakuja kujadili. *STAMICO* inapata faida nzuri sana kwenye kuchoronga na inapata faida nzuri kwenye dhahabu; lakini imeanza kuwekeza kwenye vitu vichache vichache ambavyo ndiyo hizi hizi sababu yaliyosababisha *STAMICO* zamani ikaingia kwenye migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, tumeanza kufunga *crasher* la kusaga kokoto. Unafunga *crasher* la kusaga kokoto, huna *connection* na sehemu yoyote utakayouza kokoto. Serikali yenyewe inanunua kokoto mtaani kwa watu wengine. Tuna miradi mikubwa ya viwanja na tuna miradi mikubwa ya majengo, kokoto zote na sehemu zote hizi Serikali inaenda kununua kwa *private sector,* halafu wewe unafunga *crasher* sehemu ambayo mnategemea kuuza kwenye nyumba za watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii siyo biashara na mwisho wa siku tunakuja kuziuza. Tulikuwa na *crasher* kama hilo, pale pale na lilikaa mpaka likapigwa mnada bila kufanya kazi. Ninashauri sana Serikali kwenye sehemu ya biashara iache *private sector*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo mifano mingi. Sasa tunaenda kuanza kuuza makaa yama we. Yaani shirika linaanza kufungua duka la kuuza mkaa wa shilingi 2,000. Hivi ni vitu vya ajabu; na duka lengewe upande wa kuuza mkaa, kuna mkurugenzi na kuna manunuzi; mkaa wa kupima wa mafungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana na nimuombe Mheshimiwa Waziri, kama kuna sehemu unaenda kutumbukia ni kuruhusu *STAMICO* iende kufanya biashara. Unaanza kuuza *carbon* na vilipuzi; huku mtaani vilipuzi sisi tunauziana kienyeji, hamna afisa manunuzi, *MD*, hamna nani. Unaambiwa chukua utalipa ukiuza. Sasa haya mambo ukiweka kwenye Shirika la Serikali, ninaamini kabisa tunaenda kutumbukia na Serikali itaingia hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninawaomba tusimame kwenye kazi ya kuchoronga, Watanzania na wachimbaji wadogo tunahitaji kupata taarifa tu-*stick* kwenye kuchoronga na kufanya hiyo kazi ya uchimbaji, tuache kuingia kwenye biashara, tuachie *private sectors* zifanye kazi hizo za biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ninazungumza suala la vigingi kwa Waziri wa Madini. Tumekuwa na tume nyingi sana Mawaziri wote wamepita pale, Tume ya Muhongo, Tume ya Kairuki, Tume ya Kalemani, Tume ya Biteko, Tume ya Mavunde. Sasa Mavunde ulianza vizuri sana Mheshimiwa Waziri, ninakuomba watu wetu kule tunaenda uchaguzi hatuelewi, labda sasa ikifeli na ya kwako iundwe Tume ya Musukuma, najua Tume ya kwangu haitachukua wiki mbili tutamalizana nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani Watanzania wa Geita wamekaa toka mwaka 1999 watu wamewekewa vigingi unafika mwishoni unaambiwa sisi hatuna shida na hili eneo. Ingekuwa wazungu kweli watu tumeshindwa kujenga tunakaa kwenye

hatihati miaka yote Tume na Tume mmeshindwa kutoa maamuzi? Sasa nadhani hili liwe la mwisho kuzungumza, ulianza vizuri sana Mheshimiwa Waziri, angalia ukifeli itakuja Tume ya Musukuma, sina maana nachukua Uwaziri ila mimi nitaunda Tume yangu ya Musukuma inaenda kienyeji, tutamaliza nao mtakuja kule kutakuwa kumeshatokea matukio. Nikuombe sana fikeni mahali mtusaidie ifike mwisho watu wapate haki yao na mgodi usitutawale kuvunja Sheria za Tanzania. Sheria ziko wazi mnashindwa kutoa maamuzi tunabaki kuwa mbayuwayu kila siku.

Mheshimiwa Waziri wa Madini kuhusu suala la *CSR*. *CSR* nimelia humu kila siku yaani inawezekanaje Serikali inajenga majengo saba kwa milioni 500, mgodi unajenga jengo moja kwa milioni 500 na mkija mko *busy*, njooni mkague tuwaonyeshe, unakuja kusema humu tumeshajengewa miradi ya bilioni 25 iko wapi, twende mtu akatuoneshe iko wapi hiyo miradi, tunajengewa miradi ya takwimu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo *CSR* ya mwaka 2022 haikufanya kazi bilioni 4.3 mpaka tumekuja *CSR* ya 2023 haikufanya kazi, tumekuja kuwa na bilioni 8.6 nayo tumemaliza mwaka jana mwezi wa 12, tuna bilioni 8.6 hatujatumia hata shilingi. Mheshimiwa Waziri na wewe ni kijana na pia ni Mbunge wangu wa hapa Dodoma sidhani kama hili suala litakushinda wewe ni Mwanasheria na mimi ni msaidizi wako kule Geita ‘Daktari’ tunafeli wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya mabilioni ambayo ingeweza kuisaidia Serikali haina Mkaguzi, halafu inakuja kuletewa *special audit*, inakuja kuletewa CAG! CAG akikagua anatupatia sisi hati chafu, wakati kwenye kanuni mmeweka sisi mnatuita *oversee,* ninyi mnaoangalia moja kwa moja na kutunga hizo kanuni njooni basi mkague. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri kwa kweli sidhani kama hili suala litakushinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuomba suala la wachimbaji wadogo tunategemea sana *STAMICO*, tumenunua mitambo, isiwe mitambo ya kupigia picha, tunahitaji hii mitambo iende ikasaidie wachimbaji wadogo kama mlivyomsomea Mheshimiwa

Rais taarifa pale. Wachimbaji wadogo tunataka kuwa na ripoti tuache mambo ya kumaliza kutafuta maeneo ya kuchimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachangia kwenye nishati, Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, nikuombe sana, kuna vitu ukifikiria kibiashara unajiuliza sijui wenzetu wasomi huwa mnafikiriaje. Huku Mikoani mmeweka Mameneja, mmeweka Wakurugenzi, mmeweka Maafisa Manunuzi lakini kule ukiungua hata waya kununua mpaka Dar es Salaam, sasa wale mmewaweka wa kazi gani, kwa nini msigatue madaraka haya mambo yakafanyika Mikoani, kwa sababu kila Mkoa una Mameneja, una Wakurugenzi una Taasisi nzima na magari yamejaa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wamekaa kusaini manunuzi mpaka yaende Dar es Salaam, ndiyo mnasababisha kujaza wala rushwa pale kwenye ofisi yako ya *TANESCO*. Mheshimiwa Waziri ninakuomba gatua madaraka haya mambo mengine, vikombe, goroli tununulie mikoani ili haya mambo yaende *speed*. Kwa sababu tuna makusanyo yetu, rudisha mamlaka mikoani vinginevyo hatuna sababu ya kuwa na Wakurugenzi, tuwe na kompyuta mbili na mtu wa *customer care* na mtu wa ku-*report* matukio ofisi ibaki Makao Makuu, kwa nini unarundika watu ambao hawana kazi, wana kazi ya kuandika na kupeleka madokezo hayajibiki! Ndiyo yanasababisha ukiritimba na *bureaucracy* hapo, ukienda *TANESCO* unaomba *transformer* moja miezi sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri sana upande wa *TANESCO* kwa kweli lazima pafanyiwe maboresho na muwekeze kwenye ile miradi kwa mfano, Geita sisi tunapokea umeme kutoka Rusumo, lakini kutoka Rusumo mpaka Mpomvu - Geita, mimi sijasomea umeme hakuna sehemu ya kupooza umeme likianguka tawi tu likakata umeme inatoka Geita yote, Sengerema hadi Kahama. Sasa wasomi mnafeli wapi, kwa nini msiwe na *alternative?* Itafika mahali tumuombe Rais, atupe nafasi tuwasaidie naona kama tunazinguana sana, tunawaambia hamtusikilizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri kuhusu *TANOIL; TANOIL* ndiyo haya mambo ninayowaambia ya biashara, aliyekuwepo kwenye Kamati enzi zile nilikataa mimi *TANOIL* kuwarundikia hela kwenda kufanya biashara. Tumeweka bilioni 100 kwa mwaka mmoja zimebaki 25 sijui 30 halafu nawaona mmezungusha mabati kila siku, kila sehemu vituo vipya *TANOIL* mmetuuzia nembo kule mikoani au mnafungua vituo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vinakaribia kumaliza mwaka hamna fedha, mmeshazila zote. Mme-*declare* huku bilioni 25 hasara kwa mwaka mmoja, sasa si afadhali vile vituo muwape *private sectors* wafanye biashara? Ninawaomba sana Serikali, *private sectors* ndizo zimeumbwa kwa ajili ya biashara, huku kwenye *procurement*, manunuzi, hamtaweza kulipia hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Musukuma muda wako umekwisha. Tunaendelea na Mheshimiwa Lulida, ajiandae *Engineer* Samweli na Mheshimiwa Zacharia ajiandae.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninakushukuru kwa kunipatia hii nafasi na nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema aliyenijalia na kutujalia sisi sote tukiwepo hapa na tukiwa na afya njema. Vilevile napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais ni mdau mkubwa wa mabadiliko ya tabianchi, naizungumzia Tanzania kwa upana na tuje tupewe taarifa za kutosha na elimu ya kutosha ili tuweze kuisaidia nchi yetu iangalie mabadiliko ya tabianchi na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia suala la Nishati hasa umeme. Mwaka 2007 nilikuwa katika Kamati ya Maliasili hii Kamati ilikwenda kutoa wafugaji Ihefu mpaka Mbarali ili kuhakikisha maji yanaingia katika maeneo ya Mto Ruaha, Kihansi, Kilombero, Mtera na mpaka Mwalimu Nyerere. Haikuwa kazi ndogo ilikuwa kazi kubwa sana, maji ambayo yanaingia katika maeneo hayo yanatoka katika *Congo Basin*, lakini baada ya kutoka katika *Congo Basin,* yanateremshwa katika Maporomoko ya Kalambo, Kalambo yanaingia Usangu, Usangu inaingia Ruaha,

Ruaha inaingia Kihansi, Kihansi inaingia Kilombero na yanatawanyika mpaka Mtera.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kuhuzunisha Kamati tumekwenda Mbeya, maji na mvua za kutosha Mbeya tumekuta pale Mtera utafikiri uwanja wa mpira hakuna tone la maji. Pembeni ambapo wavuvi wapo, maji ni mengi mimi nikajiuliza maswali hiki ni nini ninachokiona haya maji inakuaje hayaingii pale katika Bwawa lakini kaangalieni pembeni kushoto maji yamefurika ni mabwawa mpaka tunamaliza ile Mtera.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii hali siyo ya kuiachia. Nimevuka, nimetembea kutoka Lindi kuja Dar es Salaam, pale Daraja la Mkapa, Bonde la Tuta la Mchanga hakuna maji yanayovuka kwenda Mafia. Hii ni athari kubwa ya nchi, tukitegemea kama tutacheza michezo hiyo hii nchi itaingia katika giza ambalo tutategemea kununua majenereta na vitu ambavyo vitamuathiri na Mtanzania katika uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapozungumzia mabadiliko ya tabianchi na watu wanacheza na mifumo ya maji ina maana hata Bwawa la Mwalimu Nyerere halitafanya kazi itakuwa historia. Kuna watu waliapa kwamba Bwawa lile halitafanya kazi, Watanzania tuoneshe uzalendo tuhakikishe lile Bwawa linafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ikakae ijiulize kwa nini Bwawa la Mtera haliingii maji na kwa nini maji ya kutosha hayapo. Mvua zinazonyesha na kuporomoka kutoka Mbeya mpaka zinafika pale, eneo lile ni kavu kabisa hakuna maji yanayoingia ndani ya Bwawa, hakuna maji yanayoingia Kilombero, hakuna maji yanayoingia Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni uhujumu wa uchumi watu waende wakaangalie kuanzia *Congo Basin*, wakangalie Usangu, wakaiangalie Kalambo, wakaiangalie Ruaha, wakaangalie Kihansi, wakaingalie Kilombero, wakaiangalie Mtera mpaka Mwalimu Nyerere, tuje tupewe majibu ya haraka ili nchi hii isije ikawa ni shamba la bibi watu kutaka kuuza majenereta, watu

kuleta makampuni yafanye kazi baada ya kuhakikisha miradi yetu ile inakufa, mimi naumia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaona hiki nilikuwepo ndani ya Kamati na baadhi ya Wajumbe niliokuwa nao katika Kamati, alikuwepo Mheshimiwa Ndugai, tulikuwa naye katika Kamati hiyo mwaka 2007. Hii hali siyo ya kuichekelea, tunavyo viwanda ambavyo vinategemea umeme, tuna makampuni makubwa ya mafuta *petrol station* zinategemea umeme, kwa kutegemea umeme wa majenereta mnaionaje nchi mnapoipeleka? uchumi utaanguka!*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili nitazungumzia madini. Mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma Mikoa ambayo ilikuwa inaonekana maskini sasa hivi ni Mikoa tajiri sana. Ruvuma makaa ya mawe, Lindi mradi wa Gesi wa *LNG* unatokea pale, Mtwara mradi wa gesi mkubwa umetokea Mtwara na mradi wa Gesi Asilia umekuja kuzinduliwa Lindi na Mheshimiwa Kalemani. Lakini bahati mbaya na masikitiko makubwa mikutano yote ya gesi inafanyika Arusha na Zanzibar, lakini wananchi wa Lindi, Mtwara na Ruvuma hatujui kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapata kigugumizi kikubwa kujiuliza pale unapotoka mradi hatuambiwi chochote, wananchi wamekuwa wanatuuliza maswali ambayo hayana majibu, tunaulizwa je *LNG* imetoka Lindi hata mwananchi wa Lindi kuambiwa jamani kuna *LNG* katika Halmashauri haujafanyika mkutano hata mmoja kujua nini maana ya *LNG*, nini faida ya *LNG*, faida ya *local content* inayotakiwa kwenda kwa wananchi ni kitu gani hakuna, idadi ya *corporate social responsibility* kwa wananchi hakuna, wafanye nini ill wananchi hao waondokane na umaskini hakuna, hivyo Mtwara, Lindi na Ruvuma kimya.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tufike mahali tujiulize Kamati ilikwenda mpaka huko kote lakini Kamati ya mwaka 2014 baada ya kuanzishiwa mradi ya *optimus* Mtwara tulikwenda kujifunza huko Trinidad and Tobago, tukajifunza mengi ndiyo maana sasa hivi tunaona tunaweza tukazungumza kitu. Lakini

jiulize mwananchi wa Lindi, Mtwara na mwananchi wa Ruvuma wako wapi katika miradi hii, hakuna!

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Lindi sasa hivi umepatikana *graphite* ya kutosha, tunamshukuru Mheshimiwa Rais, Mungu amlinde ampe afya njema alituita Ikulu, kutuambia tumekuleteeni mradi mkubwa wa *graphite,* jiulize wananchi hawa wa Mkoa wa Lindi ni lini wameitwa hata kuambiwa jamani kuna moja, mbili, tatu kuhusu *graphite*? Kama hatupewi taarifa hizo itakuwa tunarudi nyuma, miradi hii itakuwa kwa wageni ma wananchi wa Lindi watakuwa maskini, haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tufike mahali mabadiliko ya maendeleo ya uchumi yawaguse na wenyewe wazawa wa eneo hilo. Tutafikia mahali ambapo atakuja mtu kuchuma tu maana yake wameambiwa Lindi kuna *nickel*, dhahabu, kuna madini mchanganyiko, Lindi kuna *gypsum* lakini unaona madude yale yote hayaendelezi wananchi wa Lindi, Mtwara na Ruvuma yanawaendeleza wageni, ni lini tutafikia mahali ambapo tutaleta mabadiliko? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji mabadiliko ya kweli ili tunapotaka kurudi hapa tunataka Wizara iende Lindi, ikafanye mikutano Lindi, Mtwara na Ruvuma ili ituambie maendeleo ya madini haya tuliyonayo yanawafaidishaje wananchi wanaozunguka katika maeneo yale. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikataba mibovu. Mikataba mingi haijabadilishwa, leo mikataba inakuambia kilichokuwa chini ya ardhi ni cha Serikali, wewe uliyekuwa juu unatolewa kama huna chochote. Kitu ambacho najiuliza tutaendelea kumfanya mtu huyu, hata kumpa hisa ya asilimia tatu ili utajiri ule uweze kuwasaidia na watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikwenda *Trinidad and Tobago* Wabunge wakati huo wa Mkoa wa Mtwara na Lindi walitengeneza *local content,* kwanza kutengeneza *low-cost design houses* (nyumba za bei nafuu) kwa watu ambao wataathirika katika maeneo yao, vitu ambavyo havifanyiki hivi. Walifanya makosa yao Geita, Simiyu sisi tunataka sasa hivi haya

yasirudie, tunataka Mikoa hii kama tunataka kukimbia kwa uchumi, tukimbie kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuende tuangalie mikataba ile ambayo haimfaidishi mtanzania, ilete mabadiliko ya Uchumi, kama anakuja mwekezaji katika eneo la shamba la mikorosho, yule mwenye shamba lake anapewa nafasi, anapewa hisa yake ili mkorosho wake unaokatwa pale awe yeye ndani, watoto wake na wajukuu zake wapate uchumi endelevu. Haiwezekani anakwambia nakata mkorosho unanilipa shilingi laki moja, lakini mimi nakaa katika mkorosho zaidi ya miaka 20 na wajukuu zangu watapata faida ya mkorosho lakini ukinitoa kienyeji umeniumiza, umeniingiza katika umaskini na sijui nitapanda tena lini mkorosho ili uweze kunisaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo suala lisiwe Lindi, liwe Morogoro kokote ambako kutaonekana uchumi endelevu wa mazao haya au manufaa ya madini iwe ni maendeleo ya Watanzania, kwa pamoja tunaweza, kwa pamoja mikataba mibovu irekebishike ili wananchi wa Tanzania wanufaike na miradi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninarudia tena suala la umeme. Tulikwenda juzi Mkulazi, tumetegemea Mkulazi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lulida kengele ya pili hiyo.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, haya ahsante baba yangu, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa *Engineer* Samweli, jiandae Mheshimiwa Issaay, jiandae Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna.

**MHE. ENG. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze mchango wangu kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya na kuweza kusimama siku ya leo kwenye Bunge lako. Pia niendelee kutoa pole kwa Wananchi wa Hanang' ambao waliathirika kwa namna moja au nyingine na maporomoko ya Mlima Hanang' pia wale ambao walipata athari za mvua hizi za *El Nino* hasa maeneo ya Basutu, eneo la Mogitu, eneo la Basodeshi na maeneo mengine ambayo yalipata changamoto iliyotokana na mvua zetu hizi za *El Nino*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuwashukuru wananchi wa Hanang' kwa kuendelea kuniunga mkono katika utekelezaji wa majukumu yangu ya Ubunge ili kuiletea Wilaya yetu ya Hanang' maendeleo endelevu chini ya usimamizi thabiti wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais ambaye ameamua kujitoa kwa ajili ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitakuwa nimetenda haki kama sitaishukuru familia yangu hasa mke wangu Elizabeth, kwa sababu wakati ambapo nikiwa nimebanwa na majukumu yangu yeye amekuwa muhimili imara wa familia na hasa amekuwa mshauri wangu mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, kwa jinsi ambavyo amekuwa akiongoza Kamati, amekuwa akifanya vizuri, mmeona alivyowasilisha taarifa yetu ameiwasilisha vizuri. Ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Waziri wa Madini, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati kwa ushirikiano mkubwa ambao wamekuwa wakiipatia Kamati yetu wakati wa utekelezaji wa majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie eneo la uzalishaji wa umeme. Nianze na bwawa letu Bwawa la Mwalimu Nyerere, Bwawa hili kwa sasa limefikia asilimia 95.83 ya utekelezaji wake ambako zimeshalipwa fedha shilingi trilioni 5.83. Niseme tu kwamba bwawa hili toka linaanza kujengwa kumekuwa na maneno mengi ya kukatisha tamaa. Mimi nipongeze kazi kubwa, kazi nzuri ambayo inafanyika kwa utekelezaji wa mradi huu

mkubwa ambao utatuondolea adha ya umeme. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa nguvu kubwa ambayo ameiweka kwenye utekelezaji wa Bwawa hili. Amekuwa akitoa fedha kwa wakati na certificates zinalipwa kwa wakati ili bwawa hili liweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kumtia moyo Mheshimiwa Rais, asisikilize maneno ya wanaomkatisha tamaa. Niendelee kumtia moyo Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Dkt. Doto Biteko, maneno ni mengi ya kukatisha tamaa lakini yeye apige mwendo mbele ili kukamilisha mradi huu. Mradi huu utatusaidia kutuondolea adha ya umeme tuliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bwawa hili litakapokamilika litazalisha megawati 2,115, ambayo itaongeza kwenye umeme ambao tunao tunaouingiza kwenye Gridi ya Taifa ambao kwa sasa ni *megawatt* 1,878. Ili mitambo yetu ya uzalishaji iweze kuzalisha kwa tija lazima tuwekee mkakati mahsusi wa matengenezo na matengenezo kinga, kwa sababu mitambo yote inayo muda wa kuishi *(life span)* ya mitambo yetu, mitambo yote ina mpango mahsusi wa matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa katikati tumekuwa na changamoto hiyo ya kwamba mitambo mingine imekuwa chakavu lakini haijafanyiwa matengenezo ya muda mrefu, tukiweka mkakati mahsusi wa namna ya kuhudumia mitambo yetu tutapata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kiwango kikubwa sana cha matumizi yetu kwa sasa iko kwenye megawati 1,400; tukiunganisha umeme wa Bwawa la Julius Nyerere na tukatunza mitambo yetu tutaondokana na changamoto ambayo tunakutana nayo ya uhaba wa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe wenzangu hasa Wahandisi wazingatie sana eneo la kusimamia mipango yetu kwa umakini kwa sababu kwa sasa hivi ukiangalia karibu 36% ya uwezo wa uzalishaji unapotea. Moja ni kwenye suala la uhaba wa maji, lakini lingine ni kwenye uchakavu; na lingine kwenye upande wa mitambo ambayo inatumia gesi kwenye upungufu wa gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tu kwamba haya masuala tuyapange vizuri mapema ili hatimaye tusipate changamoto hii ambayo tunakumbana nayo ya uzalishaji wa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mgao wa umeme ilitutesa, lakini kuna maeneo mengi nchini, suala la *line* ndefu na umeme kukatika kutokana na hitilafu imekuwa nayo ni changamoto kubwa, kwa mfano kwa Wilaya ya Hanang tumekuwa na changamoto kubwa kwa sababu umeme wetu umetoka Singida ukaenda Babati, kutoka Babati hiyo *line* inatoka kutoka Babati sasa iende Wilaya nzima ya Hanang maeneo ya Basutu mpaka Haydom. Ikitokea tawi la mti limedondoka popote umeme umekatika na tunapataga meseji nzuri sana kutoka kwa wataalamu wetu wanasema taarifa ya katizo la huduma ya umeme, baada ya taarifa hiyo tu inakuja taarifa ya katizo la huduma ya maji kwa sababu umeme tunautegemea kwenye eneo la maji. Ni muhimu tutekeleze ule mradi wa Gridi ya Imara na kujenga kituo cha kupooza umeme Wilaya ya Hanang na naamini hili ni tatizo ni maeneo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru sana Serikali, wakati wa bajeti tulikuwa tunalia kwamba vitongoji 15 tulivyopewa ni vichache, lakini tulipata *amendment* ambapo vitongoji vimeongezeka, lakini na Mradi wa *REA* unaendelea kukamilika. Niipongeze sana kwa kazi nzuri inayofanyika na tuendelee na kasi hapo ili tuhakikishe kwamba wananchi wetu wanapata umeme wa kutosha na tunapopeleka umeme vijijini na tunapojenga viwanda maana yake mahitaji ya umeme yanaongezeka na maana yake tuwekeze zaidi kwenye uzalishaji eneo hili la kuzalisha tuweke nguvu kubwa, lakini pia ile miundombinu ya usafirishaji wa umeme ambayo imechakaa tuikarabati kwa wakati ili tuwe na umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nichangie kidogo eneo la gesi asilia; ameeleza Makamu Mwenyekiti wa Kamati yetu Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda umuhimu wa gesi hii na umuhimu wa kusambaza vituo vya kutolea huduma ya gesi asilia ili magari yetu yaweze kutumia gesi badala ya kutumia mafuta ambayo tunaagiza kwa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao mradi mkubwa sana wa *LNG* mradi wa dola za Kimarekani bilioni 42 ambapo ni takribani trilioni 107 za Kitanzania. Mradi huo unahusisha kampuni sita ikiwepo Kampuni yetu ya *TPDC* ambao utajengwa eneo la Likonge – Lindi. Mradi huu ukikamilika utatusaidia sana kuongeza pato la Taifa, lakini utatoa ajira za kudumu kwa Watanzania kwa 6000 za kudumu… *(Makofi)*

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa *LNG* unatekelezwa katika eneo la Likong'o katika Mkoa wa Lindi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Injinia Taarifa hiyo.

**MHE. ENG. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana hii Taarifa naipokea ni kwa sababu tu marafiki zetu wa Kusini lugha yao ya Kiswahili na ya kwetu huku Kaskazini ni tofauti kidogo, lakini neno ni hilo hilo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninachosema mradi huu utatoa ajira za uhakika kwa Watanzania, lakini pia utachangia kwenye ukuaji wa sekta zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye miundombinu ya barabara, vituo vya afya na sekta yetu ya umeme, lakini pia *LNG* tutaitumia kwenye magari. Mradi huu ukitekelezwa nchi yetu itachangamka. Majadiliano ya awali yalifanyika kati ya Serikali na wawekezaji na yamekamilika mwezi Mei, 2023 na ukiangalia toka Mei, 2023 mpaka sasa takribani miezi tisa kwenda kumi ni muda mrefu sana na mradi huu ni muhimu kwetu na ni mradi wa kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema hapa kwenye mambo haya mambo makubwa mazuri ya kukwamua uchumi wa nchi yetu, hebu tuweke mikakati mahususi na kuweka

alama za utendaji ili kuhakikisha mradi huu una-*take off* haraka ili hatimaye Watanzania wapate manufaa ya uwekezaji huu mkubwa, lakini pia tuokoe fedha za kigeni ambazo kwa kweli kwa sasa zimekuwa adimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nihitimishe mchango wangu kwa kuongelea kidogo eneo la mafuta hasa kwenye Kampuni yetu ya *TANOIL*. Sheria yetu ya Petroli ya mwaka 2008 kifungu cha 30 ilianzisha umuhimu wa hifadhi ya mafuta. Nachotaka kusema wakati nikihitimisha kwenye eneo hili wakati tunavyotengeneza…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** *Engineer* muda wako umekwisha, kengele ya pili hiyo.

**MHE. ENG. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sasa namuita Mheshimiwa Flatei kapata dharura kaondoka, anakuja Mheshimiwa Aleksia Kamguna.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi anavyotupamabania Watanzania na wasaidizi wake wote. Pia natoa pole kwa Serikali kwa mvua ambazo zinaendelea za *El-Nino* zimeharibu miundombinu mingi ya barabara na ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania au Serikali kwa muda mrefu sana tumetegemea sana tumetegemea sana vyanzo vichache vya kuzalisha umeme na vyanzo hivi vichache vya kuzalisha umeme tunategemea sana gesi na tumetegemea sana maji ambapo kwa sasa hivi kwa karne tuliyonayo hivyo vitu havitutoshi na wala havitoshelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mabwawa yetu yanatengenezwa huenda Watanzania walikuwa wachache labda tulikuwa milioni 30, lakini sasa hivi tupo zaidi ya milioni 60 na zaidi. Kwa hiyo, ukiangalia hali halisi ukweli tunahitaji mabadiliko ya uzalishaji wa umeme hapa nchini. Kwa nini nasema hivyo; kama ulikuwa na chanzo ambacho watu walikuwa wachache kwa wakati ule na sasa wameongezeka ukiwa na chanzo kile kile watu ni wengi kwa vyovyote vile upungufu utatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naishauri nini, kutokana na hali hiyo tuliyonayo ukweli tumefikia mahali pabaya, lakini tubadilike, kutokana na mabadiliko ya tabianchi tuingie kwenye sehemu nyingine sasa, tugundue vyanzo vingine vya kupata umeme, tunavyo vyanzo vingi sana Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuingie kwenye nishati jadidifu. Nishati jadidifu ni nini, sisi Wanakamati wenzetu watu wa nishati walitueleweshа kwamba nishati jadidifu ni nishati ambayo inatokea, unaweza ukapata umeme kutokana na nishati ya upepo, nishati ya jua na nishati ya jotoardhi. Sasa kama tunaweza tukawa tunapata hivyo na wataalamu tunao kitu gani kinatukwamisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wote tunavyofahamu kwamba hali yetu ya umeme ni mbaya na vyanzo tunavyo, wataalamu tunao, sasa tunafeli wapi? Tunawaomba wataalamu ambao tumewasomesha kwa kodi ya Tanzania, najua umeme wa maji ni umeme ambao unapatikana kwa gharama nafuu, lakini huo umeme mwingine unapatikana kwa gharama kubwa, lazima tukubali tubadilike kwa sababu hatuwezi tukategemea chanzo hicho hicho kwa kuwa ni nafuu wakati watu tunaendelea kuteseka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Mungu ametuona tuna hilo Bwawa la Mwalimu Nyerere, lakini hilo Bwala la Mwalimu Nyerere ni bwawa ambalo ni la maji. Kunaweza kukawa na mabadiliko hayo hayo tena mabadiliko ya tabianchi tukapata matatizo. Je, Watanzania/wataalamu wetu tumejiandaaje jinsi ya lile bwawa likitokea labda kuna matataizo labda kuna ukame, kuna nini, tumeweka akiba gani, tumetengeneza sehemu ya

kuweka maji ya akiba ili tusije tukafika siku tukapata tena matatizo kama ambayo tunayapata sasa hivi au tunaendelea kuyapata kutokana na vyanzo vile vya mwanzo havitoshelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika matatizo ambayo tunayapata kutokana na Wizara ya Nishati kutokujipanga, hatujipangi kwamba tumeletewa huu mtambo, tunazalisha, lakini je, itakapotokea wakati wa kukarabati tunakuwa tumejipanga au tunafanya ile zimamoto mpaka umeme umezimika ile mashine imekufa tunatafuta tunaanza kuagiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tuwe na mipango endelevu ambayo itatuwezesha sisi Watanzania au shirika letu ili tuweze kuwa na umeme wa kudumu na badala ya kupelekea kwamba wao watakuwa wananunua, kwa sababu ukiwa na *emergence* kitu cha haraka haraka utanunua kwa bei ghali, lakini ukiwa na mipango ambayo endelevu utanunua kitu kwa bei ya kutulia na hatimaye tunaendelea kupata umeme ambao umekuwa mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine nazungumzia kuhusu vituo; sasa hivi utakuta vituo vyetu vya umeme hivi vya kupoza umeme vipo mbalimbali sana, ni kwamba kama kitupo kipo Dodoma kikiharibika kile kituo cha kupoza umeme kile cha Dodoma inamaana kwamba mikoa mingi labda Shinyanga, Singida mpaka Mwanza vinakosa umeme. Hii inakuwa kidogo kiuchumi inaturudisha nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashauri ikiwezekana tujenge vituo vya kupoza umeme viwe karibu karibu ili tusifanye wananchi wakakosa umeme katika eneo kubwa ina maana kwamba uchumi utakuwa umerudishwa nyuma katika eneo kubwa kuliko tungekuwa na vituo vingi vya karibu karibu, kwa hiyo, wale wachache wangekosa umeme lakini sehemu nyingine zingeendelea kuwa na umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia kuhusu transfoma; Tanzania kuna tatizo la wizi wa transfoma, kwa nini mtu anaiba transfoma wakati transfoma hiyo ndiyo inamsaidia kupooza huo umeme. Nafikiri mimi ni elimu haitoshi; je, Serikali tunachukua

juhudi gani za makusudi ili tuwaelimishe wale Wananchi ambao maeneno yale transfoma zipo wajione kama zakwao unajua sababu wao wanajua kwamba hizi transfoma siyo za kwetu ni za Serikali hata ikiibiwa mimi sina hasara, lakini tukitoa elimu kwa wananchi wetu kwamba hiyo transfoma ni mali yenu wale watu kidogo wachache watakuwa hawajaelewa lakini walio wengi wataelewa na pia sisi wenyewe tutakuwa walinzi, kwa hiyo, kinachotakiwa ni elimu ambayo yakutosheleza kila mmoja ajue namna ya kuilinda mali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye umeme wa *REA; REA* ni umeme ambao umetusaidia sana kupeleka vijijini, lakini ule umeme unakuwa na changamoto nyingi. Kwanza pesa zinakuwa hazitoshelezi, wanapewa fungu ambalo ni pungufu, matokeo yake ikifika wakati wa kujenga ile miundombinu wakandarasi wengi wanasuasua kwa sababu wanakuwa hawajalipwa pesa zao za kazi, ile kazi inasimama, inachukua muda mrefu, baadaye tunawalaumu kwamba jamani mbona *REA* hawakamilishi kazi, watakamilishaje kazi wakati hela hawana ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachoshauri kwamba hawa watu wapewe pesa na walipwe kwa wakati ili kuzuia yale mambo ya rushwa na wakati mwingine tunapomcheleweshea mtu watoe na hizo *certificate* mapema na pia walipwe kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwwa hayo machache nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay atafuatiwa na Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, kwanza niungane na Waheshimiwa Wabunge kumshukuru sana Mwenyezi Mungu wa rehema kutujalia siku hii muhimu katika maisha yetu ambapo leo tunajadili mustakabali wa Watanzania takribani milioni 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Serikali hii imefanya kazi kubwa sana katika majimbo yetu hasa Jimbo la Mbulu Mji, kazi

kubwa sana imefanyika ambayo sikutarajia katika maisha yangu. Huu ni mwaka wa nane nikiwa kwenye Bunge hili na kazi hiyo kubwa iliyofanyika ni jitihada kubwa za Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali yake, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayofanya, lakini pia kwa jinsi ambavyo Mwenyezi Mungu amekujalia nafasi hiyo ya kuwa Naibu Waziri Mkuu na hasa katika Wizara hii muhimu sana ambapo mara nyingi imepigiwa kelele, lakini pia kuna sababu mbalimbali siyo kwamba Serikali haifanyii kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nichukue nafasi hii kwanza kuchangia maeneo machache; tunaendelea kumwombea Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa ajili ya wazo hili la ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Ni wazo aliloanzisha, hata kama lilikuwa gumu kutekelezwa, lakini hatimaye waandamizi waliokuja nyuma yake kupokea kijiti wametekeleza kazi hii kubwa ya Bwawa la Mwalimu Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tujiulize bila Bwawa la Mwalimu Nyerere na saa hizi Mtera kumekauka, leo tungefanyaje, tungeenda wapi. Mimi nilikuwa naona Mungu ametoa ufunuo kwa viongozi hawa na kwa jinsi ambavyo Hayati Mheshimiwa John Pombe Magufuli amekwenda akatekeleza, akathubutu na ni mradi tunaojenga kwa fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapiga kelele sisi Wabunge tunalia umeme, lakini tunataka kila jengo au kila nyumba au kila kaya katika majimbo yetu wapate umeme. Tungepata wapi huo mpango wa umeme kila kaya, kila kijiji na hatimaye kila kaya ni kwa ajili ya uwepo wa Bwawa la Mwalimu Nyerere na kwa hiyo tunaipongeza sana Serikali, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi alivyoendeleza na anaendelea kukamilisha mradi huu muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa jinsi ambavyo

umeingia kwenye Wizara hii bado kuna mabadiliko makubwa hadi sasa yameendelea kutokea na hasa wazo lako la kupinga ununuzi wa mitambo ya dharura, tuendelee kuona mitambo ya dharura siyo njia mbadala ambayo itatusaidia kama Watanzania katika tatizo zima la kupata umeme katika maeneo yetu na hasa hasa ambapo gharama ya ya umeme huo ni mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Lulida alivyochangia kuzungumza Bwawa la Mtera. Mimi ni mmoja kati ya waliopita Bwawa la Mtera hivi punde siku chache zilizopita, nadhani Serikali iende ifanye utafiti wa kina kuhusu Bwawa la Mtera. Lile suala la Bwawa la Mtera ukishuka pale Mtera ukaongea na wananchi wanachokizungumza ni tofauti na Taarifa ya Kamati. Kuna mambo wanayazungumza na tusiyachukie sana, tufanyie utafiti kuna tatizo gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nichukue nafasi hii kuipongeza Kamati; mimi nije leo kuchangia sehemu ya uzalishaji wa umeme, kwa kuwa Bwawa la Mwalimu Nyerere tulitegemea kuwa na umeme wa ziada kutokana na kwamba Bwawa la Mtera litakuwa na maji na litakuwa linazalisha kama sehemu ya upatikanaji wa umeme, nadhani Serikali sasa iende na ione utaratibu wa umeme mbadala kwenye jotoardhi, lakini pia kwenye upepo ili kuhakikisha kwamba tuna umeme wa kutosha nchi nzima, lakini pia hata majanga mengine yakitokea hatutegemei umeme wa maji tu bado tutakuwa na umeme wa vyanzo vingine Kitaifa. Hali ya umeme sasa hivi kwa vijijini wananchi wengi wanasubiri sana, kwa mfano nikizungumza Jimbo la Mbulu Mji kuna maeneo ambayo yapo kilometa mbili katikati ya mji ama kilometa tatu, lakini umeme huo hauwajafikia wananchi kwenye maeneo hayo na tatizo kubwa ni uwezo wetu wa kifedha na hasa wakandarasi hawalipwi fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna haiba ya kwenda kila kijiji kama mpango wetu ulivyo na hatimaye kila kitongoji, tutazame nyuma, nadhani ni wakati muafaka wa kwenda kufanya tathimini ya mapitio upya kama nchi ili tuone sasa Bwawa la Mwalimu Nyerere likianza kuzalisha yale maeneo tunayaingiza kwenye mipango yetu ya Serikali ili walau kila nyumba hasa yale maeneo na nyumba zilizoko ndani ya mita 25 hadi 30 zinafungiwa umeme

ili umeme huu moja kwa moja uwafikie Watanzania walio wengi, lakini pia uzalishe kwa nchi uzalishaji wake uongezeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya maeneo yaliyowekewa nguzo niipongeze Wizara na hata Serikali, mimi sisemi wale waliotangulia hawakufanya kazi, wamejitahidi, lakini Mbulu Mjini tuna maeneo Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, kuna vijiji vya Jimbo la Mbulu Mji vina nguzo tayari, vina karibu mwaka havijafungiwa waya, ukibanana na mkandarasi anasema yeye anasubiri malipo Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani Serikali itusaidie, Kamati imeeleza hapa 32% na kwa mahitaji ya umeme tunaouhitaji na kwa haiba kubwa ya wananchi kuhitaji umeme 32% ni ndogo sana. Mimi nadhani Serikali itazame upya jambo hili kama vyanzo vya nje hatujapata fedha, basi tutazame njia nyingine mbadala Mheshimiwa Rais ametatua mambo mengi sana, katika jimbo langu amefanya miradi sijategemea mikubwa iliyokwama miaka ya 40; leo hii tunapozungumza uzalishaji wa umeme na usambazaji wa umeme tunashindwa kulipa wakandarasi, tuna hasara mbili; moja kukosa umeme kwa wakati; lakini la pili pia gharama kubwa ya ucheleweshaji wa wakandarasi inaipa Serikali gharama kubwa ya ucheleweshaji. Hali ambayo tunalipa gharama ambazo hazikutarajia na Serikali katika mipango yake ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii tukiendelea nayo athari yake ni nini? Athari yake ni kwamba wananchi wanaichukia Serikali yao lakini pia hawapati ile huduma wanayoitarajia. Pia tunawalipa wakandarasi fedha ambazo hawajazifanyia kazi wamechelewa kulipwa. Hiyo hali ya malipo ipo kwa nyakati tofauti tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi hayakufikiwa na umeme katika nchi hii, hasa maeneo ya migodi, taasisi za Serikali, taasisi za mashirika binafsi na maeneo mengi ambayo umeme unasubiriwa. Unakuta kwenye Kijiji umeme una miaka mitano, sita hadi kumi lakini kuna nyumba za walimu hazina umeme, kuna baadhi ya shule hazijafikiwa kutokana na jiografia ya maeneo tuliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni nini? Ushauri wangu ni kwamba walau tutazame nyuma. Tuangalie nyuma tuone tunawezaje kufanya kazi hii ya kujaza hayo maeneo ya ujazilishi ili pamoja na usambazaji wa upelekaji tusiwe na viraka vya miradi ya umeme ambayo utakuta kwenye Kijiji chenye kaya mia 300, kaya 50 ndizo zina umeme halafu kaya 250 hazijafikiwa na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie eneo lingine ambalo linatupa nafasi kubwa sana katika taarifa ya kamati. Tunaipongeza kamati, wamegusa sehemu nyingi hata kama ni kwa muhtasari lakini wamejitahidi. Eneo la uchimbaji wa madini, tusipoangalia nchi yetu itakuwa na mashimo mengi sana huko tuendako ya uchimbaji ambao hauna tija na hauchukui kitaalam, hatimaye tunabahatisha kuchimba na hawa ni wachimbaji wadogo. Na hawa ndio walio wengi katika nchi yetu na maisha yao wanategemea katika hayo maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa nashauri, kama inawezekana ile timu yetu ya Serikali ipite na itoe tafsiri sahihi ya maeneo hayo. Madini yanapatikana kwa kiasi gani na upatikanaji wake uko katika sura gani katika umbali wa ardhi na katika miamba ya ardhi ili kuweza kuwarahisishia wananchi walio wengi, wanapochimba na wale wachimbaji wadogo wasitumie nguvu kubwa sana lakini gharama ndogo yenye manufaa kwa kazi ndogo wanayofanya wanapata manufaa makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya mwisho ni kwamba katika maeneo mengi ambayo..., (nimalizie mchango wangu) Wabunge tunapiga kelele ili umeme uende kinachotokea ni uunganishwaji wa mita 30 kutoka ilipo nguzo, ama-*line* kubwa ama katika Makao Makuu ya Kijiji ulipoenda umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta mpango wa awali ulikuwa kilomita mbili kila upande sasa zile kilomita mbili zinashindikana kufikiwa hatimaye tunaishia ndani ya kilomita moja na kwa hivyo umeme unawapata watu wachache kwa sababu maeneo ya kijijini makazi yako mbalimbali na nyumba

zinazotarajiwa ziko mbalimbali na hata hizo taasisi zitakuwa mbalimbali, hali hii itatusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni ukatikaji wa umeme; umeme unavyokatika katika maeneo yetu, hoja kubwa ya tafsiri ya watendaji wetu wa *TANESCO* ni kwamba umeme unapokatika sababu kubwa ni hitilafu na kwa kuwa kila siku unapokatika kunatokea hitilafu, hitilafu, hitilafu. Mimi niombe Wizara, hebu wafanye mapitio upya wa mitambo, miundombinu, kama ni nguzo ama ni mitambo ya kuzalisha umeme ama ya kupokelea umeme ifanyiwe mapitio ili kuona ubora wake umri uliokaa na jinsi ambavyo unahitaji kubadilishwa, ili kusitokee inatokea hitilafu ya umeme kukatika halafu wanaenda kurekebisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio hayo yakifanyika, yataingizwa kwenye mipango ya Serikali ili walau maeneo yote ambayo yanahitaji ukarabati mkubwa ama miundombinu mipya itafanyiwa kazi na hatimaye tutapata manufaa ya kukatika kwa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengi yamewasilishwa, niishukuru Serikali kwa kazi kubwa na nikushukuru Mheshimiwa Naibu Spika.

Mheshimiwa Niabu Spika, naomba niunge mkono hoja, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Tabasam, ajiandae Mheshimiwa Mariki, ajiandae Mheshimiwa Regina Ndege.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naomba kuchangia katika Wizara hzi mbili, Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini. Kwanza naishukuru Kamati ya Nishati na Madini kupitia viongozi wetu, Mwenyekiti wa Kamati na Makamu Mwenyekiti wa Kamati, kwa kazi nzuri tunazofanya kwa muda mrefu kwa ajili ya kushauri na kuisimamia sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba tunao Mawaziri na Naibu Mawaziri, tunafanya nao kazi kubwa sana akiwemo Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ambaye alikuwa ni Waziri wetu

wa Madini na sasa hivi ni Waziri wa Nishati, ni wasikivu na bahati nzuri wote wanaijua sekta. Sasa ukiona kuna matatizo tunayazungumza hapa, kwanza tunayazungumza kwa nia njema kama watanzania, lakini la pili sisi ni Wabunge tunasimamia jambo hili. Lazima tuisimamie Serikali na kutoa ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naanza kuchangia, naanza na madini; kule katika madini tunao wachimbaji wadogo, hawa wachimbaji wetu wadogo, wengi wanaajira kubwa katika migodi mingi katika nchi hii. Migodi ambayo wao wenyewe wameitafiti na baadaye wakaanza kuifanyia kazi. Mheshimiwa Rais wakati anaapishwa alikuja hapa Bungeni, na akaja akalihutubia Taifa kupitia Bunge. Mheshimiwa Rais alizungumza kwamba yako maeneo katika *game reserve* na katika *ranch* zetu kule ambayo yana dhahabu, haya yachimbwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo ni kwamba hawa watu wetu wa madini wanazitoa leseni. Wakitoa leseni watu wetu wa maliasili kwa sheria zilizoko kule wanazuia na Rais tayari alishalihutubia Taifa na akazungumzia jambo hili. Yeye aliliona kama Rais wa nchi, amepita kule kwenye kampeni ameona malalamiko na kila wananchi wanapokwenda kutafiti hawa wachimbaji wadogo wanajikuta wameingia katika maeneo ya *game reserve*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili ni jambo ambalo tunataka tupate majibu ya Serikali kwa sababu kama Rais alielekeza na sisi Kamati tunashauri, lakini tunashindwa kuelewa hawa wenzetu wa Wizara ya Maliasili kule kuna tatizo gani wasikae na Wizara ya Madini wakamaliza hili tatizo? Hili tunaliomba sana lifanyiwe kazi na tutaomba majibu kutoka katika pande hizi mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kuhusiana na mgodi. Kule Sengerema tuna Mgodi wa Nyanzaga, huu Mgodi wa Nyanzaga leseni ilitolewa toka mwaka 2002, kwa mujibu wa sheria leseni ni miezi 18. Wananchi wa Sengerema wamekaa wanasubiri mgodi huu ikifika mwezi wa sita, tutafikisha miaka miwili mgodi hujaanza kufanya kazi. Sasa hii ni hatari kubwa na mimi kama mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Sengerema, wananchi walitegemea

kabisa kuna mabadiliko makubwa halmashauri yetu, tulitegemea itakuja kupata *CSR* na malipo kwa ajili ya *service levy* lakini na uchumi ungeweza kuzunguka na leo Sengerema ingeweza kubadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Rais Daraja la Kigongo-Busisi linakwenda kukamilika, sasa tulitegemea kwamba na mgodi huu ungeweza kufanya kazi kama ilivyopangwa, sasa tunataka tujue huu mgodi utaanza kufanya kazi lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri akija hapa, aje awaweleze wananchi wa Tanzania lakini wakiwemo wa Jimbo la Sengerema kuhusiana na matatizo yaliyoko katika ule mgodi. Serikali iwe wazi katika hili jambo kwa sababu kama ni fidia, fidia imelipwa lakini hatuoni kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia suala la nishati ya mafuta na gesi, tunalo Shirika letu la *TPDC,* hili limeanza kufanya kazi toka mwaka 1969 lakini mwaka 1972 limeanza kufanya kazi kwa uzuri na leo ni zaidi ya miaka 52. Linatafiti mafuta na gesi, sasa tunavyo vitalu vya gesi na vitaru vya mafuta, lakini leo tunafanya kazi ya kusafirisha bomba la mafuta kutokea Hoima Uganda kuja Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zetu wa Uganda, kampuni yao ya mafuta haikuanza kama yetu. Sisi tuna maeneo makubwa sana yenye viashiria vya mafuta. Tulitaka kujua je, ni maeneo mangapi ambayo Serikali tayari imeshabaini maeneo mangapi ambayo sasa yana mafuta? Na sisi nchi yetu sasa ianze kunufaika na haya mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TPDC* leo ni miaka mingi wameegemea katika gesi tu lakini huku kwenye mafuta Tanzania inaonekana ina mafuta, sasa na yenyewe ifikie mwisho. Watanzania wanataka kujua je, Tanzania ina mafuta au haina mafuta?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine limezungumzwa hapa suala la *TANOIL; TANOIL* ni mahali ambapo pesa za Serikali ziliwekezwa.

Pesa zaidi ya bilioni 110 zimewekezwa lakini toka mtaji huo umewekezwa ni zaidi ya miaka mitatu Mheshimiwa Rais akapeleka kule pesa. Leo hii tunavyozungumza wana bilioni 19 lakini madeni yaliyopo pale ni zaidi ya bilioni 46. Waliokopa wanajulikana, viongozi waliopewa dhamana ile wapo, sasa imekuwaje, zile pesa ziko wapi. Watanzania wanataka kujua, Je, bilioni 110 zimekwenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, wamenunua maeneo ya vituo vya mafuta, vituo vya mafuta vimenunuliwa hewa, vituo vimenunuliwa vya gharama kubwa. Tungeomba sana hili jambo la *TANOIL,* liundiwe Kamati ya Bunge, kwa sababu Wabunge wamepiga kelele humu ndani kuhusiana na suala la *TANOIL. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo sasa limekuwa sugu, watu wanapelekewa mitaji ya pesa ya Serikali halafu zile pesa zinakwenda kupotea. Tunaomba sana akisimama hapa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu basi awaeleze watanzania. Je, hawa watu wako salama? Kwa sababu kama wamechukua pesa za walipa kodi halafu bado wanaonekana wako mitaani na waliokopa bado wako mitaani, haiwezekani na hizi ni pesa za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la usafirishaji wa mafuta na ushushaji wa mafuta, tuna boya kule *SBM* kule Kigamboni Mji Mwema. Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu analifahamu lile jambo na ameshakwenda kule kwa sababu ni mtu ambaye tuko naye kwenye kamati na ndiye msimamizi wetu kama Waziri wa Nishati wa sekta hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule *SBM* Mji Mwema tuna boya moja tu la kushusha *diesel*, eneo lile linaloshusha *diesel,* meli zinazosimama kule ni *metric tons 110*, lakini tuna maeneo mengine kule *KLJ* Kurasini pale Bandarini, lile eneo linachukua *metric ton 40039* sasa kwa nini lisitengenezwa boya lingine? Tumeshauri katika Kamati, kwamba tutengeneze boya la pili kule ili meli ambazo zinakuja kule zije meli zenye uwezo mkubwa badala ya kukodi vimeli vidogo vidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili litatuletea matatizo makubwa, ndio maana bei za mafuta nchini zinaendelea kupanda na ucheleweshaji wa kushusha mafuta unakuwa ni mkubwa. Tunaomba tushauri, jambo hili lifanyiwe kazi kwa ukubwa kwa sababu tunakwenda kubadilisha suala la kujenga *storage* na miundombinu basi wahakikishe kutokea kule bandarini tuweze kupata boya jingine na tupate bomba jingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini *flow meter; flow meter* zilizoko kule ni za nchi sita lakini bomba zinazoshusha mafuta kule ni bomba za nchi 10. Sasa ucheleweshaji kule unakuwa ni matatizo, kila wakitengeneza zile *flow meter* zinaharibika. *Flow meter* za uhakika zilizoko, zipo *flow meter* pale *KLJ* Kurasini, zile *flow meter* zilizoko pale afadhari zibadilishwe zihamishwe zikawekwe kule Kigamboni ili tuweze kupata uhakika wa pesa za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo niko katika kushauri zaidi, kuna suala la *TANESCO; TANESCO* walinunua nguzo kutoka Busonga kule Jinja Uganda, mkataba wa mwaka 2022 nguzo zaidi ya laki mbili mpaka laki tatu na mpango sio mbaya kwa sababu nguzo zile zimekomaa na ziko katika ubora wa hali ya juu. Zingeweza kutoka kule Uganda kama ilivyokuwa, kwamba watashusha Kemondo kwa ajili ya Mkoa wa Kagera, watashusha Mwanza kwa ajili ya Mkoa wa Mwanza na Simiyu na watashusha Musoma kwa ajili ya Musoma, ili upatikanaji wa nguzo katika Kanda ya Ziwa uwe tayari umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunavyozungumza tunakwenda mwaka wa pili, ule mkataba hatujui ni nini kilichofanyika mpaka sasa hivi, na mpaka sasa hivi nguzo hazijaletwa, lakini tunavyo viwanda vya nguzo za…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia dakika moja tu, tuna viwanda vyetu vya nguzo Morogoro…

**NAIBU SPIKA:** Sekunde tano malizia.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, tuna viwanda vyetu vya nguzo hapa Pwani, viwanda vyetu vya nguzo vya zege, leo hii mvua zinavyozidi kunyesha, viwanda vimezalisha nguzo lakini nguzo hazinunuliwi na hazisambazwi, sasa hatujui tatizo ni nini. Tunaomba sana Serikali itusaidie kuhakikisha usambazaji wa nguzo, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya, ahsante, mengine unaruhusiwa kuandika.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mariki, Mheshimiwa Regina, ajiandae Mheshimiwa Ndaisaba.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika suala hili liloko mezani kuhusiana na Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini. Kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na afya njema, kwa kuniwezesha kusimama tena katika Bunge hili Tukufu kwa mwaka 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo ameendelea kusimamia miradi mbalimbali katika nchi yetu. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuwezesha Bwawa la Mwalimu Nyerere kufikia asilimia 95.8, lakini sitaacha kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Wizara ya Nishati pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Judith Kapinga kwa jinsi ambavyo wameendelea kufanya kazi kwa ukaribu na sisi Wanakamati, kwa kuendelea kuhakikisha kwamba mambo mbalimbali yanaendelea kuboreshwa katika Wizara hii ya Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sitaacha kumpongeza Mheshimiwa Kaka yangu Anthony Mavunde Waziri wa Madini na Naibu wake kwa jinsi wanavyofanya kazi nzuri katika Wizara ya

Madini, lakini pia nawapongeza Makatibu Wakuu wote wa Wizara zote hizi mbili na sitasahau kuwapongeza Mheshimiwa Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Nishati na Madini pamoja na Makamu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bwawa la Mwalimu Nyerere limefikia asilimia 95.8. ni matumaini makubwa sana kwa wananchi wa Tanzania wote kwamba Bwawa hili litakapokwenda kuanza kufanya kazi suala la umeme litakwenda kupata mwarobaini na upungufu wa kukatikakatika umeme katika nchi utakwenda kupungua kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sisi wananchi wa Mkoa wa Katavi, wananchi wa Mkoa wa Kigoma, wana Rukwa tuna matumaini makubwa kabisa Bwawa hili litakapokwenda kukamilika na kuanza kufanya kzi basi Serikali itakwenda kuhakikisha kwamba kipaumbele kikubwa ni kuhakikisha Wananchi wa Mkoa wa Katavi, Wananchi wa Mkoa wa Rukwa na upande ule wa Kigoma kwa maeneo machache tunakwenda kuunganishwa katika Gridi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kabisa Serikali imekuwa ikitumia pesa nyingi sana kutumia umeme kutoka nchi jirani ikiwepo nchi ya Zambia kwa kununua ule umeme. Serikali imekuwa ikipoteza pesa nyingi lakini wananchi tumekuwa tunashida sana ya umeme. Wawekezaji imekuwa ni mtihani mkubwa sana kuja katika Mikoa yetu kutokana na kwamba hatuna umeme wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuiombe Serikali kuhakikisha kwamba kipaumbele kikubwa Bwawa hili linavyoenda kukamilika, Wananchi wa Mkoa wa Katavi, Rukwa na kwa upande mwingine ule wa Kigoma tuweze kuunganishwa katika *Grid* ya Taifa ili na sisi sasa tuweze kwenda kupata umeme wa uhakika, Wananchi wetu wa Mkoa wa Katavi waweze kufanya shughuli zao za kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kabisa, ni matarajio yetu makubwa sisi wananchi wa Mkoa wa Katavi, mama zangu watakwenda kufanya biashara mbalimbali hususan wananchi wa

Mkoa wa Katavi pamoja na Kigoma tunalo Ziwa Tanganyika, ni fursa kubwa kwetu, tuna biashara nyingi, lakini tutakapokwenda kupata umeme wa uhakika ni dhahiri kabisa tutakwenda kuongeza pato kwa Taifa. Tutakwenda kuongeza pato kwa Mikoa yetu lakini pato kwa mwananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuchangia kwa upande wa *REA;* suala la *REA* Serikali imeendelea kusimamia vizuri, lakini ni dhahiri kabisa mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini. Tumefanya ziara nchi nzima, kuna maeneo tumeona kwamba bado wakandarasi wameendelea kusuasua kufanya shughuli hizo za umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, aweze kuhakikisha kwamba kwa wale wakandarasi ambao wameendelea kusuasua aweze kuwasukuma ili waweze kuhakikisha kwamba umeme unafika katika vijiji vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wangu wa Katavi kuna maeneo mengi hasa upande ule wa Tanganyika, umeme haujaweza kufika katika maeneo ya vijiji na hapa nitataja baadhi ya vijiji vichache kikiwepo Kijiji cha Kabanga, Kijiji cha Mrabasi, Kijiji cha Mgasa, lakini Kijiji cha Katobo pamoja na Isobangala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati aweze kusaidia wakandarasi hawa ambao wanasuasua. Mkoa wa Katavi, tuliahidiwa upande wa Tanganyika kwamba mkandarasi angeweza kukamilisha mradi huu mwaka jana oktoba, lakini mpaka sasa mradi huu haujaweza kukamilika na mvua zinaponyesha zinaenda kukwamisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe sana, mkandarasi huyu aweze kusukumwa ili aweze kukamilisha mradi huu na wananchi waweze kupata umeme kwani umeme ndio chachu kubwa ya maendeleo kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakwenda kuchangia katika suala la matumizi ya gesi katika magari, suala la matumizi ya gesi katika magari, tulikwenda kufanya ziara mwezi Novemba katika nchi ya India, amezungumza Makamu Mwenyekiti wangu wa Kamati, nchi ya India imepiga hatua kwa kutumia gesi katika magari yao kwa asilimia kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi yetu suala hili limekwishaanza. Hata hivyo, nitumie nafasi hii hii kumuomba Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kuweza kusaidia na ku-*push* suala hili ili liweze kwenda vizuri kwa kujenga vituo vingi vya kuweza kuweka gesi kwenye gari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili likienda kufanyika vizuri nchini ni dhahiri kabisa katika sekta hii vijana wengi wamekwenda kupata ajira kwa kuendesha magari ya *Bolt*, *UBA* na mengineyo kwa kutumia gesi ambayo imekuwa ikipunguza sana gharama kubwa na kuwasaidia vijana waweze kuongeza pato lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika Wizara ya Madini. Nimpongeze sana Kaka yangu Antony Mavunde kwa namna anavyofanya kazi ya kuhakikisha kwamba Wizara ya Madini inakwenda kupiga hatua akiipokea kutoka pale alipoishia Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kaka yangu Doto Biteko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze pia kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuona umuhimu wa kuwasaidia kwa kuwapa vifaa wanawake wachimbaji wadogo wadogo. Kwa kweli Mama yetu, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ni mama mwenye huruma. Mwaka 2023 alitoa leseni kwa wanawake wachimbaji wadogo wadogo, lakini pia aliweza kutoa leseni kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kuona umuhimu wa wanawake hawa. Sote tunajua kwamba ukimsaidia mwanamke umeisaidia familia kwa kiasi kikubwa kwani wanawake wengi ndiyo wamekuwa wakibeba majukumu ya familia. Kwa hiyo ninampongeza sana

Mheshimiwa Rais wangu kwa kuwasaidia akina mama hawa wachimbaji wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nichangie kwenye suala la Madini. Ninaiomba sana Serikali, ili tuweze kuwa na tija katika suala la madini ni dhahiri kabisa ni lazima tuwekeze pesa nyingi katika kufanya utafiti. Wachimbaji wengi nchini wamekuwa wakichimba kiholela pasipo ufanyaji wa utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe sana Serikali kuendelea kutenga bajeti katika eneo hili la utafiti. Tukifanya utafiti tutawawezesha wachimbaji kutokutumia gharama kubwa; wanakwenda kuchimba pasipo kuwa na tafiti na matokeo yake wamekuwa wakipata hasara. Hivyo, Serikali tukiwekeza pesa nyingi katika tafiti itawasaidia wachimbaji hawa waweze kunufaika na wasiweze kupoteza nguvu kazi pamoja na pesa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie kuhusu suala la fidia kwa wananchi. Ningeomba sana wananchi waweze kulipwa fidia zao kwa wakati. Wananchi ambao wanapisha maeneo ambayo yameonekana kuwepo kwa madini wamekuwa wakisumbuliwa na hawalipwi pesa zao kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe sana Serikali, na tuna imani kubwa sana na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu wetu, kwamba atakwenda kusimamia suala hili. Wale wananchi wote ambao wamepisha maeneo yao kwa sababu yameonekana kuwa na madini; aweze kuwasimamia wale wanaohusika kuwalipa ili waweze kulipwa kwa wakati na wenyewe waweze kuendelea na shughuli nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi. Niendelee sana kuwapongeza Wizara ya Nishati lakini pia Wizara ya Madini kwa jinsi ambavyo wameendelea kufanya kazi vizuri na sisi Wanakamati tutahakikisha kwamba tunakwenda kuishauri vizuri Serikali na shughuli zinakwenda kufanyika katika taifa letu. Ahsante sana nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Tarimo anapenda kuwatambulisha wageni wake; Ndugu Romana Olomi, Mkurugenzi *NGO* ya *Miinjeni Women Organization* na Ndugu Edward Tesha, Afisa Mipango.

Haya, tunaendelea. Mheshimiwa Regina Ndege, jiandae Mheshimiwa Ndaisaba, jiandae Mheshimiwa Kanyasu, jiandae Mheshimiwa Getere, jiandae Mheshimiwa Jesca.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia taarifa hii ya Kamati ya Nishati na Madini. Kwa kuanza kwanza nimpongeza sana Mheshimiwa Rais, Mama yetu mpendwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna anavyoendelea kufanya kazi na kupigania Taifa lake. Nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara ya Nishati inayoongozwa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Biteko, nimpongeze pia Waziri wa Madini Kaka yangu Antony Mavunde pamoja na wasaidizi wao kwa namna wanavyoendelea kufanya kazi kuhakikisha sekta hizi zinakwenda kuleta ufanisi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nianze kwa kuchangia Wizara ya Madini halafu nitamalizia na Wizara ya Nishati. Kwanza, nichukue nafasi hii kwa sisi wana Manyara na wana Simajiro kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa namna alivyoamua kuwekeza kwenye sekta ya madini. Mheshimiwa Rais alitenga bilioni 5.4 kwa ajili ya kujenga soko la kisasa katika Mji wa Mererani. Mpaka sasa bilioni 2.9 zimekwishatumika. Hata hivyo, niseme tu kwamba kwa sasa kazi ya ujenzi wa Soko la Mererani imesimama kutokana na kwamba fedha bado hazijafika. Kwa hiyo, niiombe Serikali sasa kupeleke fedha ili kazi ya biashara ya uuzaji wa madini ianze kufanyika katika Soko la Mererani.

Mheshimiwa Naibu Spika, soko lile la Mererani likishakamilika, kwanza tunauhakika kwamba wafanyabiashara wanakuwa na usalama wa kufanya biashara yao, vile vile, sambamba na hilo Serikali itakwenda kukusanya mapato kwa kiwango kikubwa. Kwa hiyo, niombe sasa Serikali ipeleke fedha ili lile soko lile la Mererani lianze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili wananchi waweze kuleta maendeleo katika maeneo yao ni lazima kuangalia afya yao. Ni kwamba, katika eneo lile la ukuta wa Mererani, wale wanaojishughulisha na uchimbaji wa madini hawana kabisa huduma ya afya ndani ya ule ukuta. Kwa hiyo, linapotokea tatizo la dharura wananchi hawa hawapati huduma ya kwanza katika maeneo yale. Kwa hiyo niiombe Serikali iangalie namna ya kwenda kujenga zahanati katika ukuta wa Mererani ili wananchi wanapopata changamoto yoyiote, waweze kupata huduma ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini eneo lote la Mererani kwa sasa hivi kuna *population* kubwa kulingana na biashara inayofanyika pale. Hata hivyo, cha kusikitisha ni kwamba tuna kituo kimoja cha afya pale kata ya Endiamutu. Kituo hicho kwa siku kinapokea wagonjwa 357. Hawa wagonjwa wanatoka maeneo mbalimbali. Si kwamba wanatoka Mererani peke yake, wapo wanaotoka Wilaya ya Hai kata za jirani lakini pia kuna wanaotoka Wilaya ya Arumeru. Hawa wote wanakwenda kupata huduma katika Kituo cha Afya cha Mererani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo linatokea ni kwamba, kituo kile kimezidiwa. Kwa hiyo, wagonjwa hawapati huduma na mwisho wa siku wagonjwa wanakimbizwa katika Hosipitali ya Rufaa kama Arumeru na kule tayari kumezidiwa. Kwa hiyo, nikumbushe ombi la Serikali kupitia Mkoa wetu wa Manyara kwamba, tunaomba sasa kujengewa hospitali katika eneo la Mererani ili kuona namna ya kuboresha na kutoa huduma za afya katika eneo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiboresha huduma ya afya ninaamini kabisa watu watafanya kazi na wataleta maendeleo. Kwa hiyo, niombe Serikali kuliangalia hilo ili kuona namna gani wananchi wanaweza wakapata huduma ya afya kirahisi badala ya kutembea umbali mrefu na wengine wanapoteza maisha wakati wakielekea kwenda kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, wachimbaji wetu wa madini wanafanya kazi, wanatumia gharama kubwa; lakini kuna gharama kubwa kwenye upatikanaji wa zana za kuchimba

madini hasa zana za kupiga baruti. Hii ni kwa sababu gharama ni kubwa na wanatozwa kodi. Kwa hiyo, mimi niiombe Serikali ione namna gani ya kuwapunguzia gharama wachimbazji madini kwa kupunguza kodi au kuondoa kodi kabisa kwenye zana za uchimbaji madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifanya hivyo kwa maana kwamba wachimaji wengi wa madini wanakata tamaa mwisho wa siku wanafirisika na kuacha biashara ya uchimbaji madini. Kwa hiyo, Serikali ione namna gani inaweza ikawapunguzia mzigo hasa wachimbaji wadogo wadogo ili waweze kujishughulisha na biashara hii ya madini ili waweze kujitegemea kukuza uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ni suala zima la umeme. Umeme wa migodini umekuwa wa gharama kubwa. Gharama hii ya umeme wa migodini ni sawa sawa na gharama iliyoko katika viwanda. Sasa, bei ya *unit* ya viwandani na bei ya *unit* ya migodini inafanana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji wa madini wa vito wanaweza wakachimba kwa muda mrefu bila mafanikio. Mtu anaweza akachimba kwa miaka 10 hajafanikiwa lakini mfanyabiashara wa kiwandani atafanya biashara yake, atazalisha *products* na atapeleka sokoni watu watanunua. Hata hivyo, huyu mchimbaji wa madini ataendelea kulipa umeme anaoutumia lakini hajazalisha. Kwa hiyo, Serikali iwaone na kuwaangalia wale wachimbaji wa madini ili kuangalia bei ya *unit* isifanane na ile ya viwandani. Wapunguziwe gharama za bei ya *unit* ili waweze kufanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ni suala linalohusiana na nishati. Kwanza, niipongeze sana Serikali asilimia kubwa ya vijiji vimepata umeme. Vile vile, mimi niishukuru Serikali yangu, Wilaya ya Babati sisi vijiji vyote 102 vyote tumepata umeme. Hata hivyo, niombe sasa vile vijiji ambavyo havijapata umeme usambazaji sasa uongezeke kasi ili vikapate umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna maeneo kama Wilaya za Simanjiro ambayo ni maeneo ya wafugaji, wananchi

hawajengi maeneo ya karibu karibu. Wengi wanakuwa katika *scattered areas* (wanatawanyika). Kwa hiyo, Serikali iangalie namna ya kuangalia wale wafugaji namna ya kuwafikishia umeme maana umeme unafika kwenye *center* ya vijiji; na hatimaye na vitongoji mwisho wa siku wale wafugaji wako maeneo ya mbalimbali na hawakai karibu kwa hiyo, inakuwa ni vigumu wao kufikishiwa umeme. Kwa kuwa dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kila nyumba inapata umeme. kwa hiyo niombe tu Serikali iangalie jiografia hasa ya maeneo ya wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa Wilaya ya Kiteto kuna vijiji ambavyo havina umeme kabisa. Kwa hiyo, niiombe Serikali iangalie namna ya kuwafikishia umeme kwa kuwa tunataka kila Mtanzania apate umeme. Tuna Kijiji cha Orkiush hakina umeme kabisa, Kijiji cha Orkitikit hakina umeme, lakini kuna Kijiji cha Makame na Kijiji cha katikati, vijiji hivi tayari nguzo zimefika ila watu hawajaunganishiwa umeme. Sasa niombe watu wa *TANESCO* wafanye kwa wepesi kuhakikisha umeme unawashwa kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuna miji midogo midogo inayotambulika kisheria. Miji hiyo inatambulika kisheria lakini hawapati zile huduma zinazofanana na miji. Niiombe Serikali iangalie namna ambavyo ile miji inaweza kupunguziwa gharama. Miji hiyo midogo midogo ambayo inatambulika kisheria, wanakuwa wanatozwa umeme sawa sawa na sehemu za mijini ilhali miji hiyo haina hadhi ya kuitwa miji midogo. Huduma nyingine za miji hawapati na hivyo, inawalazimu wananchi wanaingia gharama kubwa lakini wanaishi katika sura ya vijijini. Kwa hiyo, niombe sana Serikali ipitie upya ile miji midogo kuangalia namna ya kuipunguzia gharama ya umeme. Badala ya kulipa 320,000 waweze kulipa na kuunganisha umeme kwa shilingi 27,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Kiteto kuna maeneo kama Matui, Bwawani na Chapakazi, lakini tuna eneo la Magungu ambalo umeme unaunganishwa shilingi 320,000 badala ya shilingi 27000. Kwa hiyo, niombe sasa maeneo haya yazingatiwe ili wananchi wapate unafuu na waweze kuunganishiwa umeme katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niendelee kuishukuru sana Serikali yetu inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan. Sisi wananchi tunasema Mama anachapa kazi na tunaendelea kumuunga mkono, na aendelee kusonga mbele na tukijua kwamba atatufikisha pale ambapo hata roho yake inataka atufikishe. Kwa hiyo, Mama Samia Mwenyezi Mungu ambariki sana lakini na wasaidizi wake wote tunawatakia kila la kheri. Pia niseme kwamba naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ndaisaba, jiandae Mheshimiwa Kanyasu, jiandae Mheshimiwa Getere, jiandae Mheshimiwa Jesca.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchagia kwenye taarifa…

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa kwa Mamlaka ya Kiti naongeza muda mpaka tutakapomaliza shughuli yetu.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante sana. kwanza, mimi nipende kuanza kwa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Ngara, kwa kuendelea kuwa na imani kubwa sana na mimi katika kazi yangu hii ya uwakilishi. Vile vile, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya zawadi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Kipenzi cha Watanzania, Mama ambaye amekwishajipambanua kwa kuonyesha dhamira thabiti kabisa ya kuhakikisha kwamba anawasaidia Watanzania kuondokana na matatizo ya aina mbalimbali. Kwa kweli sisi Watanzania Mama Samia tumemuelewa. Vilevile, zawadi kubwa ambayo sisi Watanzania tunaweza tukampa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni kuhakikisha kama ule wakati utakapokuwa umefika tunampa kura nyingi za kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania hawawezi kuchagua watu wanaoshinda wanaandamana barabarani. Watu wanashinda wanavuruga vuruga barabarani huko hawawezi kuwachagua. Kwa kweli sisi Watanzania tumemuelewa Rais wetu,

tumemuelewa Mama Samia; na kwa mfano kwenye Wizara hizi mbili Wizara ya Madini na Wizara ya Nishati mama yetu ametoa kipaumbele, ameleta fedha nyingi sana. Miradi mingi inatekelezwa na Watanzania sasa wamewezeshwa kuweza kufanya kazi kwenye madini. Kwa kweli dhamira ya Mheshimiwa Rais tunaiona, tunamuunga mkono na zawadi yake tumeanza kufungasha kwenye maboksi, tunasubiri wakati ufike, na hilo halina ubishi. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nataka sasa nielekeze mchango wangu kwenye eneo la kucheleweshwa kwa miradi ya *REA;* hawa watu wakandarasi wa *REA* katika maeneo mbalimbali nchini wamekuwa wakichelewesha kukamilisha hii Miradi ya *REA*. Mathalani kwa upande wa Kagera, mkandarasi aliyepewa kazi ya kuhakikisha anajenga miradi ya *REA* Mkoa wa Kagera amekuwa akisuasua na kuchelewa kukamilisha miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Ngara; Mkandarasi huyu ambae yupo Kagera amekuwa akitusumbua. Pia, mimi nafikiri kwa kweli *TANESCO* na Wizara ya Nishati chini ya Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, sidhani nao kama wataingia kwenye mkumbo wa kuzoea matatizo badala ya kuona matatizo kama ni kitu kibaya. Sidhani kama watayazoea, kwa sababu, wakandarasi maeneo mbalimbali wananchelewesha kukamilisha miradi na hili ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Eneo la Burengo na Kagali, mkandarasi anasubiri kuona ni kiongozi gani mkubwa anakwenda kwenye eneo hilo na siku hiyo mkandarasi atakwenda kuwasha umeme kwenye transfoma. Kuwaka umeme kwenye transfoma haimaanishi umeme umewaka kwenye Kijiji, haimaanishi umeme umefika shuleni, haimaanishi umeme umefika kwenye zahanati. Tunataka tunaposema umeme umefika kwenye kijiji tuone wananchi wamepata umeme na taasisi zilizoko pale zimepata umeme. Sasa mkandarasi anasema amewasha umeme kwenye vijiji vya Burengo na Kagali lakini anakwambia umeme uko kwenye transfoma, hilo ni tatizo. Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, tunaomba umeme usiishie kuwashwa kwenye transfoma. Umeme uwashwe uende kwenye taasisi za

Serikali na uende kwa wananchi. Mathalani kata za Keza, Mganza, Bugarama na Kibogora. Kata zote hizi bado mkanadarasi hajakamilisha kupeleka umeme maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niombe Wizara ya Nishati, *TANESCO* na *REA* wasimamieni hawa wakandarasi, pengine wana matatizo ambayo ni *systemic*, matatizo yanayosababisha washindwe ku-*deliver* kazi zao. Wasaidieni kupata *letter of credit* kama hawana fedha, wasaidieni hawa wakandarasi ndugu zanguni waweze kukamilisha miradi ya *REA*. Sisi tumechoka kuona mnawaongezea muda kila mara mna-*renew* mikataba. Tunataka *REA* ajenge mikataba yake na iweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, anavyoshindwa kukamilisha miradi hii anachelewesha wananchi kupata huduma za umeme. Vilevile, anasababisha ongezeko la gharama kwa sababu vifaa vinaongezeka kupanda bei na mambo mengine. Hata hivyo, anasababisha sisi tuliotoa ahadi za kuhakikisha umeme unawaka kwenye hayo maeneo ahadi zetu zinachelewa kutimia pamoja na Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Sasa, niwaombe, naomba mumsimamie huyu mkandarasi ambaye yuko Kagera. Sisi tumechoka kuendelea kuona anachelewesha kukamilisha miradi ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine, alipokuja Waziri wa Nishati ndugu yangu January Makamba wakati huo, tulimwomba atusaidie kupata umeme kwenye mitaa nane ya mamlaka ya Mji mdogo wa Rulenge. Ndugu yangu Makamba aliahidi kwamba ndani ya mwaka mmoja utafanyika utaratibu tuweze kuipata mkandarasi aanze kupeleka umeme kwenye ile mitaa nane ya mamlaka ya Mji mdogo wa Rulenge, hata hivyo mpaka sasa hivi hakuna kitu kilichofanyika. Sasa niwaombe ndugu zangu Wizara ya Nishati, *TANESCO* pamoja na *REA*, Waziri anaposimama akaahidi, mnaposhindwa kutekeleza ndani ya muda mrefu mnamaanisha nini? Niwaombe tuleteeni mkandarasi mwingine aweze kupeleka umeme kwenye mitaa ya Mamlaka ya Mji mdogo Rulenge.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kusuasua kwa kukamilika kwa ujenzi wa Bwawa la

Kufua Umeme la Rusumo.  Huu mradi wa kufua umeme wa Rusumo ulitakiwa uwe umekamilika mwaka jana, na matarajio yetu ni kwamba mwezi wa kumi na mbili mwaka jana Marais wa nchi tatu wangekuja kuzindua ule mradi. Hata hivyo, ziko taarifa inawezekana ni hujuma, inawezekana ni uzembe, inawezekana ni figisu figisu; katika kufunga *turbine* moja walisahau vyuma ndani kama vile ambavyo mtu anaweza kafanyiwa operation wakasahau visu kwenye mwili au viwembe. Matokeo yake walivyoacha vile vifaa mle ndani kwenye t*urbine* moja walivyoiwasha ilivyoanza kuzunguka vile vitu vilivyosahalika mle ndani vikasababisha kuchanachana kwa *turbine* moja matokeo yake ile *turbine* imechelewa kufanya kazi na mpaka sasa hivi inafanya kazi *turbine* moja na pengine ndiyo maana mradi huu umechelewa kuja kufunguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika,  ninaiomba Wizara ya Nishati fuatilieni kama ni hujuma zimefanyika muwashughulikie watu, lakini ninaomba mfuatilie kwa sababu mkandarasi bado yupo katika kipindi chake anatekeleza ule mradi aondoe hizo *nut* zilizoko mle kwenye *turbine* kama kuna vitu vilichanikachanika avitoe aweke vingine, tunataka kusikia zile *turbine* zote zinazunguka na umeme unawaka ili sisi wananchi wa Mkoa wa Kagera ambao tumeendelea kuwa na umeme wenye nguvu ndogo tuondokane na adha hiyo, hilo ninaomba liweze kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na fidia eneo hilo la Rusumo *lane* ya kutoka Rusumo kwenda Gitega – Burundi, wananchi walidai fidia kwa muda mrefu sana. Kabla sijawa Mbunge nilikuta watu wanadai zaidi ya miaka sita nilivyofika pale nilipambana wananchi wengi wakalipwa ndani ya miezi mitatu, namshukuru Mungu kwa ajili hilo lakini nawashukuru na *TANESCO* na wengine walioshiriki kuhakikisha fidia zinalipwa, lakini kuna huyu mfanyakazi wa *TANESCO* anaitwa Agnes Masanja anasumbua wananchi wangu 10 ambao walikuwa na *dispute* kwenye malipo yao. Huwezi amini tokea mwaka 2021 Agnes Masanja, mfanyakazi wa *TANESCO* anawasumbua wananchi wangu kumi wanaodai fidia kati ya wananchi wengi na fidia zao zilikuwa na *dispute*. Mambo haya sikutarajia mimi kwamba ingechukua muda mrefu

sana wananchi wangu kumi kuweza kuwa wamelipwa fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunapojadili taarifa ya Kamati yetu tunapokuwa tunakwenda huko kukagua utekelezaji wa mambo yaliyofanyika huko, tunakutana na mambo haya na kwa kweli nafikiri Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko umenielewa nilipomtaja huyu mtu, nilivyosema wananchi wangu hawa kumi ambao wanadai fidia, naomba uweze kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kusuasua kwa ulipwaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha uchimbaji wa madini kwenye migodi mikubwa hapa nchini, mathalani kwa mgodi wangu ambao upo kwenye Jimbo la Ngara mgodi wa Tembo *Nickel.* Tulipowatembelea kwa mara ya mwisho pale *Tembo Nickel* tuliwapongeza wamejitahidi wamepambana kwa muda mfupi kazi inaonekana lakini tuliwaambia wananchi wangu walikuwa wanataka waipate hela wakati wanakula Sikukuu ya *Christmas* hela zao za fidia wawe wamezipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninwashukuru *Tembo Nickel* wamejitahidi wameweza kulipa bilioni tisa, lakini kati ya wananchi zaidi ya 1,100 wanaodai ni wananchi 400 tu ambao wamelipwa fidia na *Tembo Nickel* na nimuombe Waziri wa madini wasimamie vizuri Tembo *Nickel.* Juzi tumesikia kuna *retrenchment* watu wengi wameacha kazi pale wameachishwa kazi hatujui ni nini kinaendelea pale *Tembo Nickel*. Ndugu yangu Waziri wa Madini matarajio yangu ni kwamba watu zaidi ya 700 waliobaki mpaka dakika hii walitakiwa kuwa tayari wamekwishalipwa fidia yao. Mathalani kuna wananchi wanadai hela nyingi sana kama ndugu yangu Mathias yupo wa Kabanga, Askofu Simon Lumito, hawa watu wamekuwa wakidai muda mrefu sana, wanadai fedha zao *Tembo Nickel* inachelewesha kulipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba wananchi 700 ambao wanadai fidia Tembo *Nickel,* Wizara ya Madini mkasimamie vizuri ndugu yangu Mavunde kaa sawasawa, wasimamie hawa wananchi 700 waweze kulipwa fidia. Fedha hizi sisi Wananchi wa Ngara tunazitaka zinapolipwa kwa wananchi wetu zinarudisha

uchumi, zinasababisha mzunguko uongezeke lakini zinafanya wananchi wa Jimbo la Ngara waweze kutumia fedha hizo kuziwekeza kwenye kujiendeleza. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Ndaisaba kengele ya pili.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninashukuru sana, nauonga mkono hoja ila naomba wananchi walipwe.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu, ajiandae Mheshimiwa Getere, ajiandae Mheshimiwa Jesca.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nami naomba nianze kwa kumpongeza Mwenyekiti kwa taarifa yake lakini pia kuwapongeza Mawaziri wote wawili Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati na Mheshimiwa Waziri wa Madini. Nitumie nafasi hii kumpongeza Rais kwa kazi nzuri inayoendelea kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere kwa mujibu wa taarifa Bwawa limefikia asilimia 95, majaribio yote muhimu yamefanyika. Kwa hiyo ni matarajio ya Watanzania kwamba hiki kilio ambacho kinaendelea sasa hivi nchini cha upungufu wa umeme kinaweza kuja kupata majibu hivi karibuni. Kwa hiyo tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kwenye maeneo machache lakini nitaanza na gesi. Hivi karibuni Serikali ilileta ruzuku na mkatugawia baadhi ya mitungi ya gesi kwenda vijijini, tunawashukuru sana kwa sababu tumeona tumetoa ingawa ni michache lakini wale tuliowapa wameshukuru sana. Shida kubwa ambayo naiomba Serikali ijue kwamba tumegawia watu mitungi ya gesi wanaokaa kilometa 30, 40 kutoka mitungi inakouzwa, maana yake ni kwamba huu mtungi unapoisha gharama ya kuiendea gesi na kurudi ni karibu shilingi 20,000, ninachokiona mbele ni kwamba watu wote watakaomaliza kutumia mitungi tuliyowapa watakwenda kuitunza ndani au watakwenda kuwauzia madalali wanaouza ile mitungi ya gesi.

Sasa nikuombe Mheshimiwa Waziri uweke mifumo ambao itasababisha gesi hii ipatikane mpaka kwenye *level* ya chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kwenye eneo hilo ni vizuri sana tukaangalia tuwe na *long-term plan,* kama tumeweza ku-*subsidize* tukagawa mitungi mnaonaje kama tunge-*subsidize* tukashusha kabisa bei ya mitungi hiyo na bei ya gesi yenyewe badala ya 23,000 ikawa shilingi 10,000 ili kila mwananchi ambaye alikuwa anapikia kuni aache kupikia kuni. Maana sasa hivi namna ilivyo gharama kwa mwananchi ambaye yuko kijijini akinunua 23,000 jumlisha nauli ya kuifuata ni karibu 30,000, huyu mtu atarudi kwenye mkaa, atarudi kwenye kuni. Kwa hiyo, uwekwe utaratibu ambao utakuwa ni wa muda mrefu utakaotuondoa kwenye uharibifu wa misitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la pili ni kwenye Wizara ya Madini. Geita tumekuwa na tatizo la vigingi, namshukuru sana Mheshimiwa Musukuma amezungumza kidogo nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu nilisema jana na Mheshimiwa Waziri wa Madini, tumeanza kuzungumza kuhusu ulipaji wa fidia kwa Wananchi wa Samina, lakini bado tumekwama kwenye maeneo ya Nyakabale na mitaa mingine karibu minane na shida kubwa hapo ni mgongano wa kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilipouliza swali jibu nililojibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba waridhiane wanaodai fidia pamoja na mgodi jambo ambalo haliwezekani. Huwezi ukawaambia watu wanaodai fidia waende waridhiane na mtu wanaemdai haiwezekani! Kama sheria zetu za madini zinampa haki mtu mwenye leseni kumiliki madini chini na akazuia walioko juu wasifanye maendelezo lakini sheria zilezile zinampa haki mtu mwenye ardhi juu asiondolewe mpaka alipwe fidia, maana yake tuna tatizo kwenye sheria! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotakiwa kufanyika pale ni aidha tupitie upya sheria mapema au katika maeneo yenye migogoro kama hiyo huu mgongano wa kisheria kwa sababu ni wa Kiserikali, Serikali iwalipe wale wananchi halafu yenyewe ianze

kuhangaika na yule mwekezaji, bila kufanya hivyo wananchi wanaoishi kwenye maeneo haya wanateseka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulianza mgogoro Nyakabale pakiwa na watu 500 leo pana watu takribani 10,000 watu ambao ili afike hospitali anatembea kilomita 50, kilomita 25 kwenda 25 kurudi, lakini njia yao ya asili ni kilomita nne iliyofungwa na watu wa mgodi. Sasa mazungumzo kama tunavyosema tumesikiliza sana, tunamshukuru Mheshimiwa Waziri amefanya kazi kubwa lakini tunakoelekea kama inashindikana kupata *solution* sisi tutavunja yale mageti, tutapita pale katikati turuhusu wananchi wetu wapite, kwa sababu hatuwezi kufika pahala miaka 30 tunazungumza jambo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kwenye eneo hilo ni kwamba tunapitisha kanuni za *CSR*, mimi namkushukuru sana Mheshimiwa Waziri kanuni ni nzuri, shida iko sehemu moja tu tatizo anayetenga fedha ya *CSR* anapofanya yeye manunuzi halafu Halmashauri wawe wasimamizi, halafu inapotokea tatizo kwamba yule Mzabuni aliyepewa ameshindwa kukidhi viwango, Halmashauri ndiyo itapata hati chafu! Hivi kwa nini asitenge fedha akawakabidhi Halmashauri wafanye manunuzi yeye alipe kwa sababu *ownership* haipo kwenye kulipa peke yake, yeye alipe ili Halmashauri wawajibike na *quality* ya mradi unaoendelea. Kwa hiyo, tunaomba maeneo hayo yafanyiwe marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipongeza kuhusu mradi wa Mwalimu Nyerere, mimi naipongeza sana Serikali na hivi karibuni imesema itaongeza *megawatt* 470, bado naliona tatizo Mheshimiwa Waziri. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais nimpongeze alifanya mabadiliko *TANESCO* lakini matatizo bado yanaendelea. Mimi nadhani iko haja ya kufanya *cross section* kabisa ya hilo Shirika zima kuangalia huko ndani kuna nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kisingizio huko nyuma ilikuwa maji hakuna kwenye mabwawa, Mungu kaleta mvua za ajabu sasa kisingizio kingine ni mitambo haifanyi kazi! *okay fine* mitambo itapona, ninachokiona sasa Mheshimiwa Waziri, sasa hivi uzalishaji ni megawati 1,200; *storage capacity* ni 1,800, Mwalimu Nyerere

itaingiza 2,000 tutakuwa na takribani 4,000. Ukiangalia historia ya sasa *storage capacity* ni 1,800 unaozalishwa ni 1,200 kama asilimia 63, ukichuua historia hiyohiyo ukaipeleka kwa Mwalimu Nyerere maana yake tutakuwa na *almost* 1,400 ndiyo zitakuwa zinakuwa *produced* kwa siku, tutakuwa na *megawatt* 2,600.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vyote vikipata umeme vitongoji vyote vikapata umeme, umeme tutakaokuwa nao utatutosha kwa miezi sita peke yake au mwaka mmoja, kwa nini? Kwa sababu ninadhani kuna haja ya kuangalia vizuri wataalamu wetu huko ndani. Pale ambapo kuna sababu *genuine* tunawakubalia lakini pale ambapo tunaona kabisa kwamba hata juhudi za Serikali zinazofanyika haziwezi kuzaa matunda iko haja ya Mheshimiwa Waziri kutazama upya. Mmetuletea sawa Mkurugenzi mpya yule Ndugu Kisimba lakini inawezekana wanaomuangusha bado wapo palepale kule chini ndiyo ambao hawatimizi wajibu wao, hili lisipofanyika Mheshimiwa Waziri tutaendelea kulalamikia umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho tuna vyanzo vingi sana vya umeme, wenzangu wamezungumza kuhusu *geothermal* lakini tuna umeme wa jua, tuna vyanzo vingine vya tungamo taka, tuna maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu hapa Tanzania ikiendelea kwa mfano, sehemu kubwa yetu ya umeme sasa hivi ilikuwa ni gesi na gesi takribani *megawatt* 1,100 sasa hivi tunaambiwa mgandamizo wa gesi umepungua, maana yake ni kwamba tukiendelea kutegemea umeme wa Nyerere na hivi vyanzo vingine vilivyopo huko tunakokwenda kadri mahitaji yetu yanavyozidi kuwa makubwa bila kufanya *diversification,* ipo siku tutajikuta *grid* imekatika lakini kule tunakotegemea kutoa umeme umeme hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri tuende kwenye vyanzo vyote vya umeme, kuna umeme wa makaa ya mawe tutafute watu wafanye kwa *PPP,* kuna umeme wa joto ardhi tutafute watu wafanye, tumepitisha juzi hapa tumesaini Mkataba wa *IRENA*, huu mkataba tuweke *speed* ili uweze kutusaidia, lakini kuna umeme wa gesi ambao

tunaendelea nao na wenyewe tuendelee kuwekeza, maana yake moja ya malalamiko yaliyoko kule ni kwamba hatuna uwekezaji mpya mwingine uliofanyika kwa takribani miaka karibu 20 kwenye joto ambalo linazalisha umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii maana yake nini? Maana yake ni kwamba tunaongeza idadi ya watumiaji wa umeme tunafikiria sana Mwalimu Nyerere ambayo kwa hesabu zinavyoonekana itaweza kusaidia kwenye soko kwa muda mfupi sana, maoni yangu ni kwamba nchi hii ni kubwa maeneo *potential* ya ku-*invest* ni mengi tukuombe tu Mheshimiwa Waziri kama inawezekana wakaribishwe wawekezaji binafsi ili waweze kusaidia nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni *TANOIL*, nilikuwa nasoma taarifa ya *TANOIL* hapa na kwa kweli inasikitisha kidogo, hawa walianza na mtaji wa bilioni karibu 110 na wameendelea kufanya kazi na *almos*t sasa hivi wana bilioni 26, ukija kwenye...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa kengele ya pili hiyo.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie jambo moja tu.

**NAIBU SPIKA:** Sekunde mbili.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kwenye sababu za kwa nini wanafikiri wameshindwa kuendelea wanasema kwenye taarifa yao ushindani usio sawa katika soko uliosababishwa na ukiukwaji wa taratibu za kibiashara unaofanywa na baadhi ya washiriki kwenye soko. Maana yake ni nini? *TANOIL* ni Shirika la Serikali, umemdumbukiza kwenye ushindani na mashirika ya watu binafsi, yaani ile *advantage* ya kuwa Shirika la Serikali hana, anakwenda kupambana kufukuzia zabuni na mashirika ambayo yana pesa yanakuhonga, yanakufanya nini, wanacheza naye biashara. Huyu mtu ata-*collapse* kama tunataka a-*survive* tumtengenezee *threshold*, kwamba hii *threshold* ya *ten percent* tunakupa *TANOIL* halafu

huyu a-*syndicate* na watu wenye makampuni makubwa apate pesa aweze kuingia kwenye ushindani kama Shirika la Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere, ajiandae Mheshimiwa Jesca Kishoa.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia hizi Kamati mbili, Kamati ya Madini na Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anazozifanya za kuendeleza miradi mikubwa ya kimkakati, Bwawa la Mwalimu Nyerere, Reli, Busisi na maeneo mengine, nampongeza sana

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka kuliangalia hili la Mheshimiwa Rais na Wabunge wote hasa kila Mbunge anaposema namuunga mkono, namuunga mkono, sasa tukubaliane humu ndani unamuunga mkono kwa sura mbili. Sura ya kwanza ni kama Mbunge, maana yake ukiteuliwa kugombea 2025 utamuunga mkono, sura ya pili ni pale ambapo wewe kama Boniphace ambapo huko mbele ukipigwa chini maana yake hukuteuliwa uendelee kumuunga mkono. Kwa hiyo nafikiri kwamba tuunge mkono kwa sura zote mbili, sura ya kuja humu kama Mbunge na sura ya kubaki kama jina lako, hilo ninaendelea kuwaambia Wabunge tumuunge mkono kwa njia hiyo yote, tusiwe tunasema tu Wabunge kwa sababu umeteuliwa tu hata usipoteuliwa ingia kazini umuunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi yangu machache tu kwanza nimpongeze...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lucy uko salama hapo? Mheshimiwa endelea *(Kicheko)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nilikuwa naomba nichangie mambo matatu ama manne hivi. Jambo la kwanza kuweka umeme katika maeneo ya

machimbo. Katika Jimbo langu la Bunda kuna eneo linaitwa Nyabuzume na kuna mgodi unaitwa Nyaburundu kuna kampuni imeteuliwa pale kwenda kufanya hiyo kazi na kampuni imeshapewa fedha inaitwa *O.K Company,* ambayo tayari imesaini mkataba lakini mpaka leo inaenda mwezi wa pili mwezi wa tatu haijaenda kufanya hiyo kazi. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri na maeneo yanayohusika waiambie hiyo kampuni inayohusika Mama Samia ameshawapa fedha waende wakatekeleze Mradi wa Nyabuzume na Mradi wa Nyaburundu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili nilikuwa nazungumza tatizo liko Bunda sasa. Kituo cha kupozea umeme Bunda kimeharibika na *transformer* yake imeharibika inaitwa Kinga *transformer*. Sasa ni miezi miwili Wananchi wa Bunda wanateseka hawana umeme, hiyo *transformer* imeonekana kwamba akiba yake iko Musoma lakini kutoka Musoma kuileta hapa Bunda imechukua miezi miwili sasa, wanasema wanatengeneza barabara ya kuichukua *transformer,* sasa ni miezi miwili. Naomba wanaohusika wasitese watu wa Bunda, waende wachukue hiyo *transformer* ije Bunda ifanyekazi ili watu wa Bunda wasiteseke na umeme unaokatika kila mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna umeme wa vijijini, umeme wa vijijini tunaahidiwa hapa umeme wa vitongoji 15 na Wabunge wote tuliahidiwa, lakini ukienda kuna wao unakuta ni *REA II C* umeme wa kawaida, ule umeme wa vijiji 15 haujaonekana uko wapi. Sasa naomba tuambiwe kwamba huu umeme upo au haupo ili tuweze kujua kwa sababu tulipeleka taarifa kwamba kuna umeme wa vitongoji 15 ambao Wabunge tayari tulipewa, ili tuwaambie wananchi kwamba umeme huo uko sehemu gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la gesi limezungumzwa na Wabunge wengi sana hapa, nilikuwa nafikiri kwamba ni muda muafaka sasa Serikali iweke ruzuku kwenye makampuni ya gesi ili gesi yote ishuke bei na wananchi watumie gesi badala ya kuni na mkaa. Kwa hiyo, hili ni jambo la muhimu sana kupunguza kwa kuweka ruzuku au kupunguza bei ya ruzuku au bajeti inayokuja

muangalie namna gani mnapunguza ruzuku ya gesi ili wananchi waweze kupata huduma hii kwa urahisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nazungumza habari ya bwawa la Mwalimu Nyerere na bwawa la Mtera najiuliza maswali mengi sana, kama Mtera ina *megawatt* 80 na umeme mdogo sana ukilinganisha na bwawa la Mwalimu Nyerere 2,115, sasa najiuliza kama *condition* ya Mtera maji hayapatikani leo mvua zinanyesha kila mahali maji hayapatikani, je huo tunakokwenda huko kwa bwawa la Nyerere itakuwaje? Huko mbele itakuwaje? Kwa hiyo, niombe mkakati utakaotumika kuweka maji ya bwawa la Mwalimu Nyerere usiwe tena mkakati wa Bwawa la Mtera, kwa sababu vinginevyo hivi vyanzo vya maji vitakuwa vinatuletea shida sana kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushukuru naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Jesca Kishoa.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini kwa wasilisho lake zuri pia kwa uongozi wake kwenye Kamati yetu, anatuongoza vizuri yeye pamoja na Makamu Mwenyekiti pia Makatibu wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitajikita hasa kwenye eneo la ubovu wa mitambo. Wizara ilizungumza na Kamati na ikaeleza kwa ufasaha sana kuhusiana na sababu zinazopelekea umeme kuwa mdogo au umeme kukatika katika. Moja ya sababu kubwa waliyoitaja walisema ni ubovu wa mitambo kwa maana ya kwamba hakuna *maintenance* kwenye mitambo ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua yapo madhara makubwa sana yanayotokana na mitambo kutofanyiwa *maintenance;* madhara ya kwanza, kwanza lazima kutakuwa kuna upungufu wa umeme kwa sababu mashine zinazalisha kwa kiwango cha chini; madhara ya pili, gharama za kutengeneza mitambo

zinakuwa kubwa kwa sababu *maintenance* zinakuwa hazifanyiki mara kwa mara; madhara ya tatu ni usalama mdogo wa wale wafanyakazi wa mitambo hiyo, wanakuwa wana-*risk* sana maisha yao kufanyakazi kwenye mitambo ambayo haifanyiwi *maintenance;* na madhara mengine ambayo ni ya nje au ya mbali ni inafukuza wawekezaji, hakuna mwekezaji ambaye anaweza kupenda kuwekeza kwenye nchi ambayo umeme wake ni wa kusuasua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, madhara mengine ni kikwazo kwa wananchi na inaharibu hata siasa za nchi. Hivyo *maintenance* ya mitambo ya umeme ni jambo muhimu kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwamba Serikali imetenga fedha shilingi bilioni 838 kwa ajili ya kufanya marekebisho kwenye mitambo ya umeme, lakini pamoja na kwamba hii ni hatua kubwa, lakini inaweza ikawa siyo mwarobaini kwa sababu kama hakutokuwa na *consistency* kwenye *maintenance* ya mitambo yetu bado tutakuwa na changamoto ya upungufu wa umeme hata kama mabwawa yakajaa maji ya kutosha, kama hakuna *maintenance* ya uhakika tutaendelea kuwa na changamoto ya umeme; hata kama tunazungumza leo *energy mixing* kama ndio mwarobaini wa umeme wa uhakika, kama mitambo ya kuzalisha umeme bado itakuwa ina changamoto, hatutakuwa na umeme wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Julius Nyerere ambayo imeonekana kama ndio mwarobaini pekee kwa sasa. Nataka nikwambie hata kama Mwalimu Nyerere lipo, kama mitambo ya uzalishaji haitafanyiwa *maintenance* hatutakwenda popote. *Maintenance* ni muhimu sana kwenye mitambo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huwa najiuliza Kidatu mfano ambayo inazalisha takribani megawati 200 na kitu; toka mwaka 1975 lilipoanzishwa imefanyiwa *maintenance* mara mbili tu; mara ya kwanza 1994, mara ya pili mwaka 2003. Ukienda Kihansi kuna changamoto ya kufanyiwa *maintenance* kwa wakati, Mtera hivyo hivo megawati 80 pale, mashine mpaka sasa hivi ndio wanazungumza kufanya *maintenance* kwenye *turbine* moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali, duniani kote *maintenance* zinafanyika za aina nyingi, lakini zote zina-*fall to two categories;* ya kwanza inaitwa *preventive maintenance*, wengine wanaita ni *predictive maintenance* na nyingine inaitwa *collective maintenance*, wengine wanaita *reactive maintenance*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *preventive maintenance* ni pale unapofanya *maintenance* ya mitambo ya umeme wakati bado hakuna hitalafu yoyote imetokea. Mfano rahisi ni kama gari unalotumia, unajua kabisa kwamba kuna wakati wa kuifanyia *services* kabla hujaona hitilafu yoyote, lakini sisi tuna *apply corrective maintenance* ambayo yenyewe ni baada ya changamoto kutokea. Ni sawasawa na mtu mwenye gari ambayo gari lake lina tairi upara, lakini anasema mpaka lipasuke akiwa barabarani ndio alifanyie marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna umuhimu mkubwa, nashauri Serikali wawekeze zaidi kufanya *preventive maintenance* au *predictive maintenance* kwa aili ya kuondoa kabisa changamoto ya kuwa na ukosefu wa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mwingine nataka kuipa Serikali ni kwamba wakatenge fedha za kutosha kila wakati wahusika wanapokuwa wanahitaji fedha kwa ajili ya *maintenance* Serikali iwapatie fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumaliza wote tunatambua kwamba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameonesha dhamira ya dhati kabisa ya kuhakikisha kwamba ameondoa changamoto ya umeme na kwa kusema hivyo yapo mambo kadhaa ambayo yamedhibitisha hilo. Hakuna asiyejua hapa ya kwamba Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alipokea kijiti cha uongozi kipindi ambacho nchi ilikuwa inapitia matatizo magumu ya kuondokewa na mtangulizi wake, lakini Rais alisimama imara akasema tutavuka. Baada ya hapo tunajua mtangulizi wake alikuwa ameanzisha miradi mikubwa, mizuri na ya kimkakati

ambayo mingi ilikuwa ndio imeanza, mmojawapo ulikuwa ni Mradi wa Julius Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama hapa nikisikia fahari moyoni mwangu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan amekuta mradi huo ukiwa na asilimia 37 tu na leo tunazungumza asilimia 95 ndani ya Bunge. Leo hii humu ndani nikimpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan mtasema huyu Mbunge anajizima *data* au ni *5G*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *data* hazidanganyi, mifano iko mingi, sasa hivi tuna uwezo wa kufanya biashara kubwa sana na wenzetu hata kusafirisha mafuta kwa njia rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Daraja la Busisi; daraja ambalo ni kubwa Afrika nzima linashika nafasi ya sita *East Africa* nzima hakuna na la kati hapa. Daraja hili limetumia zaidi ya shilingi bilioni 700 za Serikali, lina ukubwa wa kilometa zaidi ya tatu. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameingia madarakani amelikuta daraja hili lina asilimia 25 tu, leo nilimsikia mkwe mwenzangu Mheshimiwa Bashungwa akiwa anamjibu Katibu wa Itikadi na Uenezi, Paul Makonda kwamba daraja lile sasa kutoka asilimia 25 sasa hivi lipo asilimia zaidi ya 80. Sasa mtu huyu, Rais wetu huyu tukimpongeza tutaonekana tunajizima *data* au tuko *5G*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kusisitiza kwamba kwa kweli tunafurahia sana kuona kwamba miradi mikubwa na ya kimkakati inaendelea kufanyika vizuri na tunaona sasa hivi mpaka tumeanza kuingia na tunatunishiana vifua na wenzetu kwenye suala … mzigo…

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam kaa chini, usitutoe utamu kaa chini. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia ni kwamba kweli tunafurahia sana kuona jitihada zinazoendelea kufanyika na Serikali hii kwa kuendeleza miradi. Sisi

tunajua duniani huko mara nyingi Marais wanaokuja kuchukua awamu zinazofuata huwa hawapendi kufanya yale ambayo wenzao walifanya. Mama alikuwa na uwezo kuwa hana sababu ya kusema akamilishe ile kazi, kwa sababu hakuna ambaye angekuwepo wa kumuhoji, lakini amefanya kwa sababu siyo mbinafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii na Bunge lako tukufu kumshukuru sana Mheshimiwa Rais na kumpongeza na kumtia moyo ya kwamba anaendelea kutengeneza *presidency* kubwa sana kwa wanawake kwamba tunao uwezo wa kuwa viongozi wazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Nilikuwa nikuongeze muda tu, lakini ulisema umemaliza, ahsante.

Sasa namwita Mheshimiwa Kitandula, ajiandae Mheshimiwa Mavunde.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili tuweze kuchangia kwenye hoja iliyoletwa na Kamati na nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye imempendeza kwamba wote tuko salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze kwenye hoja moja ambayo imeelekezwa kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii na muda ukiruhusu nitachangia na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo hoja imetolewa na Mheshimiwa Tabasam kuhusiana na uchimbaji wa madini kwenye maeneo ya hifadhi. Nataka nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa maono yake na miongozo yake kuhusiana na jambo hili ambalo linaenda kuwawezesha Watanzania kunufaika na rasilimali ya madini ambayo yanapatikana kwenye maeneo yetu ya hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nikimpongeza kwa hilo, nataka nitumie fursa hii vilevile kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa miongozo yake kwenye jambo hili na kwenye kuliendea jambo hili. Mheshimiwa Rais ametupa maelekezo mahsusi kwamba jambo hili lazima tuliendee kwa umakini mkubwa, lazima jambo hili lituongoze kwa kutumia taaluma ya wataalam wetu ili tusije tukaliingiza Taifa kwenye matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 32 ya ardhi ya nchi yetu ni maeneo ya hifadhi yaliyotengwa kwa mujibu wa sheria. Unapokuwa na eneo kubwa kama hili katika nchi ambalo tumekuwa na uthubutu wa kulitenga na kulilinda kisheria katika zama hizi za mabadiliko makubwa ya tabianchi ambayo yanaitesa dunia, kama nchi lazima tujipige kifua kwamba tumethubutu kufanya jambo kubwa. Tungeweza kutoshughulika na jambo hili, tukaruhusu kila kitu kikawa shamba la bibi, mwisho wa siku jamii ya sasa ingenufaika lakini kizazi kinachokuja kingekuwa kwenye matatizo. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kutupa maelekezo haya kwamba tuliendee jambo hili kwa umakini mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunapozungumza, mito yote mikubwa inatoka kwenye misitu ambayo tumeihifadhi. Kwa hiyo, kwenda kucheza na misitu hiyo ni kuhatarisha usalama wa Taifa letu. Ni kwa kutambua haya ndio maana Mheshimiwa Rais amesema katika kuliendea jambo hili tusiende nalo kwa pupa, lazima tuchukue hatua za kujiridhisha kwamba hayo maamuzi tutakayofanya hayatatuingiza kwenye matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi kusema katika miongozo hiyo tuliyopewa wataalamu wetu wametushauri, maeneo yameshabainishwa ambayo tunaweza kwenda kufanya shughuli hii ya uchimbaji wa madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Madini, Wizara ya Nishati wamekwishakutana mara kadhaa kuona jinsi ambavyo jambo hili linaweza kushughulikiwa. Mheshimiwa Rais aliagiza kwamba tusichimbe kiholela kwamba kila aina ya madini tuende tukachimbe, hapana. Amesema lazima yawe ni madini ya

kimkakati, madini ambayo yanaweza kuiletea Taifa hili faida kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa madini wamekwisha ainisha aina ya madini ambayo ni vizuri twende tukayachimbe, madini ya kimkakati. Sasa wakati tunakamilisha taratibu hizi lakini na Bunge linajua kwamba misitu hii na maeneo haya ya hifadhi yanalindwa kwa mujibu wa sheria. Zipo taratibu lazima zifanyiwe kazi, zipo sheria lazima zibadilishwe, kazi inayofanyika sasa ni kuainisha ni sheria zipi, ni taratibu gani zifanyiwe marekebisho na mwisho wa siku lazima hayo maamuzi yaletwe kwenye Bunge hili. Waheshimiwa Wabunge mtakuwa sehemu ya kufanya maamuzi hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwasihi sana Waheshimiwa Wabunge tusiende kwenye jambo hili kwa pupa, twende kwa tahadhari kubwa, kwa sababu tunaona yapo maeneo hatukuyashughulikia vizuri, leo hii yanatutesa. Leo hii tunapozungumza tumeruhusu shughuli za kibinadamu kwenye maeneo ya hifadhi zetu, lakini kwenye maeneo ya shoroba zetu na matokeo yake leo hii tuna changamoto kubwa ya wanyama wakali na waharibifu na kwa bahati mbaya maisha ya watu wetu wakati mwingine yanapotea. Bunge hili lina kazi ya kuhakikisha tunalinda uhai wa Watanzania. Tusiliendee jambo hili kwa pupa, tupate muda wa kutafakari na kufanya maamuzi sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Mavunde, Waziri wa Madini na baada ya hapo atakuja *Deputy Prime Minister* na Waziri wa Nishati, Dkt. Biteko.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi na mimi naomba nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetuwezesha kufika hapa siku hii ya leo. Kipekee kabisa nichukue fursa hii kuishukuru sana Kamati ya Nishati na Madini ikiongozwa na Mwenyekiti wake Dkt. Mathayo na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Kilumbe na Wajumbe wote kwa michango, miongozo na ushauri wao ambao

umetuwezesha kuweza kufanya kazi hii kwa weledi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kipekee pia nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu kwa maono na ushauri wao na maelekezo yao katika utekelezaji wa majukumu ndani ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja za Wajumbe zimesemwa kwa kiwango kikubwa na eneo la kwanza ambalo limechangiwa kwa kiwango kikubwa ni eneo la utafiti wa kina ili kuweza kubaini rasilimali madini ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi wamechangia kwamba Serikali iendelee kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kufanya utafiti wa kina na sisi kama Wizara ndio maana tulikuja na mkakati wetu ule ambao tumeuita "*Vision 2030* Madini ni Maisha na Utajiri."

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo lake kubwa ni kuendelea kubaini maeneo ambayo yana madini na kuwaongoza wachimbaji wetu vizuri kuliko ambavyo ilivyo hivi sasa ambavyo asilimia kubwa wanapoteza mitaji na nguvu kubwa kwa kuchimba kwa kubahatisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo niliambie Bunge lako kwamba moja kati ya maeneo ambayo tutayawezesha kwa kiwango kikubwa ni pamoja na Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini *(GST),* kwanza kwa kuhakikisha kwamba tunawajengea uwezo wataalamu waliopo pale, kwa maana ya nguvu kazi; lakini la pili ni kuendelea kuhakikisha ya kwamba tunakuwa na maabara ya kisasa ambayo itasaidia pia kutoa huduma katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni kuhakikisha ya kwamba tunaendelea kuongeza fedha kwa maana ya bajeti ili *GST* aweze kufanya kazi hii kikamilifu. *GST* ndio moyo wa Wizara ya Madini, wao ndio ambao watatuongoza vyema na tumeanza

vizuri. Kwa hivi sasa baada ya tangazo lile la *Vision 2030* tulipata wadau ambao walijitokeza kuja kushirikiana nasi katika eneo la utafiti wa kina kwa maana ya *High Resolution Airborne Geophysical Survey* na tumeanza baadhi ya maeneo na mwezi huu wa pili tutaendelea na maeneo mengine mawili; eneo ambalo tutakwenda kufanya utafiti wa kina ni eneo la mikoa ya Kusini kwa maana ya Mtwara na Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tumeweka eneo la Mirerani pale ambapo panachimbwa *Tanzanite* kama eneo mahsusi ambalo pia nalo tutakwenda kufanya utafiti wa kina ili tuweze kubaini madini yaliyopo katika eneo hilo kwa sababu hivi sasa tunafahamu asilimia kubwa wamejikusanya katika eneo moja wakiamini madini yote ya *Tanzanite* yako hapo, lakini tunaamini tukifanya utafiti wa kina itatupa wigo mpana zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hoja hiyo tumeipokea, lakini sambamba na hilo Taasisi yetu ya Utafiti ya *GST* hivi sasa ipo katika ushirikiano mkubwa na mashirika ya utafiti ya kutoka Finland ambayo ni *GTK* na kule Uingereza ya *BJS*, ni sehemu ya mashirikiano ili mwisho wa siku tuweze kufanya kazi hizi kwa pamoja kwa kupata pia ushauri na kujengewa uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni eneo ambalo limesemwa hapa la uboreshwaji wa sheria na kanuni na hili lina lengo kubwa kuhakikisha kwamba tunakuwa na usimamizi mkubwa wa shughuli za madini. Vilevile pia imelenga hasa katika kurahisisha ufanyaji wa biashara ya madini ya vito hasa *Tanzanite* kwa kufanya marekebisho ya sheria na kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitushauri kuzipitia sheria hizi na taarifa njema tu ni kwamba katika Bunge linaloendelea hivi sasa Muswada wa Marekebisho ya Sheria ambayo yataingia ni pamoja ikiwa na marekebisho ya Sheria ya Madini Sura ya 123 na ambayo katika eneo hilo pia litagusa mambo ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyapendekeza kwa kiwango kikubwa likiwemo hili suala la uanzishaji wa minada na vilevile maonesho katika madini ya *Tanzanite*.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo limezungumzwa ni huduma kwa wachimbaji wadogo; jukumu hill la ulezi wa wachimbaji wadogo lipo chini ya *STAMICO* na kama ambavyo wote tulishuhudia *STAMICO* inaendelea kuwalea wachimbaji wadogo kwanza kwa kuendelea kuwajengea uwezo na hivi sasa inawasimamia katika uanzishaji wa Benki ya Wachimbaji Wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo pia *STAMICO* hivi sasa anafanya kazi ya kutoa huduma kupitia mitambo ya uchorongaji ambapo mwaka jana tulishuhudia Mheshimiwa Rais akikabidhi mitambo mitano ya uchorongaji na ikifika Juni mwaka huu tutakuwa na mitambo zaidi ya 15 ya uchorongaji. Lengo lake kubwa ni kwenda kuwahudumia wachimbaji wadogo na mitambo hii itasaidia katika kutoa huduma kwa wachimbaji wadogo kwa gharama nafuu kuliko ambavyo ilivyo hivi sasa gharama ya uchorongaji ni kubwa sana na wachimbaji wadogo wengi hawawezi kumudu gharama hii. Hivyo kupitia huduma hii kupitia *STAMICO* wachimbaji wengi zaidi watapata huduma hii ya uchorongaji na itakuwa pia ni sehemu ya kuwasaidia kuweza kuwainua kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo kwenye kuwasaidia wachimbaji wadogo kupata mitaji. Mwaka jana mwezi Oktoba tulifanya kikao na benki zote 42 na taasisi za fedha pale Dae es Salaam. Lengo kubwa lilikuwa ni kuzungumza namna bora ya kuweza kusaidia upatikanaji wa mitaji kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kazi hii inakwenda vizuri. Ninavyozungumza hivi sasa baadhi ya benki zimeonesha nia ya kushiriki nasi katika eneo hili na hivi sasa ziko baadhi ya benki ambazo zimeanza kutoa mikopo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mitambo kwa wachimbaji wadogo na hasa katika mitambo ya uchenjuaji ile ya *CIP*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo limesemwa ni eneo la fidia; eneo hili limesemwa kwa kiwango kikubwa sana. nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba kama Wizara tutaendelea kusimamia ulipaji wa fidia wa wananchi kupisha miradi mikubwa ya madini kama inavyosemwa kwenye Sheria yetu na hasa kifungu cha 95 mpaka 97 ambacho kimetoa

sharti la lazima la mwenye hakimadini ahakikishe ya kwamba anakamilisha zoezi la ulipaji wa fidia ili aendelee na shughuli zake za uchimbaji wa madini. Kazi hii sisi kama Wizara tunaendelea kuisimamia kuhakikisha kwamba wananchi wetu wananufaika na rasilimali iliyopo na hasa katika eneo hili la ulipaji wa fidia kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, imezungumzwa hoja kuhusu *STAMICO* na miradi ambayo inaifanya. Mapendekezo yamekuja kwamba *STAMICO* sasa wajikite katika miradi ambayo itakuwa na tija na miradi mikubwa. Tunaupokea ushauri huu na niseme tu kwamba moja kati ya mkakati mkubwa tulionao hivi sasa ni sisi kushirikiana na Wizara ya Nishati kuhakikisha ya kwamba kupitia mradi wa makaa ya mawe tunaanza zoezi la haraka la uzalishaji wa umeme kupitia makaa ya mawe ambalo litakuwa na uwezo wa kuzalisha zaidi ya megawati 200 na tumeanza mazungumzo na *TANESCO*. Hii ni kati ya miradi mikubwa ambayo itakuja pia kusaidia upatikanaji wa nishati ya umeme hapa nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo limesemwa ni eneo la maduhuli. Kamati imeleta mapendekezo na ushauri na sisi tumeupokea tutaendelea kuboresha ili tukusanye maduhuri hayo ya kutosha kuweza kusaidia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Moja kati ya mkakati tunaoufanya katika eneo hili ni hasa kuhakikisha kwamba tunaendelea kuhamasisha shughuli za madini kufuata taratibu na hasa katika kupitia vituo vyetu vya ununuzi na masoko ya madini yaliyopo ili Nchi iweze kunufaika na tuweze kukusanya maduhuri ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, imezungumzwa hoja hapa ya kuhusiana na Mradi wa Uchimbaji wa Madini pale Nyanzaga na ilikuwa ni swali kwamba lini mradi huo utaanza kufanya kazi? Kama ambavyo itakumbukwa kwamba katika mradi huu ni mradi wa uchimbaji wa madini ya dhahabu ambapo unamilikiwa kwa pamoja kupitia Kampuni ya Ubia ya Sotta; Serikali ikiwa ina 16% lakini vilevile na Kampuni ya *Nyanzaga Corporation* ikiwa na 84%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa kuna changamoto hivi sasa ya Kampuni ya *OreCorp* ambayo imeendelea kuwa na

mazungumzo na Kampuni ya *Silvercorp Enterprises* kwa ajili ya kuona namna ambavyo wanaweza wakauziana *share* wao ambayo haiwezi kuathiri umiliki wa Serikali. Sisi kubwa ambalo tumewasisitiza ni kwamba ile *workplan* ambayo wameiweka ya kuanza mradi huu nusu ya pili ya mwaka 2025 ibaki pale pale. Nimshukuru sana Mheshimiwa Tabasam amekuwa akilifuatilia sana jambo hili na amekuwa mtu ambaye ana msaada mkubwa sana kwenye kuhakikisha kwamba mradi huu unakamilika, ninaamini hata wananchi wake watanufaika sana mradi huu ukianza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Serikali tutahakikisha ya kwamba tunasimamia makubaliano haya yaliyowekwa kwa maana ya *workplan* ya mwaka 2025 kazi ya uzalishaji ianze na Nchi iweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nilitaka nilisemee ni eneo la *local content* na urejeshaji kwa jamii, imesemwa hapa hoja juu ya jamii kunufaika na uchimbaji wa madini. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba kama Serikali tutaendelea kusimamia ili wananchi wengi zaidi waweze kunufaika na rasilimali madini katika masuala ya urejeshaji kwa jamii pamoja na kushiriki moja kwa moja katika kutoa huduma na usambazaji wa bidhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante; sasa namwita Mheshimiwa *Deputy Prime Minister* na Waziri wa Nishati Mheshimiwa Dkt. Biteko, karibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwanza kwa kunipa nafasi lakini nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kuwepo hapa Bungeni leo na kutupa nafasi ya kumsikiliza mtoa hoja Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Mheshimiwa Dkt. David Mathayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nichukue nafasi hii vile vile kwa sababu ya muda na ninajua anayepaswa kuja kuhitimisha hoja hapa ni mtoa hoja wetu Mwenyekiti wetu wa Kamati; kwa kweli kwa moyo wa dhati nimshukuru na kumpongeza sana kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuisimamia Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe utakuwa shahidi; waswahili wanasema, "Isiyo kongwe haivushi." Mheshimiwa Mathayo ukongwe wake na uzoefu wake kwenye kusimamia masuala mbalimbali siyo tu tunayaona kwenye Kamati lakini hata kwenye maisha yake binafsi tunapokutana naye. Ndiyo maana sikushangaa kabisa nilivyoona wakati anakuja kuwasilisha hoja, Waheshimiwa Wabunge kwa sababu wanamfahamu walipiga makofi mengi sana na mimi ni miongoni mwa watu ambao wamempigia makofi sana leo kwa sababu najua uwezo wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru sana vilevile Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Kilumbe pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano na maelekezo ambayo wanatupa kama Wizara kwenye kusimamia suala muhimu la nishati kwenye Nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wamechangia mambo mbalimbali na kwa sababu ya muda pengine nisingeweza pia kupata nafasi ya mimi kuchangia kwa sababu na mimi hapa ni mchangiaji lakini ninaweza kupata nafasi ya kuzungumza machache kati ya mengi waliyoyazungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza wamezungumza suala la umeme. Suala la umeme linawakera Waheshimiwa Wabunge, linawakera wananchi, linamkera Mheshimiwa Rais wetu na kwa kweli linatukera Wizara. Ninachotaka kusema hapa tunaweza kuwa na mipango mizuri sana ya kukabiliana na changamoto ya umeme lakini muhimu sana hapa ni lazima kujua kwanza sababu ya changamoto hii ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu hiyo wanaifahamu Waheshimiwa Wabunge, sababu ya kwanza upungufu wa

umeme na sababu ya pili ni miundombinu tuliyonayo ya kusafirisha huo umeme. Sasa Serikali imefanya juhudi kubwa; kwanza kwa kuangalia mawanda mapana ya *energy mix* (vyanzo vyetu vya kuzalisha umeme) vinahali gani. Ndiyo maana utaona tutazungumza mambo yote, hatua ya awali tunayokuja kuzungumza tutalitaja Bwawa la Mwalimu Nyerere kama suluhu ya kwanza ya muda mrefu kwa kipindi ya kutusaidia tatizo la upungufu wa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza hapa leo upungufu wa umeme tulionao, tulikuwa kama mwezi Septemba tulikuwa na upungufu ambao ulikuwa unaelekea *megawatt* 400. Ninafurahi kusema kwamba baada ya mvua kunyesha, ukarabati wa mitambo, kuongeza gesi kwa maana ya mgandamizo wa gesi, upungufu huo umeendelea kupungua. Hivi ninavyozungumza hapa kwa leo tuna upungufu wa *megawatts* 193 kwenye Gridi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya upungufu huu pamoja na kingine kilichotajwa na Waheshimiwa Wabunge kwamba kisingizio kilikuwa ni mvua. Ni kweli kwamba mabwawa tuliyokuwa tunayatumia kwa ajili ya kuzalisha umeme yalikuwa yameshuka sana kiwango cha maji. Mfano leo tunapata bahati kwamba ongezeko hilo tunaloliona linalodhibiti upungufu linatokana na kuongezeka kwa maji kwenye mabwawa hayo. Mtera kwa mfano ambayo ilishuka mpaka ikafika mita 689 kwa taarifa ya leo tumeshafika mita 695, bado mita tatu tufike kwenye kiwango cha juu kabisa cha uzalishaji wa umeme kwenye Bwawa letu la Mtera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Lulida na Waheshimiwa Wabunge wengine; Waheshimiwa Wabunge, upungufu huu utasababishwa vilevile na ikolojia tuliyonayo kwenye vyanzo vyetu vya maji. Sisi kama Serikali hatujakaa pembeni na kulalamika; *TANESCO* kama mshirika mkubwa wa mabwawa haya tumeamua tuwe mbele kwenye kusimamia mazingira na vyanzo vya maji ili tuvipe uhakika vyanzo vyetu vya maji ili tatizo hili tunaloliona leo lisiweze kuwa la kujitokeza kila baada ya muda. Ndiyo maana tumetengewa na Bunge lako kuanzia sasa tutakuwa na shilingi bilioni tano pamoja

na mamlaka nyingine za Serikali kwa ajili ya kufuatilia vyanzo vyetu vya maji kuwe na maji ya uhakika hasa kwenye maeneo ya Mtera na Julius Nyerere ili kusiweze kukauka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa miundombinu tunafahamu Waheshimiwa Wabunge tunayo changamoto ni lazima tukubali kuwekeza. Uwekezaji kwenye miundombinu ya umeme siyo jambo la leo kesho linatokea. Ni kweli tunakiu kwamba matatizo haya yatoke leo lakini ni ukweli pia kwamba tunahitaji muda kwa ajili ya kuwekeza na kusimamia hiyo miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kujenga *line* moja ya umeme siyo chini ya miezi 12, *line* ya kusafirisha umeme mwingi lakini Nchi hii tuna vituo vya kupoza umeme pungufu na mahitaji tunayohitaji. Tunahitaji kwa Nchi nzima zaidi ya vituo vya kupozea umeme 231 lakini tuna vituo hivyo 171. Alichokizungumza Mheshimiwa Musukuma na Wabunge wengine kwamba kuna *line* ndefu sana zinazohudumia wananchi. Kukitokea hitilafu mahali fulani hata kama ni tawi likaanguka litawatoa wananchi wengi sana kwenye Gridi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali inafanyia kazi. Tumepata fedha na tunashukuru sana Serikali na Mheshimiwa Rais ameweka msukumo mkubwa tunajenga vituo hivyo na tunabadilisha *line* nyingine za zamani kuweka *line* kubwa zaidi. Ningeweza kuzitaja *line* kwa *line,* vituo kwa vituo lakini kwa sababu ya muda ninachelea nisije nikapoteza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna tatizo la *vandalism* (uharibifu wa miundombinu). Nitawapa mfano Waheshimiwa Wabunge, kwa mfano Kanda ya Pwani (Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani) kuna changamoto kubwa ambayo tunahangaika nayo kwa sasa; hata hizi transfoma tulizonazo katika kipindi kifupi zaidi ya transfoma 87 zimeibiwa. Katika 87 hizo ikiibiwa itawatoa wananchi wengi sana kwenye umeme lakini wananchi watakachokiona ni kwamba ni tatizo la *TANESCO*. Nataka niwahakikishie kwamba wale wote wanaodhani kwamba wataendelea na mchezo wa kuiba transfoma, kuhujumu

transfoma siku zao zinahesabika na wakitaka kujua hilo wawaangalie wale ambao tumewakamata hatua gani zinachukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije kwenye suala la gesi. Ni kweli kwamba tunahitaji gesi kwa ajili ya kuzalisha umeme lakini ni ukweli vilevile kwamba mgandamizo wa gesi umepungua. Tumefanya nini kwa ajili ya kuhakikisha hilo jambo linakwisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, mmeona hata juzi tulieleza kule Madimba tunafanya utaratibu wa kuongeza *compression* ya gesi na fedha zimeshapatikana. *TPDC* pamoja na *MNP* wanafanya kazi ya kujenga ule mradi kuongeza kiasi cha gesi kiweze kutusaidia. Vilevile mradi wa Ntori ambao ulisubiri kwa muda mrefu na wenyewe tunajenga bomba jingine la kuongeza gesi kwenye *pipe* yetu tupate gesi nyingi zaidi ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, muhimu sana hatujaacha miradi mingine inayokuja ambayo tunahitaji umeme zaidi. Ni kweli alivyosema Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwamba pamoja na Julius Nyerere kuwepo itatupa *brief* ya muda fulani, baada ya muda huo umeme hautatosha na hautatosha kwa sababu gani? Tunaongezeka kwa idadi ya watu, viwanda vinaongezeka na wachimba madini na wao wamejua kutumia umeme kila mahali. Kwa hiyo, utaona mahitaji ya umeme yanaongezeka kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunamiradi ambayo tunaendelea nayo ndiyo maana mtaona tumesaini Malagarasi sasa hivi kwa ajili ya kujenga Mradi wa Malagarasi ambao toka mwaka 1982 unasubiri. Ruhuji na Rumakali miradi yote hiyo tunaijenga kwa ajili ya kuongeza *energy mix* na hata kwenye *renewables* tumeanza kujenga mradi mkubwa wa *solar* kule Kishapu wa *megawatts* 150. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaanza kujenga miradi vilevile tunakamilisha mazungumzo kwenye miradi ya upepo ili na yenyewe iweze kuingia kwenye Gridi. Tunaangalia kila mahali ambapo tunadhani tunaweza kupata hata kama ni *megawatt*

moja iwepo kama chanzo itupe uhakika, itupe nafasi ya kufanya matengenezo kwenye miundombinu tuliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kuna wakati huwezi hata kutengeneza miundombinu; kwa nini? Mahitaji ya umeme uliyonayo na uwezo wa kuzalisha vipo pale pale tena vinatofautiana. Kwa mfano Pangani tulipata tatizo maji yakaingia kwenye mgodi Pangani nzima ikaenda *off*. Ilivyokwenda *off* maana yake ni nini? Mkoa wa Tanga, Kilimanjaro pamoja na Arusha ikaathirika. Kutengeneza kile kituo kimoja imewachukua zaidi ya wiki tatu kwa sababu ni mgodi maji yameingia kule chini, kituo kizima kimeanguka hakiwezi kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema ni kwamba Serikali inafanya kila linalowezekana kutuondoa kwenye hii changamoto. Mambo mengine yatahitaji muda lakini mambo ya muda mfupi tunayo tunayafanyia kazi. Tukubaliane pia kwamba kuna wakati mwingine wataona umeme unakatika siyo lazima kwamba kuna upungufu wa umeme wakati mwingine ni miundombinu inapotokea shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano wakati mvua zinaponyesha, Mikoa ya Katavi hata Mikoa ya Kaskazini lakini Dar es Salaam kuna mahali ambako mvua imepeleka nguzo kubwa zinazosafirisha nyaya. Wakati mwingine niliona vijana wetu wenyewe wa *TANESCO* wanabeba nguzo kwenye matoroli ya punda; kwa nini? Hata barabara yenyewe ya kufikia kwenye eneo la kwa ajili ya ku-*rescue* hawawezi kufika lakini wanafanya kila wanachoweza kuhakikisha kwamba tunafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, uzembe ndani ya Shirika letu la *TANESCO* hauwezi kuvumiliwa. Inawezekana tusitangaze tumechukua hatua gani. Tunachukua hatua za ndani kila inavyoitwa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu yeyote ambaye anatukwamisha mahali fulani tunahakikisha kwamba yeye anakwama kwanza kabla ya wananchi kukwama; wananchi wanachotaka ni umeme. Ningeweza kuzungumza idara kwa

idara tumefanya maboresho ya namna gani siyo muhimu kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwahakikishie kwamba tumepewa maelekezo na Mheshimiwa Rais, tumepewa maelekezo pamoja na Kamati hii ambayo imetoa hoja hapa kwamba tukashughulike na matatizo ambayo ni udhaifu wa kiusimamizi yabaki yale ambayo yana sababu za kujieleza lakini kama kuna mtu anatukwamisha basi tuone namna gani tunashughulika naye kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nataka kumalizia tu kwamba kwa wakandarasi wetu wa umeme vijijini, nimemsikiliza Mheshimiwa Ndaisaba na Wabunge wengine. Mkandarasi yeyote ambaye hajamaliza mradi kwenye miradi hii inayokuja hatumpi kazi. Hilo lilishazungumzwa na mimi sitanii. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tume-*take stock* wakandarasi ambao wana-*underperform* wote wale hatuwezi kuwapa mardi mwingine. Tutashughulika na wale ambao wanaweza kufanya kazi hao tuwape kazi nyingine ili waweze kufanya kazi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunavyozungumza tunamalizia vijiji tuko 95%. Tunakwenda kwenye vitongoji, tuna vitongoji 64,000 tumeshaweka vitongoji 32,000. Hivi ninavyozungumza vitongoji tuna 50.1% tumepeleka umeme. Kuna changamoto moja ya kuamini kwamba uememe ukifika mahali fulani basi siku hiyo hiyo utaenea kila mahali. Tupeane muda kwa sababu kazi ni umeme ufike mahali fulani halafu inakuja hatua ya pili ya kuwapelekea wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la *connectivity* ni jambo la muda mrefu. Hata Dar es Salaam Waheshimiwa Wabunge; Dar es Salaam pamoja na kwamba tuna umeme kila mahali lakini asilimia karibu 80 ya wananchi wa Dar es Salaam hawajaunganishwa na umeme. Huwezi kusema kuwa Dar es Salaam haina umeme. Kwa hiyo, tupeane muda tuweze kulifanya hili jambo na ninataka niwahakikishie kwamba Waheshimiwa Wabunge tunalifanyia kazi kwa nguvu zetu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuzungumzia mambo ya *flow meter* Mheshimiwa Tabasam amelizungumza. Ninakushukuru sana kwamba *flow meter* unayoizungumza Mheshimiwa Tabasam tayari tumeshaibadilisha. Tuna *flow meter* na ninataka niwakaribishe Waheshimiwa Wabunge na Kamati yote kama mtapata nafasi muende mkaone upakuaji wa mafuta unavyofanyika kwa kasi. Tutaongeza vilevile miundombinu mingine ya kupakua mafuta ili tuweze kuwaongezea kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mama Lulida amezungumza kwa uchungu sana kwamba haya mambo mnayafanya ya gesi lakini mnafanyia Dar es Salaam na Dodoma. Nakubaliana na yeye, nimeenda mwenyewe Mtwara na Lindi. Kuna wakati wananchi wanavyolalamika malalamiko yao pengine ni katikati ya mawasiliano yetu. Wananchi kwa sababu hawajui tunasababisha wanaona kama hatufanyii kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano tulisaini Mradi wa Ntorya, kwa sababu yule tuliyempa nafasi ile ni lazima tusaini ili aende akafanye *financing.* Muda ulikuwa hautoshi ku-*mobilise* watu kule Mtwara kwa ajili ya kufanya hiyo shughuli isingetosha. Tukakubaliana tukutane mahali pengine nje ya Mtwara. Nataka nikuombe mama, yangu tunakuja Mtwara hatuji kwa sababu ya miradi ya gesi vilevile tunakuja na mradi wa kufunga mtambo mpya wa kuwapatia umeme watu wa Lindi na Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiingii akilini watu ambako gesi inatoka wao umeme wao ni wa mashaka. Tumeamua kuchukua mtambo Ubungo tunawapelekea watu wa Mtwara na tayari hivi ninavyozungumza mtambo umefika. Kuna watu walituletea Sayansi haiwezekani sijui utaratibu gani, tukawaambia pelekeni mtambo tutakutana na matatizo hayo mbele ya safari ili wananchi wa Mtwara waweze kupata umeme. Mheshimiwa Lulida pamoja na Wabunge wa Mtwara na Lindi nataka niwahakikishie kwamba tunakuja Mtwara tutawaambia na mipango tuliyonayo kwenye gesi ya kubadilisha hata *lively hood* ya watu wa Mtwara ambako gesi inatokea wafanane na gesi wanayoichimba kwa sababu hayo ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie tena kuwaomba Waheshimiwa Wabunge; Mheshimiwa Getere jambo la *transformer* nalichukulia kwa uzito mkubwa. Nataka nikuhakikishie, baada ya hapa tukutane nitakupa mpango wote wa kupeleka lile *transformer* kwa ajili ya kufanya marekebisho hayo. Maeneo mengne haya; Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge tunaomba tena tumpongeze sana kwa usimamizi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini najua pamoja na taarifa aliyowasilisha hapa na mapendekezo aliyotuletea hapa sisi kama Wizara ya Nishati tutayachukua yote kwa ajili ya kuyafanyia kazi. Nisingependa kusema kama nahitimisha hoja kwa sababu yeye atakuja na maelekezo maalum ya Bunge mimi nayasubiri tuweze kuyachukua kwa ajili ya kwenda kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nawashukuru sana wajumbe wa Kamati na nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kweli kwa kuwa na uchungu na suala la umeme wa nchi yetu. Nataka niwakikishie kwamba tuko karibu na mwisho hili jambo litapungua kwa kiasi kikubwa. Kuna maeneo mengine yanahitaji muda kujenga *line* kunahitaji muda na kubadilisha *conductor* kunahitaji muda; lakini nataka niwakikishie cha kwanza cha ku-*solve* ni kuwepo kwa umeme. Tukipata jambo la uwepo wa umeme unaokidhi haja jambo la usafirishaji na usambazaji ni jambo la pili ambalo tutaendelea nalo kila wakati. Baada ya kusema hayo nakushukuru kwa nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa maneno ya faraja na matumaini makubwa ya kuendeleza Uchumi wa Taifa letu, ahsante sana. Sasa namuita mtoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya jamani ahsanteni, Mheshimiwa. *(Makofi)*

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuhitimisha hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini. Hoja hii imepata wachangiaji wa kuzungumza 16 wakiwemo

Waheshimiwa Wabunge 13 na Waheshimiwa Mawaziri wawili na Mheshimwia Naibu Waziri Mkuu. Naamini pia kutakuwa na waliochangia kwa njia ya maandishi. Baadhi ya maeneo ambayo yamechangiwa na wengi yamegusia pamoja na mambo yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, uchimbaji na matumizi ya gesi asilia, upatikanaji wa umeme nchini na utunzaji wa miundombinu yake. Umuhimu wa Serikali kuanzisha vyanzo mbadala vya umeme kama vile joto ardhi, umeme wa jua na kadhalika. Usambazaji wa umeme vijijini kupitia *REA*, usimamizi wa sera, sheria na kanuni kuhusu wajibu wa mmiliki wa leseni za madini kwa jamii *(Corporate Social Responsibility)* na *local content.*

Mheshimiwa Naibu Spika, *STAMICO* kujielekeza katika miradi mikubwa badala ya miradi midogo midogo. *STAMICO* kusaidia utafiti kwa wachimbaji wadogo, biashara ya mafuta, ulipaji wa fidia katika maeneo ya uchimbaji wa madini na kadhalika. Kwa dhati ya moyo wangu napenda niwashukuru sana wachangiaji wote waliojitokeza kwani wamesaidia kufafanua na kuifanya hoja ya Kamati ieleweke vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha napenda kumshgukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kutoa ufafanuzi mzuri, na napenda kumshukuru sana Waziri wa Madini kwa kutupa ufafanuzi katika mambo mbalimbali ambayo yamejitokeza kwenye ripoti. Vilevile, si mwisho kwa umuhimu, namshukuru sana Naibu Waziri Mkuu kwa kutoa maelezo ya kina ambayo yanatupa matumaini makubwa sana katika upatikanaji wa umeme na mambo mengine yanayohusu Wizara yake. Kusema kweli sisi Kamati tunafurahia sana kufanya kazi na Wizara hizi mbili wakiongozwa na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu pamoja na Waziri wa Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu orodha ya wachangiaji ni chache, na kwa sababu naona muda unanitosha naomba tu niwasome kwa haraka haraka majina sekunde ishirini hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni pamoja na Mheshimiwa Kilumbe ambaye ni Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Musukuma Joseph Kasheku, Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa *Engineer* Samweli Xaday, Mheshimiwa Aleksia Kamguna, Mheshimiwa Zacharia Issaay, Mheshimiwa Tabasam Mwagao, Mheshimiwa Regina Ndege, Mheshimiwa Martha Mariki, Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mheshimiwa Mwita Getere, Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mheshimiwa Dustan Kitandula, Mheshimiwa Anthony Mavunde na Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nahitimisha hoja hii kwa kuweka msisitizo kwenye mapendekezo ambayo Kamati imeyatoa ili Bunge lako Tukufu liweze kuyaazimia na Serikali ikayatekeleze kwa manufaa ya Taifa letu na ustawi wa wananchi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Mapendekezo ya Jumla, Kusuakusua kwa Utekelezaji wa Bajeti (Ukusanyaji wa Maduhuli).

Kwa kuwa, ukusanyaji wa maduhuli kama ilivyoidhinishwa na Bunge katika Wizara zote mbili uko chini ya lengo kwani hadi Disemba 2023 ukusanyaji ulikuwa wastani wa asilimia 32.08 ya lengo.

Na kwa kuwa, hali hiyo inachangia kukwamisha Wizara na taasisi zake kutekeleza kikamilifu na kwa wakati shughuli mbalimbali zilizopangwa kutekelezwa katika kipindi hicho na hivyo kuathiri matarajio ya wananchi ya kupata huduma bora kutoka katika Wizara hizo na taasisi zake.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Seikali ihakikishe kunakuwa na mikakati madhubuti itakayowezesha ukusanyaji wa maduhuli kutekelezwa kikamilifu ili kutoathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa na Wizara na taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusuasua kwa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;

Kwa kuwa, utekelezaji wa baadhi ya miradi unasuasua ikiwemo Mradi wa Kinyerezi *One Extension Mega Warts 185,* Mardi wa Musambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili, Mradi wa Kuzalisha Mkaa Mbadala wa Kupikia (Kiwira na Kisarawe) na Ujenzi wa Ofisi ya Tume ya Madini Dodoma.

Na kwa kuwa, kusuasua huko kunasababisha ongezeko la gharama na utekelezaji wa miradi hii kukosesha wananchi huduma iliyotarajiwa kutokana na miradi hiyo na kuathiri utendaji katika taasisi ambazo zinatekeleza miradi hiyo.

Na kwa kuwa, kusuasua huko kunaendelea kuchochea uharibifu wa mazingira kwani wananchi wanakata miti kwa ajili ya kuni na kuchoma mkaa ambavyo pia vinaharibu na vinaleta athari kiafya.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali iharakishe utekelezaji wa miradi na ifanyike kikamilifu na kwa wakati na hivyo kuokoa ongezeko la gharama na kuwezesha wananchi kupata huduma tarajiwa kutokana na miradi hiyo na kupunguza uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Nishati, Utekelezaji wa Bajeti;

Kwa kuwa, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina hasa zile kutoka nje hauridhishi, kwani hadi kufikia Disemba 2023 upatikanaji ulikwa wastani wa asilimia 43 *(*Fedha za *IMF)* kutoka nje kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)* hazikupatikana kabisa.

Na kwa kuwa, hali hiyo inachangia Wizara na taasisi zake kushindwa kutekeleza kikamilifu majukumu yaliyopangwa na hivyo kuathiri huduma tarajiwa kwa wananchi kutoka katika Wizara na taasisi zake.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali ihakikishe: -

(a) Fedha zilizoidhinishwa kwa Wizara ya Nishati na taasisi zake zinapatikana kwa utoshelevu na kwa wakati.

(b) Serikali ijielekeze kutenga fedha kutoka vyanzo vya ndani ili kuepuka adha ya utegemezi wa fedha za nje ambazo mara nyingi hazipatikani kwa uhakika na kwa wakati, na;

(c) Serikali iboredhe mfumo wa ufuatiliaji wa fedha za nje zilizotengwa kwenye bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Usambazaji na Upatikanaji wa Umeme Nchini. *(Makofi)*

Kwa kuwa, hali ya usambazaji na upatikanaji wa umeme nchini siyo ya kuridhisha kutokana na ukame, uhaba wa gesi, uchakavu wa miundombinu na uchache wa vituo vya kupoza umeme;

Na kwa kuwa, hali hiyo inaathiri uzalisahaji wa bidhaa na huduma nchini na hivyo kuathiri ukuaji wa uchumi na kuchangia ongeeko la mfumko wa bei;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali ihakikishe:-

(a) Mradi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere unakamilika haraka na kuanza uzalishaji Februari mwaka huu;

(b) Serikali ihakikishe Mradi wa Kufunga Mtambo wa Kupoza Hewa *(Chillar)* katika Kituo cha Kinyerezi *One Extension* na kuongeza uzalishaji wa umeme kutoka *Mega Warts* 160 hadi 185 unakamilika ifikapo Disemba mwaka huu;

(c) Seikali kupitia *TPDC* iongeze uzalishaji wa gesi asilia katika visima vya Songosongo na Mnazi *Bay* ili kuongeza uzalishaji wa umeme, na;

(d) Serikali ihakikishe mitambo ya kuzalisha umeme inafanyiwa ukarabati wa mara kwa mara ili kuepuka uchakavu ambao unaathiri uwezo wamitambo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya mafutra kuwa Juu.

Kwa kuwa, bei ya mafuta imeendelea kuwa juu kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na uhabva wa fedha za kigeni, gharama za kubadoilisha fedha za kigeni, ukosefu wa maabara ya kupima ubora wa mafuta Bandari za Mtwara na Tanga na ufinyu wa maghala ya kuhifadhia mafuta;

Na kwa kuwa, hali hiyo inachangia ongezeko la mfumko wa bei kwenye bidhaa na huduma nchini hivyo kuchangia ongezeko la gharama za maisha na kuibua hisia na chuki miongoni mwa wananchi dhidi ya Serikali;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali ikamilishe: -

(a) Upanuzi wa miundombinu ya Bandari ya Dar es Salaam na ujenzi wa Maabara ya kupima ubora wa mafuta katika Bandari za Tanga na Mtwara ili kuongeza kasi na uwezo wa upatikanaji wa mafuta.

(b) Serikali ichukue hatua madhubuti ya kuhakikisha nchi inajitosheleza katika akiba ya fedha za kigeni hususan Dola za Marekani.

(c) Serikali ichukue hatua ili kuongeza uwezo wa maghala ya kuhifadhia mafuta na hivyo kuiwezesha nchi kuwa na mafuta ya kutosha, na;

(d) Serikali iiwezeshe *TPDC* kwa kuijengea mazingira wezeshi kibiashara ili iweze kushindana kwenye soko la ndani na nje ya nchi hivyo kuihakikishia nchi usalama wa mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la magari yanotumia gesi asilia *CNG* dhidi ya vituo vya kujaza vilivyopo.

Kwa kuwa, matumizi ya gesi asilia kwenye magari yameongezeka nchini kutoa magari 1,139 hadi kufikia magari

3,000 mwishoni mwa 2023 kutokana na unafuu wa kutumia gesi ukilinganisha na mafuta ya *petrol* na *diesel;*

Na kwa kuwa, ongezeko hilo linasababisha foleni kwenye vituo vitano vya kujaza gesi vilivyopo nchini na hivyo wenye magari kulazimika kutumia muda mwingi kujaza gesi.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba; Serikali iongeze idadi na mtandao wa vituo vya kujaza gesi kwenye magari nchini kwa kuanza na maeneo ambayo taratibu za awali za ujenzi zimeanza ambavyo ni Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma na vituo vya *GYPSA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Gharama na Uhaba wa Wakaguzi wa Mfumo wa Gesi Asilia.

Kwa kuwa, magari mengi yanayoingizwa nchini hayana mfumo wa kutumia gesi asilia hivyo yanalazimika kuwekwa mfumo huo iwapo mmiliki anahitaji.

Na kwa kuwa, baadhi ya wamiliki wa magari wanashindwa kuweka mfumo wa kutumia gesi asilia kwenye magari kutokana na gharama kuwa kubwa (2,000,000 kwa gari), uchache wa wakaguzi (wakaguzi wa mfumo hapa nchini wako 10) na uchache wa karakana ambazo ziko nne.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali: -

(a) Ichukue hatua zitakazowezesha kupunguza gharama za kufunga mfumo wa kutumia gesi kwenye magari;

(b) Serikali ichukue hatua zitakazosaidia kuongeza idadi ya wakaguzi kwa mfumo wa magari yanayotumia gesi asilia, na;

(c) Serikali ianze kuhamasisha uagizaji wa magari nchini yenye mfumo wa kutumia gesi asilia ili kupunguza gharama za kuweka mfumo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Madini, kusuasua kwa fidia kwa wananchi wanaopisha miradi ya uchimbaji wa madini.

Kwa kuwa, kumekuwa na ucheleweshaji wa fidia kwa wananchi wanaohama kwenye maeneo yao ili kuruhusu utekelezaji wa miradi ya uchimbaji wa madini;

Na kwa kuwa, hali hiyo inachangia kudidimiza wananchi kiuchumi kutokana na kutoruhusiwa kufanya shughuli za kimaendeleo na kijamii katika maeneo hayo na hivyo kujenga chuki dhidi ya wawekezaji;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali: -

(a) Isimamie kikamilifu suala la fidia na kuhakikisha wananchi wanalipwa kwa wakati ili kuondoa malalamiko dhidi ya Serikali na kuwakwamua dhidi ya athari za kiuchumi, kisaikolojia na kijamii;

(b) Serikali ihakikishe wawekezaji wanaweka fedha katika mfuko fidia ya ardhi kabla ya kuwaondoa wananchi katika maeneo yao jambo ambalo litawahakikishia wananchi hao kulipwa fidia na kwa wakati, na;

(c) Serikali ihamasishe wananchi kulipwa fidia kwa njia ya kupewa hisa huru katika miradi ya uchimbaji wa madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taaarifa ya utafiti wa madini kuwanufaisha wachimbaji wadogo na kuvutia wawekezaji.

Kwa kuwa, sehemu kubwa ya nchi (asilimia 84) haijafanyiwa utafiti wa teknolojia ya kisasa *(High Resolution Geophysical Survey)*

Na kwa kuwa, hali hiyo inasababisha uendelezaji wa leseni za madini kufanyika kwa gharama kubwa bila ya kuwa na uhakika wa taarifa za madini katika eneo husika jambo ambalo linachangia upotevu wa mitaji na uharibifu wa mazingira kutokana na uchimbaji wa kuhamahama.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali ihakikishe inatekeleza mikakati yake ya kuongeza eneo lililofanyiwa utafiti wa kiteknolojia ya kisasa *(High Resolution Geophysical Survey)* kutoka asilimia 16 hadi kufikia asilimia 50 ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uboreshaji waSheria na Kanuni katika Sekta ya Madini.

Kwa kuwa, badhi ya changamoto zinazoikabili sekta ya madini zinachangiwa na udhaifu kwenye baadhi ya sheria na kanuni ya sekta ya madini;

Na kwa kuwa, udhaifu huo unaathiri masuala mbalimbali ikiwemo usimamizi wa baruti, usimamizi wa biashara ya makinikia na uchenjuaji wa madini ghafi utaratibu wa masomo na maonesho ya kimataifa ya madini na biashara ya madini ya Tanzanite.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali iharakishe ukamilishaji wa mchakato wa: -

(a) Kutunga sheria ya usimamizi wa baruti nchini kwani iliyopo ni ya mwaka 1962 na imepitwa na wakati;

(b) Kufanya marekebisho ya sheria ya madini Sura 123 ili kuwezesha usimamizi wa biashara ya makinikia na uchenjuaji wa madini ghafi.

(c) Kurekebisha kanuni za eneo tengefu la Mererani ili kuruhusu biashara ya madini ya Tanzanite yaliyosanifiwa (yaliyochakatwa) kufanyika pia maeneo mengine ya nchi nje ya Mererani.

(d) Kutengeneza kanuni zitakazotoa mwongozo wa minada na maonesho ya Kimataifa ya madini hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa sera sheria na kanuni kuhusu wajibu wa mmiliki wa leseni za madini kwa jamii *(Corporate Social Responsibility)*.

Kwa kuwa, utoaji na upatikanaji wa huduma za kijamii *CSR* unasuasua kutokana na baadhi ya wamiliki wa leseni za uchimbaji wa madini kuchukua jambo hilo kuwa ni hisani jambo ambalo ni kinyume na wajibu wa wamiliki wa leseni za madini ya Mwaka 2023.

Na kwa kuwa, jambo hilo linachangia jamii zinazozunguka miradi ya uchimbaji wa madini kutonufaika na huduma za *CSR* kutoka kwa mwekezaji pamoja na kusababisha migogoro baina ya wawekezaji na jamii hizo.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali ihakikishe inasimamia kikamilifu utekelezaji wa Kanuni za Wajibu wa Wamiliki wa Leseni za Madini kwa Jamii ya Mwaka 2023 ili wamiliki wa leseni watimize wajibu wao kikamilifu na jamii husika ziweze kunufaika na uwekezaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasii hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Kuhudu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023 na Mapendekezo yake.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Nachukua nafasi hii kuishukuru Kamati kwa kazi nzuri mliyofanya kushirikiana na Wabunge wa Kamati yenu lakini lakini kwa michango muhimu ya Wabunge na kauli ya Naibu

Waziri Mkuu mikakati ambayo Serikali chini ya Mama Samia imeenda kuifanya kuhakikisha kuondokana na adha ya umeme. Safari bado ni ndefu lakini tutafika.

Sasa kuna tangazo muhimu. Naomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa Mheshimiwa Spika amefanya mabadiliko kidogo kwenye ratiba ya Mkutano wa 14 wa Bunge kama ifuatavyo: -

Siku ya Ijumaa tarehe 9 Februari, 2024 tutaanza na maswali, taarifa za Kamati, itakuja Kamati ya Maji na Mazingira na Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Kwa hiyo, Ijjumaa tutakuwa na Kamati mbili. Siku ya Jumatatu tarehe 12 Februari, 2024 tutakuwa na maswali, Taarifa za Kamati - Kamati ya Afya masuala ya Ukimwi na Kamati ya Viwanda Biashara, Kilimo na Mifugo. Kutakuwa na Kamati mbili siku ya Ijumaa halikadhalika na siku ya Alhamisi.

Ratiba yenye mabadiliko hayo inatumwa kwenye vishikwambi vya Waheshimiwa Wabunge muda huu. Mwenyekiti wa *Bunge Marathon* anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa Ofisi ya Bunge inaandaa tukio la mbio zijulikanazo kama *Bunge Marathon* lenye lengo la kupanua wigo wa ushiriki wa wadau na wananchi mbalimbali ili washirikiane kwenye uwakilishi wao Bungeni katika mbio hizo.

Tukio hilo litafanyika kwa mara ya kwanza jumamosi tarehe 13 *April,* 2024 Jijini Dodoma. Mbio hizo zinatarajiwa kuwa na washiriki 5,000 kutoka ndani na nje ya nchi, ikiwa ni mbio za umbali wa nusu *Marathon* (kilometa 21, kilometa 10 na kilometa 5). Mwananchi yeyote anaruhusiwa kushiriki kwa kuchangia shilingi 40,000 za vifaa vya kushiriki mbio hizo.

Aidha, hivi karibu mtajulishwa rasmi kuhusu taratibu za usajili na malipo kufanywa. Tukio hili pia linalenga kukusanya fedha zitakazotumika kuboresha huduma za kijamii hususan katika nyanja ya elimu kwa kujenga Shule ya Sekondari ya Wavulana *Bunge Boys Secondary School.* Hivyo, Waheshimiwa Wabunge, Watumishi wa Ofisi ya Bunge, wadau na wananchi mbalimbali

wanahimizwa kujiandaa kushirikiana na Ofisi ya Bunge katika tukio hili muhimu. *(Makofi)*

Aidha, Waheshimiwa Wabunge mnaombwa mkahamasishe wapiga kura wenu majimboni na pia kuwafadhili baadhi yao ili waweze kushiriki tukio hilo muhimu. Nawashukuru tena kwa kumaliza kazi ya Kamati hizi za Nishati na Madini leo, na sasa ni Taarifa Rasmi ya Bunge ambayo inakwenda Serikalini kufanyiwa kazi.

Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 8.23 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 7 Februari, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*